ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID	-	SPIKA
1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6. Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais

9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
11. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13. Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake
18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais

19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais
20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Mihayo Juma N'hunga	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa pili wa Rais wa Zanzibar/ Jimbo la Mwera
22. Mhe. Shamata Shaame Khamis	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ / Jimbo la Micheweni
23. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete
24. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani
25. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
26. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
27. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Naibu Waziri wa Uwezeshaji,Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake

28. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
30 Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
31. Mhe.Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
32. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe
33. Mhe. Ali Salum Haji	-	Jimbo la Kwahani
34. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)	-	Jimbo la Kijitoupele
35. Mhe. Ame Haji Ali	-	Jimbo la Nungwi
33. Mhe. Amina Iddi Mabrouk	-	Nafasi za Wanawake
37. Mhe. Asha Abdalla Mussa	-	Jimbo la Kiwengwa
38. Mhe. Bahati Khamis Kombo	-	Jimbo la Chambani
39. Mhe. Bihindi Hamad Khamis	-	Nafasi za Wanawake
40. Mhe. Hamad Abdalla Rashid	-	Jimbo la Wawi
41. Mhe. Hamida Abdalla Issa	-	Nafasi za Wanawake
42. Mhe. Hamza Hassan Juma	-	Jimbo la Shaurimoyo
43. Mhe. Hassan Khamis Hafidh	-	Jimbo la Welezo
44. Mhe. Hidaya Ali Makame	-	Nafasi za Wanawake
45. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa)	-	Jimbo la Mtoni
46. Mhe. Jaku Hashim Ayoub	-	Jimbo la Paje
47. Mhe. Khadija Omar Kibano	-	Jimbo la Mtambwe
48. Mhe. Machano Othman Said	-	Jimbo la Mfenesini
49. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti	-	Jimbo la Mtopepo
50. Mhe. Makame Said Juma	-	Jimbo la Kojani
51. Mhe. Maryam Thani Juma	-	Jimbo la Gando
52. Mhe. Masoud Abrahman Masoud	-	Jimbo la Bububu
53. Mhe. Miraji Khamis Mussa	-	Jimbo la Chumbuni
54. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha	-	Jimbo la Mtambile
55. Mhe. Mohamed Said Mohamed	-	Jimbo la Mpendae

56. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali- Jimbo la Uzini
57. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Jimbo la Bumbwini
58. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame - Nafasi za Wanawake
59. Mhe. Mussa Ali Mussa - Jimbo la Ole
60. Mhe. Mussa Foum Mussa - Jimbo la Kiwani
61. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake
62. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis - Nafasi za Wanawake
63. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini - Jimbo la Dimani
64. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy- Jimbo la Chaani
65. Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Kikwajuni
66. Mhe. Omar Seif Abeid - Jimbo la Konde
67. Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake
68. Mhe. Rashid Makame Shamsi - Jimbo la Magomeni
69. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa - Nafasi za Wanawake
70. Mhe. Said Omar Said - Jimbo la Wingwi
71. Mhe. Said Hassan Said - Mwanasheria Mkuu
72. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma - Nafasi za Wanawake
73. Mhe. Salma Mussa Bilal - Nafasi za Wanawake
74. Mhe. Shaib Said Ali - Jimbo la Chonga
75. Mhe. Simai Mohammed Said - Jimbo la Tunguu
76. Mhe.Sira Ubwa Mamboya - Uteuzi wa Rais
77. Mhe. Suleiman Makame Ali - Jimbo la Ziwani
78. Mhe. Suleiman Sarahan Said - Jimbo la Chakechake
79. Mhe. Tatu Mohamed Ussi - Nafasi za Wanawake
80. Mhe. Ussi Yahya Haji - Jimbo la Mkwajuni
81. Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Nafasi za Wanawake
82. Mhe. Wanu Hafidh Ameir - Nafasi za Wanawake
83. Mhe. Yussuf Hassan Iddi - Jimbo la Fuoni
84. Mhe. Zaina Abdalla Salum - Nafasi za Wanawake
85. Mhe. Zulfa Mmaka Omar - Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem - Katibu wa Baraza la Wawakilishi

BARAZA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA NNE

WIMBO WA TAIFA

*(Hapa wimbo wa Taifa uliimbwa kuashiria kuanza kwa Mkutano***)**

Kikao cha Kwanza - Tarehe 23 Novemba, 2016

(Kikao kilianza Saa 3.00 Asubuhi)

DUA

Mhe. Spika, (Zubeir Ali Maulid) alisoma Dua

KIAPO CHA UAMINIFU

Mjumbe afuataye aliapa kiapo cha uaminifu na kukaa katika nafasi yake ndani ya Baraza.

Mhe. Dkt. Sira Ubwa Mamboya

TAARIFA YA SPIKA

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe kwanza nichukue fursa hii kuwakaribisha sana katika mkutano wetu huu wa nne wa Baraza letu la Tisa, ambao unaanza leo tarehe 23 Novemba, 2016.

Waheshimiwa Wajumbe napenda kutoa kwenu na kwa wananchi kwa ujumla taarifa kuhusu Miswada ya Sheria iliyopitishwa katika Mkutano uliopita wa Baraza la Wawakilishi uliofanyika kuanzia tarehe 21 hadi tarehe 30 Septemba, 2016.

Katika mkutano wa tatu wa Baraza la Tisa la Wawakilishi Baraza hili lilipitisha Miswada mitano ya Sheria ambayo ni:

1. Mswada wa Sheria wa kuanzisha Taasisi ya Elimu ya Zanzibar na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

2. Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbali mbali na kuweka masharti yaliyo bora kuhusiana na mambo hayo.

3. Mswada wa Sheria ya Usimamizi, Utafutaji na Uchimbaji wa mafuta na gesi asilia, kuanzisha mamlaka ya udhibiti wa shughuli za utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia, kuanzisha kampuni ya maendeleo ya mafuta na kuhakikisha uwajibikaji wa taasisi za mafuta na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

4. Mswada wa nne ni Mswada wa Sheria ya kurekebisha Sheria ya Chuo Kikuu cha Zanzibar namba 8 ya mwaka 1999 kama ilivyorekebishwa na sheria Nam.11 ya mwaka 2009 na kuweka masharti bora pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

5. Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Katiba ya Zanzibar ya 1984 kama inavyotakiwa chini ya kanuni ya 91. 3 ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2012.

Naomba kutoa taarifa kwamba Miswada hiyo sasa imekuwa sheria kamili baada ya kusainiwa na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Waheshimiwa Wajumbe nawashukuruni sana. *(Makofi)*

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika naomba kuwasilisha mezani nakala zote za Gazeti Rasmi la Serikali pamoja na vijalizo vyake kuanzia tarehe 1 Oktoba, 2016.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha Hotuba ya uwasilishaji wa Mswada wa Sheria ya Kufuta na Kutunga Upya Sheria ya Ushahidi Sura ya Tano na Masuala yanayohusiana na hayo.
Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mwenyekiti Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Mswada wa Sheria ya Kufuta na kutunga upya Sheria ya Ushahidi Sura ya Tano na Masuala yanayohusiana nayo.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 81

Upungufu wa Miundombinu Katika Bonde la Umwagiliaji Maji Kirundunda

Mhe. Masoud Abrahman Masoud - Aliuliza:

Katika utekelezaji wa malengo ya Milenia ya kupunguza makali ya umaskini kwa wananchi wetu Serikali kupitia mradi wa TASAF ilitoa shilingi milioni 100 kwa wakulima walioko katika Bonde la Bumbwisudi eneo la Kirundunda miaka mitatu iliyopita. Fedha hizo tayari zimeshatumika kuimarisha miundombinu ya eneo hilo na wananchi wamechangia kwa 70% ya nguvu kazi ili bonde hilo liweze kutumika katika shughuli zao za kilimo cha umwagiliaji. Pamoja na juhudi hizo zote kufanyika bado eneo hilo halitumiki kama ilivyokusudiwa kutokana na ukosefu wa huduma ya umeme, na hali hiyo imepelekea baadhi ya wananchi kufuga ng'ombe na kuharibu baadhi ya miundombinu.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuziokoa fedha hizo ambazo zimeshatumika katika kuboresha eneo hilo pamoja na nguvu kazi ya nchi.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - Alijibu: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 81 kama ifuatayo:-

Mhe. Spika, Wizara yangu inathamini sana msaada mkubwa uliotolewa na Mradi wa *TASAF* pamoja na nguvu za wananchi katika kuendeleza sekta ya kilimo cha umwagiliaji maji kwa kuweka miundombinu ya kilimo hicho katika bonde la Bumbwisudi.

Mhe. Spika, Serikali imeshaanza kuchukua hatua ya kulipatia ufumbuzi tatizo la ukosefu wa umeme katika bonde hilo kwa kuiagiza Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi kukaa pamoja na Shirika la Umeme *(ZECO)* ili kuufikisha umeme katika eneo hilo.

Mhe. Spika, katika hatua za dharura Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi pia imeanza kulifanyia kazi suala la kutafuta *pump* zinazoendeshwa kwa nguvu ya nishati ya jua *(Solar pumps) ili* kupunguza gharama kubwa za kuunga umeme mkubwa kwa vituo vilivyo mbali na njia kuu za umeme, ikiwemo katika bonde

hilo ambalo umeme wa kawaida upo katika umbali wa *(km. 3),* na ili kuufikisha katika eneo hilo zinahitajika zaidi ya Shs. Milioni mia moja.

Mhe. Masoud Abrahman Masoud: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, kwa kujibu swali la kwanza katika Baraza hili lakini naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Ni lini umeme huu utafikishwa, kwa sababu katika kikao cha Baraza kilichopita Mhe. Waziri wa Kilimo alisema hili suala tayari litakaa sawa na wakati wowote umeme utafikishwa, lakini na yeye anasema wapo katika Mipango kwa *TASAF* pamoja na Wizara ya Kilimo kuhakikisha huo umeme unapelekwa, hiyo kauli inaonekana inajirejea rejea. Sasa nataka aniambie ni lini umeme utapelekwa katika bonde hili.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Tukubaliane naye lakini kwa kuwa Serikali imeshaanza jitihada zake za kuhakikisha tatizo hili linatatuka. Pia binafsi nimeshafanya ziara ya kwenda kulitembelea bonde hili la Bumbwisudi tukakutana na wananchi ambao wametumia nguvu zao katika kuliboresha bonde lile sambamba na Sheha wa Bumbwisudi.

Baada ya hayo tumueleze tu Mhe. Mwakilishi kwamba tayari Wizara yangu tumeshawaita Watu wa Wizara ya Kilimo, tumeshamuita Meneja wa Shirika la Umeme la *ZECO* tumeshakubaliana nao na tayari wameshaanza hatua zinazostahiki katika kuhakikisha dhamira ya kupeleka umeme pale inafanikiwa katika kipindi kifupi. *(Makofi)*

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Kijiji cha Kirundunda ni kijiji ambacho kiko katika Shehia ya Bumbwisudi jimbo la Mfenesini, na tukiacha bonde la Kirundunda jirani wao wana mabonde kama Mambosasa ambao pia wanalima kwa umwagiliaji. Na kutoka Mambosasa mpaka Kirundunda haizidi kiliomita moja urefu wake au kubwa wake.

a) Je, Mhe. Naibu Waziri atakubaliana na mimi kwamba bado Serikali iendelee na kupeleka umeme huu ambao umekusudiwa na usipelekwe umeme wa *solar*.

b) Wizara ya Kilimo katika kuwasidia wakulima masikini ilikuwa na mradi wa barabara za vijijini za wakulima kupitia mradi

wa *MIVARF* na barabara kutoka Mwachealale kupitia Mambosasa hadi Bumbwisudi imefika karibu zaidi na Kirundunda.

Je, Serikali haioni kama ingelikuwa ni vyema kijiji kile cha Kirundunda ambacho kina wakulima wengi na mazao mengi ikaongezewa barabara ile ya *MIVARF* ili na wananchi wa kule nao waweze kupunguza kero zao.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Kwanza tushukuru sana wenzetu wa *TASAF* ambao kwa namna moja au nyengine wamekuwa wakitumia gharama kubwa kwa dhamira ya kuisaidia Serikali na kuhakikisha matatizo ya wananchi tunaweza kuyatatua kwa namna moja au nyengine.

Lakini pia kweli anachokisema Mhe. Mwakilishi kwamba kuna barabara zile za *MIVARF* ambazo zimejengwa chini ya Wizara ya Kilimo na Mifugo, imani yangu na dhamira ya Serikali kwamba barabara zile jukumu la Wizara ya Kilimo ilikuwa kwenda kuzikabidhi katika Wizara ya Mawasiliano na Ujenzi, Wizara ya Mawasiliano na Ujenzi kwa kushirikiana na Serikali sasa ndio itaziingiza barabara zile katika mradi wa kuhakikisha barabara zile zinafanyiwa maboresho.

Lakini pili kweli, katika mradi huu wa *TASAF* wa Kirundunda tumwambie tu kwamba Mhe. Mwakilishi *TASAF* pale ina mradi mmoja kwa mitatu. Mradi wa Kirundunda kuna Kirundunda (1) kuna Kirundunda (2) na kuna Kirundunda (3). Miradi hii yote ipo katika eneo moja, lakini kilomita moja baadae kwa pembeni kuna huu mradi mwengine ambao pia ulifadhiliwa na *TASAF* lakini wenyewe *TASAF* walishakamilisha kila kitu kutokana na gharama yake pale ya kufikisha umeme mikoani takriban shilingi 25 milioni.

Lakini katika huu mradi wa Kirundunda tuna takriban milioni mia moja za Kitanzania, sasa kidogo kutokana na hali ya bajeti inapelekea jambo hili kulifanya awamu kwa awamu, ndio maana Wizara ya Kilimo na kupitia wataalamu wetu sasa tunaona ipo haja ya kuanza kutumia mashine za *solar* kuliko umeme huu wa kawaida. Ahsante sana.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza kama ifutavyo.

Mhe. Spika, katika miradi hii ya *TASAF* ya awamu ya tatu mradi ambao lengo lake ni kuokoa kaya masikini inalalamikiwa sana kwamba ndani ya mradi huu,

wale ambao wamepata fedha hizi wengine hawana vigezo vya kuweza kupata fedha hizi kwa ajili ya suala hili la kuokoa kaya masikini.

1) Je. Mhe. Waziri unalielewa hili
2) Na kama hilo lipo, je, ni hatua gani ambazo zimechukuliwa na Serikali ili kuona kwamba fedha hizi zilizoingia katika Mikono ya wasiohusika zinarudi na wale ambao wana haki ya kuweza kupata fedha hizo wanapata haki hiyo. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Kwanza nikubaliane naye kwa lile ambalo analisema, lakini niseme kwamba *TASAF* kwa mfano sasa hivi imeanza kupitia upya watu wote ambao wananufaika na mradi wa *TASAF* wale ambao wanatokana na kaya masikini.Dhamira kubwa ni kutaka kutizama katika hizi changamoto ambazo zimekuwa zikiibuka kwa namna moja ama nyengine. Lakini serikali kama serikali kupitia TASAF tayari tumeshaliona hilo na tumeshalitambua ndio maana tukawa na dhamira sasa ya kuanza kupitia upya kaya zote ambazo zimekuwa zikinufaika na mradi huo wa TASAF.

Mhe. Spika, ahsante. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante sana. Mhe. Waziri nimpongeze sana kwa *professionalism* ambayo ameionyesha katika siku yake ya mwanzo ya kazi.

Waheshimiwa Wajumbe naomba nimtambue mgeni mmoja ambaye yupo hapo juu naye ni mume wa Mhe. Dkt. Sira Ubwa Mamboya anaitwa bwana Islam, amekuja kumuona mkewe akiapishwa. Shukran na karibu sana. (*Makofi*).

Nam. 82

Ukemeaji wa Vitendo Viovu

Mhe. Ali Khamis Bakari - Aliuliza:-

Serikali mara nyingi hukemea vitendo viovu visivyotakikana hapa nchini. Katika hali isiyo ya kawaida kuna wananchi ambao wanajitoa fahamu kwa kuwaingilia wanyama jambo ambalo sio zuri na baya sana, ukizingatia kwamba wanyama hao ni sehemu ya chakula cha binadamu.

Je, Wizara ina mpango gani wa kuwachukulia hatua kali watu hawa.

Mhe. Naibu Waziri wa Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora - Alijibu**:-**

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Tumbe swali lake nambari 82 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kabla ya kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi naomba kwanza kutoa maelezo yafuatayo:-

Mhe. Spika, ni kweli kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekua ikichukua hatua mbalimbali kukemea vitendo viovu katika jamii yetu ikiwemo kuwaingilia wanyama na vitendo vyengine visivyokubalika katika jamii ambavyo vinaonekana kuibuka kwa wingi katika siku za hivi karibuni.

Mhe. Spika, kuibuka kwa vitendo hivi ni matokeo ya athari za mmong'onyoko wa maadili unaoikumba jamii yetu ya sasa. Naomba kuchukua fursa hii kuiomba jamii yetu kuendelea kuchukua hatua za kukemea vitendo viovu ambavyo vinasababisha athari kubwa katika jamii yetu.

Mhe. Spika, baada ya maelezo haya naomba sasa kujibu swali la msingi la Mheshimiwa kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa kitendo cha kumuingilia mnyama ni kosa kisheria kwa mujibu wa kifungu cha 50 (b) cha Sheria ya Mwenendo wa adhabu nambari 6 ya mwaka 2004, Wizara kwa kushirikiana na vyombo vyengine vya Dola inaendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kupambana na tatizo hilo ikiwemo kuwafungulia mashtaka watuhumiwa wa matendo hayo.

Aidha, Wizara kupitia taasisi zake inaendelea kutoa elimu kwa umma juu ya kujiepusha na vitendo viovu vinavyoweza kuhatarisha amani ikiwemo vya kuwaingilia wanyama. Ahsante

Mhe. Ali Khamis Bakari: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu yake lakini napenda kumuuliza swali moja la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Je. Mhe. Naibu Waziri wanyama wale ambao walisharipotiwa kuingiliwa mnawachukulia hatua gani, mnawadhibiti nyinyi ama mnawaachia wafugaji wanaendelea tena kuwafuga kwa ajili ya kitoweo.

Mhe. Naibu Waziri wa Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, linapotokea tukio kama hili la mnyama kuingiliwa na

binadamu kwa upande wetu sisi moja kwa moja kazi yetu huwa ni kupokea ile kesi. Suala la mnyama kutumiwa au kutotumiwa hili tunakuwa sisi sio suala la upande wetu, sisi kwetu moja kwa moja tunapokea kesi na kesi ile kuhakikisha kwamba tunaipeleka mahakamani na mtuhumiwa yule kuchukuliwa hatua ipasavyo.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Naomba kumuuliza Mhe. Naibu Waziri, mnyama yule kwa taratibu ni kwamba keshanajisiwa. Mhe. Naibu Waziri anasema mnyama yule kwa upande wake yeye hahusiki tena wakati yeye ndiyo mtunga sheria. Sasa mnyama yule atahukumiwa katika nafasi gani wakati sheria yeye aliyonayo ni kwamba haimgusi mnyama yule.

Mhe. Naibu Waziri wa Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, naomba Mheshimiwa arejee swali lake.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Spika, nasema kwamba hii ni Wizara ya Sheria na Katiba ambayo inamlinda yule mnyama au inatulinda watu wote. Yule mnyama ambaye keshanajisiwa kwa hali yoyote tayari keshaathirika. Sasa Mhe. Waziri anasema kwamba hahusiki na mnyama yule au hamtambui au hana maadili naye yoyote na yeye ndiye mwenye sheria. Ina maana hakuna sheria kwa upande wa kwake yeye ya mnyama yule nini atafanywa.

Mhe. Naibu Waziri wa Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, maelezo yangu ya awali nimesema kwamba linapotokea tatizo kwa upande wa Wizara yetu ni suala la mtuhumiwa kufikishwa katika vyombo vinavyohusika. Kwa upande wetu sisi kupitia Ofisi ya *DPP* linapoletwa faili tunaliangalia na kama kuna kesi tunapeleka Mahakamani ili kuendelea na suala hilo.

Mhe. Spika, ninachokisema ni kwamba suala hili kwa maana kwamba kama mnyama huyu ataliwa au haliwi kwa upande wetu sisi huwa tunaendelea na hii kesi, suala hilo litakuwa katika sehemu nyengine. Napenda kueleza kwamba, mnyama kama alivyo binadamu, mnyama na yeye ana haki zake vile vile, kitendo cha kumuingilia mnyama ni kosa kwa mujibu wa sheria zilizopo Zanzibar. Kwa hivyo yeyote yule ambaye ataamua kumuingilia mnyama ajue kwamba anatenda kosa, kwa sababu mnyama yule analindwa na ana haki zake kama ilivyooneshwa katika sheria hiyo ambayo imetajwa awali.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kumuuliza swali moja la nyongeza. Ni watu wangapi ambao wameshafikishwa Mahakamani na kuhukumiwa kwa kufanya vitendo hivyo kwa Unguja na Pemba.

Mhe. Naibu Waziri wa Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, zipo kesi mbali mbali ambazo watuhumiwa wa masuala haya ya kuwaingilia wanyama zimepelekwa Mahakamani. Hili kwa kuwa ni suala la *statistics*, inakuwa ni vigumu kumjibu sasa hivi.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako ningeliomba kwamba Mheshimiwa huyu kumjibu kwa maandishi. Lakini ni lazima ifahamike kwamba kesi zipo, lakini sio idadi ya kutisha, kwa maana kwamba sio nyingi, inawezekana ikapita mwaka mzima kesi hizo hazijatokea. Lakini inawezekana wakati mwengine mwaka mmoja ikatokezea kesi moja au mbili.

Nam. 1

Tatizo la Kuwaka kwa Taa Zinazotumia Mionzi ya Jua

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Serikali imeamua kuweka taa za kutumia mionzi ya jua lakini taa hizo zimekuwa zikiwaka na kuzima, na katika mitaa mingine zimekuwa haziwaki kabisa kwa mfano Maisara kuelekea Uwanja wa Ndege, Michenzani, Kisiwandui na Darajani.

(a) Je, Serikali inalijua tatizo hilo na imechukua hatua gani ili kuhakikisha lengo la uwekaji taa linafanikiwa ili kuondoa giza katika mitaa.

(b) Katika mpango wa uwekaji wa taa hizo, ni mradi wa Serikali na umegharimu kiasi gani na taa zipi zinatokana na msaada.

Mhe. Spika, kwa heshima kubwa naomba uniruhusu dakika moja nitoe shukurani kwa kuwapongeza Manaibu Waziri waliopata uteuzi hivi juzi, niwatakie kazi njema na wale waliokuwa wanatamani nafasi hiyo wasikate tamaa, waendelee kusikiliza redio.

Vile vile nimpongeze aliyekuwa Naibu Waziri wa Afya na akawa Naibu Waziri wa Kilimo na kupata uteuzi kutoka jimbo la Ikulu. Baada ya maelezo hayo Mheshimiwa naomba swali langu lijibiwe.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ - Alijibu:-
Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 1 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, serikali kupitia Baraza la Manispaa inalitambua tatizo la kuwaka na kuzimika au kutokuwaka kabisa kwa taa za barabarani zinazotumia mionzi ya jua. Taa hizo zipo katika maeneo ya Michenzani, Kisiwandui na Darajani. Hatua ambayo ilichukuliwa na Baraza la Manispaa ni kuzitengeneza taa hizo ambapo makubaliano yalikwishafikiwa baina yake na Kampuni ya "*Ware link*". Kabla ya kusainiwa kwa mkataba wa matengenezo ambayo yangegharimu Tsh. 27,000,000.00. Hata hivyo, Baraza la Manispaa lilipokea taarifa kutoka Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwamba Serikali ya Watu wa China kupitia Ubalozi Mdogo uliopo Zanzibar ambayo ndio iliyoweka taa hizo, itafanya matengenezo ya taa hizo kupitia kampuni ya ZTE.

(b) Mhe. Spika, taa zilizowekwa njia nne za Michenzani pamoja na Darajani ni msaada kutoka Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China. Aidha, taa zilizowekwa kuanzia kwa Biziredi kupitia Amani '*round about'*, Mwanakwerekwe, Magomeni, Mwembenjugu hadi Kariakoo na maeneo mengine ya Bustani za Jamhuri, Victoria na maeneo ya Mji Mkongwe ni mradi wa Serikali kupitia mradi wa *ZUSP* na gharama zake ni Tzs 5.5 bilioni.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, naomba nitumie lugha kidogo sauti iwe ndogo ili apate kusikia kutokana na hii *mic* kwa vile Mhe. Naibu Waziri ni mgeni ili aweze kusikia kwa utulivu.

Kwa vile serikali imo humu ndani na Kanuni ya 37 inaruhusu swali moja kujibiwa na Waziri mwengine au Mwanasheria Mkuu.

Alipokuwa akijibu swali alisema kuna mkataba wa matengenezo ambao unagharimu Shilingi milioni 27. Hata hivyo Baraza la Manispaa limepata taarifa kutoka kwa ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, inaweza ikawa taarifa hiyo ni kweli au si kweli ndio maana ya taarifa.

a) Suala hili ni la muda mrefu, lini taa hizo zitatengenezwa baada ya kutupiwa Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

b) Kampuni ya ZTE ya Kichina ni ya kwanza kufunga taa za barabarani na ndio kampuni vile vile ya kwanza kufunga *camera* za CCTV na ilizinduliwa na Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Spika: Mheshimiwa jielekeze kwenye swali.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kampuni ya ZTE ilikuwa ni Kampuni ya mwanzo kufunga taa kabla ya uchaguzi 2015 na kufunga *camera*. Kampuni hii nafikiri ilipata pigo kama sio msaada wa Mwanasheria Mkuu na yupo hapa baada ya kuleta taa na *camera* karibu 300 na zikakaa muda mrefu Bandarini, haioni kuwa imekata tamaa au imevunjwa moyo kwa kukaa kwa muda mrefu taa zile.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, niombe radhi kidogo sijamfahamu vizuri lakini hata hivyo ambavyo nimemsikia naomba niendelee kumjibu.

Mhe. Spika, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba tatizo hilo ni la muda mrefu, lakini hata hivyo matengenezo ya tatizo hili, tunatarajia kazi itaanza muda si mrefu. Tunategemea kwamba vifaa vya ujenzi ambavyo vinaweza kutumika katika matengenezo hayo, tunategemea vitawasili ifikapo mwezi Disemba 2016.

Mhe. Spika, niwaombe radhi wananchi waweze kuvuta subira kidogo, mipango mizuri ya serikali yetu inaendelea kuyachukua na kuhakikisha kwamba tatizo hili linaondoka kwa mujibu ambavyo limekusudiwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, kuhusu utaratibu.

Mhe. Spika: Mheshimiwa tafadhali. Mhe. Zulfa.

Mhe. Zulfa Mmaka Omar: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali langu dogo tu lenye (a) na (b).

a) Kwa kuwa mradi wa taa za barabarani ni wa Zanzibar na tayari tumeshaona taa hizo kwa upande wa Unguja katika miji tofauti zimeanza kuwaka. Ni sababu gani zilizopelekea hadi leo ikawa Pemba hawajaanza kufunga taa hizo katika mji hata mmoja.

b) Je, ni lini ufungaji huo wa taa kwa upande wa Pemba utaanza na tutaanza kuondokana na tatizo la giza.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri mwenyewe naona unalo jibu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, kwanza nataka nimpongeze sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake ambayo aliyomjibu Mheshimiwa muuliza swali la nyongeza la kwanza.

Mhe. Spika, miradi hii miwili ambayo imeweka taa za njiani zinazotumia mionzi ya jua, mradi mmoja ulikuwa ni msaada kutoka China ambao ulitekelezwa na ndugu zetu wa Kampuni ya ZTE, lakini msaada ulipewa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Watu wa China. Msaada huo ulikuwa kama ni *pilot* kwa ajili ya kuweka taa za njiani, kwa hiyo katika *pilot* ya mradi huo ilielekeza katika mji wa Unguja peke yake.

Mradi wa pili ni mradi wa *ZUSP*, ambao Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia mradi huu wa *ZUSP* imekopa fedha kwa ajili ya kuweka taa za njiani. Mradi wa *ZUSP* umekwenda katika mikoa mitatu katika wilaya nne za Unguja, Wilaya tatu za Pemba na wilaya moja ya Mjini Unguja. Kwa hivyo katika mradi huu za *ZUSP* una miradi una sehemu, una sekta tofauti nazo ni:

- Sekta ya Ujenzi
- Sekta ya Machinjio
- Sekta ya Michirizi

Kwa hivyo katika eneo la taa za barabarani inaonekana kwamba mji wa Zanzibar ambao ni mji mkuu kwa Zanzibar kuna umuhimu wa kuweka kipaumbele katika kuweka taa za barabara. Ndio maana taa hizi zimewekwa katika mji wa Unguja. Lakini kwenye mji wa Pemba katika mradi huu kuna mambo mengi sana ambayo yamefanywa kupitia mradi wa *ZUSP*.

Hata hivyo nataka nimuhakikishie Mhe. Zulfa kwamba awamu ya pili ya mradi huu wa *ZUSP*, tunatarajia kwamba tutakapoweka taa za njiani tutaelekea katika maeneo mbali mbali ya Unguja na Pemba na serikali imelizingitia hilo, ahsante sana.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.
Nichukue fursa hii kumpongeza sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake, lakini vile vile na majibu ya Mhe. Waziri.

Mbali na majibu mazuri hayo Mhe. Spika, nichukue fursa hii kuipongeza Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa kuweka mtandao mzuri wa taa katika mji wa Zanzibar yakiwemo maeneo ya Kikwajuni, Maisara, Amani, Kijangwani na maeneo mengine. Mbali na maeneo hayo kuna tatizo la taa kuanzia maeneo ya Kinazini kuja Kariakoo na Kariakoo kuja Miembeni.

Je, serikali ina mpango gani kuifanyia ukarabati au kuweka mitandao mipya ya taa za mionzi ya jua katika maeneo hayo.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, naomba nimuhakikishie Mheshimiwa Mwakilishi kwamba tatizo la kukosekana kwa taa katika maeneo hayo ya barabara kuanzia Kinazini kuelekea Kariakoo ni tatizo ambalo kwa kweli lipo, lakini kwa sasa Wizara inafanya ukarabati mkubwa wa barabara katika maeneo yale, nadhani baada ya kukamilika kazi hiyo serikali kupitia wizara yangu itajitahidi kuona inatafuta namna ya kurejesha huduma hiyo kama ilivyokuwa hapo awali na kuweza kufanikisha yale malengo ya kuweza kuleta usalama na uangalifu zaidi katika mji wetu wa Zanzibar.

Napenda nimuhakikishie Mheshimiwa Mwakilishi baada ya kumalizika kazi hiyo, lengo la serikali ni kuhakikisha kila maeneo ambayo yanahitaji huduma hiyo inaweza kupatikana kwa mujibu wa vile ambavyo inastahiki.

Nam. 112

Mpango wa Serikali Kununua Chata kwa Ajili ya Watalii

Mhe. Viwe Khamis Abdalla – Aliuliza:-

Naipongeza Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuweza kununua ndege mbili ambazo zitakuwa zikiwapeleka watalii katika sehemu ambazo zina vivutio vya Utalii hapa Tanzania.

Je, Mhe. Waziri Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imejipanga kwa kununua japo vichata angalau vikaweza kupeleka watalii kwenye visiwa vyenye vivutio vya utalii hapa Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kujibu swali nambari 112 la Mhe. Mwakilishi Viwe Khamis Abdalla nafasi za wanawake kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba hivi karibuni Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT) imenunua ndege mbili kwa nia ya kuimarisha huduma za usafiri wa anga nchini. Kwa kauli za viongozi wa juu wa SMT, utaratibu wa kupatikana ndege nyengine mbili unaendelea ili kutimiza idadi ya ndege nne. Naomba kuchukua nafasi hii kumpongeza sana Mhe. John Pombe Magufuli, Rais wetu

wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kufanikisha haya yatakayosaidia ukuaji zaidi wa huduma za utalii na kuchangia katika kuimarisha uchumi katika nchi yetu.

Mhe. Spika, pamoja na kutambua umuhimu wa usafiri wa anga katika kukuza na kuimarisha utalii na uchumi nchini, SMZ kwa sasa haina mpango wa kununua ndege, badala yake, kwa kuzingatia hali ya uchumi wetu, mahitaji makubwa ya jamii kwa sasa na uwezo wa wastani wa Serikali kimapato, SMZ itaendelea kuweka mkazo katika kuimarisha huduma za msingi za kiuchumi na kijamii. Uimarishaji wa huduma za usafiri wa anga utafikiriwa baadae hali ya uchumi wetu itakapoimarika. Kwa kipindi hiki Serikali itaendeleza jitihada zake za kuweka mazingira bora ya uwekezaji na biashara ili sekta binafsi iweze kukua na kutoa huduma mbali mbali ikiwemo za usafiri wa anga.

Mhe. Viwe Khamis Abdalla: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kumuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Sekta ya Utalii Zanzibar inakuwa ikiongeza pato katika nchi yetu, je Mhe. Waziri ni kiasi gani cha fedha ambazo zinaingia hapa nchini zinazotokana na sekta hii ya utalii.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Spika, Sekta ya Utalii ikijumuisha sekta ya huduma inachangia wastani takriban wa asilimia 43 ya pato la taifa. Ni mchango mkubwa ukilinganisha na sekta nyengine zote na ndio maana Serikali inaweka mkazo sana katika sekta ya utalii kutokana na umuhimu wake unaotokana na mchango wake katika uchumi wetu. Naomba kile kiasi cha fedha anachokihitaji Mheshimiwa nitampatia kwa maandishi.

Mhe. Suleiman Sarahani Said: Mhe. Spika, ninakushukuru sana kwa kuniona na mimi nataka nimuulize Waziri kwamba Serikali imejikita sana katika kuhudumikia wananchi wake kwa usafiri wa Pemba na Zanzibar kwenye meli, na kwa kweli tunaishukuru Serikali yetu kwa jitihada zake kubwa sana. Lakini nimeona kuwa suala la upande wa anga suala hili Serikali halikulitilia mkazo, haikutilia maanani.

Je, Serikali imeona hakuna umuhimu wa jitihada za dharura kuweza kuweka chombo hiki ambacho kwa visiwa vyetu hivi ni muhimu na vya haraka katika nchi yetu. Je, Serikali haikuona umuhimu wa kuweka kipaumbele kununua ndege kwa ajili ya biashara ya kiserikali, kuliko kuwaachia biashara hizi kwa wafanyabiashara binafsi.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Spika, Serikali inaona umuhimu wa usafiri wa anga na ndio maana katika jibu mama nilisema kwamba Serikali itaendelea kuweka mazingira bora yatakayosaidia sekta binafsi kuwekeza katika eneo hilo. Nilisema kwamba hapo baadae uchumi wa nchi yetu ukiimarika Serikali itazingatia suala la ununuzi wa ndege zake.

Mhe. Spika, lakini kupanga ni kuchagua. Zanzibar ina mahitaji yake, Zanzibar ina *priorities* zake. Kwa sasa katika kipindi cha miaka 3 ijayo ununuzi wa ndege sio eneo la umuhimu la kupewa kipaumbele. Eneo la kupewa kipaumbele katika usafiri wa baharini ambao sisi na Serikali imeona kwamba ni eneo muhimu, Serikali imenunua meli kubwa MV Mapinduzi II na inafanya kazi vizuri tu baina ya visiwa vyetu viwili na Dar es Salaam. Hapo hali itakapoimarika Mhe. Spika, basi Serikali itazingatia suala la usafiri wa anga.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii kumuuliza swali la nyongeza Mhe. Waziri wa Fedha. Katika jibu lake mama alisema Serikali bado haijakuwa na mpango wa kununua ndege kulingana na hali yake ya kiuchumi lakini badala yake Serikali imewaachia wawekezaji binafsi katika masuala ya usafiri wa anga.

Je, pamoja na kwamba wanatoa huduma hizi za anga wawekezaji binafsi katika visiwa viwili hivi lakini Serikali inajua kwamba wawekezaji hawa bado wanahatarisha uhai wa abiria wao kwa ndege zao ambazo kila ndege ina *pilot* mmoja tu na bila ya kuwa na *pilot* mwengine wa akiba, kitu ambacho kwamba yule ni binadamu akitokezea kuumwa uhai wa abiria wale wote umepotea. Je, Serikali ina mpango gani katika kulisimamia hili na kama analijua.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Kwanza na mimi nimpongeze Mhe. Waziri wa Fedha kwa majibu yake mazuri kuhusiana na mambo haya ya anga ambayo ameyatolea maelezo mazuri sana. Lakini vile vile nikuombe kwa idhini yako Mhe. Spika, nimtake Mhe. Mwakilishi Shehe Hamad Mattar hili suala lipo katika masuala yetu tuliyopangiwa safari hii, kwa hivyo avute subira tu na sisi tutamjibu au kama anataka kupewa jibu sasa hivi tutampa, lakini hili swali ambalo limeulizwa na Mhe. Mwakilishi katika mkutano wetu huu sasa hivi wa Baraza la Wawakilishi.

Nam. 143

Kulipwa Posho la Mazingira Magumu kwa Wafanyakazi wa *ZBC*

Mhe. Yussuf Hassan Iddi - Aliuliza:

Kwa kuwa Mhe. Rais wa Zanzibar Dk. Ali Mohamed Shein aliwaahidi Wafanyakazi wa ZBC-TV na RADIO kuwapatia posho la mazingira magumu na posho hilo wameanza kulipwa mwezi wa Agosti 2016.
Je, ni sababu gani zilizopelekea wafanyakazi wa ZBC TV na RADIO kutolipwa posho hilo kwa mwezi wa Septemba 2016.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo - Alijibu:

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Yussuf Hassan Idd Mwakilishi wa Jimbo la Fuoni swali lake Nam. 143 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, sababu zilizopelekea wafanyakazi wa ZBC Radio na TV kutolipwa posho hilo kwa mwezi wa Septemba ni kutokana na tatizo lililojitokeza kwa upande wa Wizara ya Fedha, na hata hivyo Shirika la Utangazaji la Zanzibar lilifuatilia na kushirikiana katika kulitatua tatizo hilo na baadae walilipwa posho hilo tarehe 27/10/2016.

Mhe. Yussuf Hassan Idd: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, kwanza nimpongeze tu kwa jitihada ambazo wamechukua kuhakikisha kwamba wafanyakazi hawa wanapata stahiki zao. Lakini kwa kuwa ZBC TV na Radio ina kada mbali mbali za uandishi, utangazaji, mafundi pamoja na kada ya utawala wakiwemo madereva na hasa hawa madereva ndio wanawaleta hawa waandishi wetu hapa na kuwarejesha na wao hawamo katika mpango huu wa kupata posho hii. Sasa je, lini nao madereva hao watastahiki kupata posho hili.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Ahsante sana Mhe. Spika, kama nilivyojibu katika swali mama kama tumefuatilia na kuwalipa wafanyakazi maposho haya, nichukue fursa hii kwanza kumpongeza Mhe. Waziri wa Habari kwa usimamizi mzuri wa kusimamia tatizo ambalo limejitokeza kwa muda mrefu la kuwapatia maposho haya baadhi ya wafanyakazi. Pia shukurani za pekee ziende kwa Mkurugenzi wetu wa ZBC kwa muda mfupi tumesimamia hili na kulipa maposho haya wakiwemo

madereva, likizo, *overtime* za wafanyakazi, watu wa mawio na wafanyakazi wote kwa jumla. Kwa hivyo nimwambie Mhe. Mwakilishi kwamba suala hili tumeshalisimamia na hatua tayari tumeshaanza kuzitekeleza.

Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kwa kunipa fursa hii ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri kwa vile suala la posho Wizara imeweza kulishughulikia vizuri. Je, Wizara ina mpango gani wa kuajiri wafanyakazi walioko Bungi ambao kwa kipindi kisichopoungua miaka mine kwa sasa wawafanya kazi za mikataba.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika, nakiri kwamba kuwepo kwa wafanyakazi katika kituo cha Bungi ni walinzi ambao hawajaajiriwa na wanaendelea kupata posho. Lakini naomba kwa faida ya Waheshimiwa Wawakilishi wote na wananchi wetu kwamba Wizara sasa hivi ina mpango wa kuwaajiri au kuchukua watu wa vikosi kwa sababu sehemu ile ni sehemu nyeti na wale wafanyakazi waliopo pale wameshazidi umri, kwa hivyo hili Serikali sasa hivi ina mpango wa kuchukua walinzi wa Serikali ili kupeleka katika kituo kile, kwa sababu kuwepo kwa walinzi wa kawaida bila silaha pale ni hatari na hili tunalichukulia tutawaajiri walinzi tuwapeleke pale.

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba niulize swali moja la nyongeza lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo. Mhe. Spika, sote tunakubaliana kwamba taaluma ya habari ni kama muhimili, wengine wanasema ni muhimili wa nne, sio rasmi lakini, na wana habari ni watu muhimu sana katika kuendesha shughuli za maendeleo ya nchi.

(a) Ni lini Serikali kupitia Wizara hii ya Habari itajenga maslahi mazuri kwa wanataaluma wetu wa TVZ, Radio na Gazeti la Zanzibar Leo ambao kwa muda mrefu wamekuwa maslahi yao ni madogo sana na wanalalamika sana.

(b) Nusu ya wafanyakazi wa vyombo hivyo bado hawajaajiriwa na wanapelekwa katika sehemu nyeti. Serikali ina mpango gani wa kuwaajiri ili nao pia waweze kuitumikia nchi yao vizuri.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Ahsante sana Mhe. Spika, napenda kumpongeza sana Mhe. Naibu Waziri kwa ufasaha wa majibu anayoyajibu. Ninamshukuru sana kwa ufasaha wa majibu aliyoyatoa, lakini nichukue fursa hii kumjibu Mhe. Machano Othman Said swali lake la nyongeza.

Kwanza nianze na swali (b) suala ambalo linaonekana kuna wafanyakazi wengi ambao wamechukua muda mrefu hawajaajiriwa. Kama alivyoionesha tasnia ya habari, tasnia ya habari inaajiri watu ambao wanaajiriwa moja kwa moja kama watumishi wa Serikali. Lakini kuna watumishi wanaoajiriwa kwa kujitolea, wanaitwa *freelance*. Wafanyakazi hawa wana uwezo wa kupeleka taarifa za habari popote, si ZBC pekee, pale wanapohisi habari zao zinauzika, vyombo vyengine vya habari basi wanaiacha ZBC na kupeleka katika vile vyombo ambavyo wanahisi vina maslahi kwao.

Kwa hivyo ni wafanyakazi ambao wanapata maslahi kupitia vyombo zaidi ya maslahi wanayopewa na ZBC. Kwa maana hiyo kuchukua muda mrefu wafanyakazi wale inaonekana kwamba *performance* yao inawezekana kwamba haikufikia viwango lakini pale tu wanapoonesha utendaji mzuri Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo inawaajiri kupitia ZBC iwe Radio au Televisheni. Kwa hawa waliobakia ambao wame-*suffer* muda mrefu hivi sasa Wizara ina mpango maalum, kuhakikisha kwamba inawakwaza waweze kufanya kazi vizuri na itawaajiri wakati wowote Serikali ambapo inaweza kutoa ruhusa ya kuajiri.

Kuhusu swali lake la kuboresha maslahi ya wafanyakazi katika tasnia ya habari. Nataka nimuunge mkono mawazo yake kwamba habari ni karibu ya muhimili wa nne na una umuhimu wake katika nchi, kwani taarifa zikipotoshwa tumeupotosha umma, lakini taarifa zikitengemaa tumeutengeneza umma. Hivyo, nataka nimwambie wazi kwamba lengo zima la serikali kuifanya *ZBC* kuwa shirika, ni hili la kuhakikisha kwamba inawadumisha vizuri wafanyakazi wake wanakuwa wafanyakazi wanaofanya kazi zao kwa mujibu wa shirika lilivyo. Hivi sasa tumekamilisha mpango wa *scheme,* tumekamilisha mpango wa *job grade* na *job descriptions* zao ziko wazi. Muda mfupi wafanyakazi hawa watakuwa wanafanya kazi kishirika, tunalowaomba wajiendeshe wasitegemee pato la serikali, mapato yanawatosha na Mhe. Machano awe mzuri katika kulipia matangazo. Nashukuru sana.

Nam. 2

Umiliki wa Shamba la Razaba (Makurunge) kwa Serikali

Mhe. Yussuf Hassan Iddi – Aliuliza:-
Kwa kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inamiliki hekta 6,200 za shamba la RAZABA (MAKURUNGE) baada ya kugawanywa upya mwaka 2007.

(a) Je, hatimiliki ya shamba hilo imepatikana au bado.

(b) Kuna baadhi ya maeneo ya shamba hilo limevamiwa na wananchi wa Bagamoyo kwa ujenzi, malisho ya wanyama na kilimo. Je, serikali imechukua hatua gani kwa wavamizi hao.
(c) Je, serikali ina mpango gani wa muda mfupi na muda mrefu wa kuliendeleza shamba hilo ili lilete tija kubwa kwa Zanzibar.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi – Alijibu:-
Mhe. Spika, ahsante sana kwa idhini yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake lenye kipengele (a) (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Chuo cha Kilimo Kizimbani kimekuwa na mawasiliano ya karibu na Wizara ya Ardhi, Maendeleo ya Makaazi pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo katika kutafuta hatimiliki ya shamba la Makurunge kama ilivyoagizwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Aidha, suala la kupatikana hati hiyo hakuna pingamizi juu ya utoaji wa hatimiliki kwa shughuli za kilimo na mifugo kwa kuzingatia masharti yafuatayo:-

I. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilipewa gharama za utengenezaji wa hati ambazo zinakadiriwa kufikia shilingi za Kitanzania bilioni moja, milioni mia mbili hamsini na tano, laki tatu elfu tisini na tisa, mia moja kumi na tano (Tshs. 1,255,399,115/=)
II. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar italazimika kurejesha hati hiyo baada ya mpango wa mji mdogo wa Bagamoyo kupitishwa rasmi.

Mhe. Spika, Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kupitia Chuo cha Kilimo Kizimbani imeona kwamba suala la kupatikana kwa hatimiliki kwa matumizi ya kilimo na mifugo halitakuwa na faida kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kwa mantiki hiyo, na kwa pamoja tumeonelea ni vyema tukubaliane na mpango mpya wa matumizi unaoendana na matakwa ya Sheria ya Mipango Miji ya Tanzania Bara pamoja na mpango wa mji mdogo wa Bagamoyo.

Mhe. Spika, ni kweli maeneo hayo yamekuwa yakivamiwa na wananchi wa Bagamoyo kwa ujenzi, malisho ya wanyama na kilimo. Chuo cha Kilimo kimechukua hatua madhubuti ya kuyahifadhi na kuyalinda ili yasiendelee kuvamiwa. Hatua zilizochukuliwa ni pamoja na:-

- ✓ Kuweka mabango maalumu katika sehemu za mipaka yake ili kuwafahamisha wananchi kuwa eneo hilo ni la Serikali ya

Mapinduzi ya Zanzibar kwa Chuo cha Kilimo Kizimbani na kwamba hairuhusiwi kwa mtu yeyote kufanya uvamizi wa aina yoyote;

- ✓ Kufanyika ziara za viongozi wa kitaifa eneo husika akiwemo Mhe. Makamu wa Pili pamoja na Naibu Waziri na uongozi wa Wizara ya Kilimo.

- ✓ Kuimarisha ulinzi kwa watendaji wa chuo walioko Bagamoyo**.**

Mhe. Spika, kuhusiana na kipengele cha (c) swali la Mheshimiwa Mwakilishi ni kwamba serikali imekubaliana na Mipango Miji ulioandaliwa na Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo ambayo imeelekeza kuwa eneo hilo ligawiwe kwa kufuata matumizi ya Mpango Mkuu ambao utahusisha maeneo ya makaazi, biashara, taasisi za mafunzo na mambo mengine. Ikiwa eneo la RAZABA litatumika kama ilivyopendekezwa katika mpango wa matumizi uliopendekezwa litaweza kuzalisha mapato, na hivyo kupelekea kuimarika kwa uwezo wa chuo katika kutekeleza malengo yake. Hali hii itawezesha eneo hilo kutumika kwa uwekezaji kwa taasisi za serikali kuuzwa au kukodishwa kwa taasisi au watu binafsi na hatimaye kuongeza pato la serikali kwa fedha zitakazopatikana na mauzo hayo.

Mhe. Spika, mpango wa matumizi uliopendekezwa tayari umeridhiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo katika vikao rasmi vilivyofanyika kulijadili suala hilo. Mpango huu utakapokamilika inakadiriwa kupatikana viwanja na vitalu vyenye thamani ya shilingi za Kitanzania bilioni mia tatu na themanini na saba (TShs. 387,000,000,000/=).

Fedha hizo zitakapopatikana zitaiwezesha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutimiza dhamira yake katika mipango ya taifa ikiwemo kukiendeleza Chuo cha Kilimo Kizimbani. Ahsante.

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: Mhe. Spika, ahsante pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja dogo tu la nyongeza. Kwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo kama alivyosema katika jibu lake mama imebadilisha matumizi ya eneo hilo la RAZABA. Je, serikali haioni kwamba *ZSSF* ikawapa eneo hilo kwa ajili ya kuwekeza na kuleta tija kwa nchi yetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Spika ningeomba Mhe. Mwakilishi arudie swali lake.

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: Mhe. Spika, ahsante sana Mhe. Spika naomba nirejee swali dogo ambalo nimeuliza la nyongeza. Kwa kuwa katika jibu mama amesema kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo imebadilisha matumizi ya eneo hilo. Je, serikali haioni kwamba eneo hilo ikawapa *ZSSF* kwa ajili ya kuwekeza kule kwa sababu kuna maeneo yenye bahari ili kuleta tija kwa Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, kwa vile eneo hili ni la serikali, lakini vile vile tayari limeshapewa Chuo cha Kilimo Kizimbani, na tayari limo katika *process* ya upimaji na ukataji wa viwanja, na tunategemea kupata mshindi huyu ambaye labda amechukua zabuni tunatarajia kutoa kati kati ya mwezi huu wa Disemba na suala la *ZSSF* hilo litafikiriwa kwa baadae.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, ahsante sana kwanza naomba nimshukuru sana Naibu Waziri kwa majibu fasaha kabisa aliyoyatoa, na kama alivyoeleza kwamba ni kweli serikali imeamua kabisa kuwa eneo hili litumike vizuri ili kuliletea pato la juu nchi yetu. Kwa hiyo, tumetangaza *tender* kupata mshauri ambaye atatushauri namna bora ya kupatikana mapato katika eneo hilo. *Tender* tayari imeshafunguliwa tunategemea mwezi wa Disemba itakuwa tayari mapendekezo yamepatikana tutawasilisha serikalini, na hatimaye serikali itaamua ni namna gani matumizi yafanyike.

Lakini kama alivyosema Naibu Waziri katika eneo hilo kuna maeneo makubwa muhimu sana. Kwa mfano, kuna ukanda tu wa bahari yenye *beach* kilomita 10 hiyo peke yake ukiwekeza ni fedha nyingi sana tu unaweza ukapata. Kwa hiyo, nasema hatua hiyo itakapokamilika tutawasilisha serikalini halafu hatimaye serikali itaamua ni namna gani na nani na nani akodishwe kupewa sehemu hizo.

Mhe. Abdalla Ali Kombo: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako mimi naona jibu la shamba la Makurunge halina uhakika, Baraza lilopita niliuliza, na kama kwenye *hansard* wamerikodi basi ipo, nilimuuliza waziri shamba letu liko wapi, na je tunalo. Jibu likawa tunawapa Chuo cha Kilimo Kizimbani, sasa leo kuna jibu kwamba Halmashauri ya Bagamoyo kwa kushirikiana na sisi watakata viwanja lakini hati imetushinda kwa sababu *cost* yake ni kubwa. Mimi naona litafutwe jibu ambalo litaturidhisha wananchi wa Zanzibar, na kama

kuna uwezekano kama hilo shamba lipo, maana sina uhakika kwa majibu haya…

Mhe. Spika: Mheshimiwa uliza swali…

Mhe. Abdalla Ali Kombo: Kwa majibu mengine, na leo majibu mengine nakuomba Mhe. Spika twende tukatizame shamba kama lipo, na ikiwezekana twende kwenye hiyo Halmashauri ya Bagamoyo na Wizara ya Kilimo twende pamoja. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, majibu yaliyopo katika maandishi yaliyosomwa na Naibu Waziri kwanza ni sahihi, shamba hili awali lilikuwa na hekta 28,000 serikali baada ya kuchelewa sana kupata hatimiliki hatimaye tukabakiwa na hekta 6,700. Hekta 6,700 zimepimwa na ndio maana akikabidhiwa rasmi Chuo cha Kizimbani kuwa ni mmiliki wa eneo hili. Kutokana na gharama za kulipia hati kama bilioni na zaidi, serikali ikafikiria ni njia gani inaweza ikapatikana hizo fedha badala ya ku-*invest one billion*, tutafute fedha za ziada ndani yake, ndipo kupitia Chuo chetu cha Kizimbani ikatangazwa *tender* ili kupata mshauri mwelekezi atushauri namna gani tunaweza tukapata fedha nyingi kwa kutumia hizi hekta 6,700 ambazo zipo, ambapo ndani yake kuna hiyo *beach* kama nilivyoeleza. *Exercise* hiyo itakapokamilika ndipo sasa tutasema kwamba tunaweza kulipia zile hati, *at the same time* tuka-*raise* pesa ndani ya hilo shamba.

Kwa hiyo, sio kweli kwamba hatunalo, hekta 6,700 tunazo ndio maana Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikabidhi Chuo cha Kizimbani rasmi, hati zipo na kila kitu kipo na ndio maana tunaendelea na mazungumzo kwa kufuata mpango wa mji wa Bagamoyo kuona ni namna gani tunaweza kukidhi yale matakwa ya mji kama ambavyo Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeelekeza.

Kwa hiyo, Mhe. Spika, majibu yetu ni sahihi, shamba liko ndani ya mikono ya serikali, tumeshakabidhiwa rasmi, nataka nichukue fursa hii kuwashukuru sana Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kukupa rasilimali ambayo unaweza uka-*raise* bilioni mia tatu si jambo la kawaida hata kidogo. Wale ambao wanakejeli Muungano wajue kwamba hii ni faida kubwa kwa serikali yetu kupata, na kwa kweli ni mapato makubwa sana tukiliendeleza eneo hili. Ahsante sana Mhe. Spika.

Nam. 6

Kuvuja kwa Jengo la Skuli ya Mtule

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Skuli ya Mtule iliyopo katika Jimbo la Paje ujenzi wake umekamilika lakini skuli hiyo inakabiliwa na tatizo la kuvuja, ukosefu wa huduma ya maji ambayo ni huduma muhimu kwa wanafunzi hao.

(a) Kwa nini skuli hiyo mpya ivuje kwa muda mfupi tangu kukamilika kwa ujenzi wake, na hatua gani zimechukuliwa ili kukarabati sehemu zinazovuja.

(b) Je, wizara imechukua hatua gani kwa mkandarasi aliyejenga skuli hiyo kwa mujibu wa mkataba wa ujenzi pamoja na mshauri muelekezi wa mradi huo.

(c) Skuli mpya kukamilika ujenzi wake na baadae kuanza kuvuja serikali haioni ni kutumia vibaya fedha za walipa kodi za wananchi pamoja na skuli hiyo kujengwa na mkopo wa Benki ya Dunia.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 6 lenye sehemu (a), (b) na (c) kwanza naomba kutoa maelezo ya utangulizi kama hivi ifuatavyo:-

Skuli ya Paje Mtule ni miongoni mwa skuli 19 za Sekondari zilizojengwa kupitia Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Lazima uliotekelezwa kwa ushirikiano baina ya SMZ na Benki ya Dunia. Mchoro uliotumika uliandaliwa na Kampuni ya *PCM Architect* ya Dar Es Salaam. Mchoro huo ndio chanzo cha kasoro ya kuvuja kutokana na maji ya mvua kupenya katika kingo za kuta na mapaa yaliyolazwa na kusababisha maji kukaa. Kasoro hizo ziligundulikana mwaka mmoja baada ya majengo kukabidhiwa na kutumika.

Pia, skuli ya Paje Mtule ilijengwa na Kampuni ya *Electric International* ya Dar es Salaam ambayo mkataba wake ulikatishwa baada ya kushindwa kukamilisha ujenzi kwa wakati na kazi iliyobakia kukamilishwa na mkandarasi mwengine

Rans Company Ltd wa Zanzibar. Baada ya maelezo hayo napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi kama hivi ifuatavyo:-

(a) Kuvuja kwa skuli ya Paje Mtule na nyenginezo zilizotumia mchoro huo ni makosa yaliyosababishwa na mchoro wa Mshauri Elekezi. Wizara imechukua hatua za dharura za kuziba sehemu zinazovujisha. Kwa sasa tatizo hilo limepungua kwa kiasi kikubwa.

(b) Mkataba wa ujenzi wa Mkandarasi Kampuni ya *Electric International* ulivunjwa kutokana na utendaji mbovu na kushindwa kukamilisha kazi kwa wakati. Mkandarasi alifungua kesi ya madai katika Mahakama Kuu ya Zanzibar na alishindwa katika dai lake na kutakiwa kutulipa fidia ya ucheleweshaji wa kukamilisha kazi. Mkandarasi baada ya kushindwa na kutakiwa kutulipa fidia ameiomba Mahakama kuipitia upya hukumu hiyo. Kesi hiyo inaendelea katika Mahakama Kuu na wizara inasubiri maamuzi ya Mahakama. Kuhusu Mshauri Elekezi Kampuni ya *PCM Architect* ya Dar es Salaam, wizara ilimchukulia hatua ya kuvunja Mkataba wa Kampuni hiyo katika kazi za mradi mwengine kwa kuchelea kutokea makosa kama hayo.

(c) Malipo ya fidia yatakapopatikana pindipo kesi hiyo tutashinda yatasaidia katika kurekebisha makosa yaliyojitokeza na kusababisha uvujishaji wa mapaa. Ahsante.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu marefu ya Mhe. Naibu Waziri na mimi ndio ajira yangu ilipo hapa tatizo hilo halijapungua Mhe. Naibu Waziri na niombe tu tufanye ziara baina ya mimi na wewe lakini isijekuwa kama ile ziara ya Mhe. Waziri wa Elimu baada ya kumpitishia bajeti yake hapa hata *Assalam alaykum* haipatikani, ni lini tutakwenda mimi na wewe ukaone hali halisi ilivyo. Nataka unihakikishie katika muda mfupi pamoja na jitihada nilizochukua kama Mwakilishi wa eneo hilo.

La pili hizi kesi za michoro zimekuwa nyingi hata Uwanja wa Ndege tuna kesi kama hiyo, serikali inajipanga vipi kuangalia utaratibu kama huu wa michoro na kipi kinachokuja mwanzo kati ya ramani na michoro, hata ikafika jengo limeshafika juu Wizara ya Elimu hamna wakaguzi hata ikafika hatua hiyo. Je, hamuoni fedha za walipa kodi zinapotea kiholela.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, katika swali mama tulisema kwamba tatizo la uvujaji limepungua, na mimi binafsi

nilifanya ziara nikakutana na mwalimu mkuu, nikakutana na wanafunzi tukalizungumzia suala hili wakasema limepungua. Lakini hata hivyo niko tayari kufuatana na Mhe. Mwakilishi kwenda katika Skuli ya Paje Mtule wakati ambapo tutapata muda.

Pili, kuhusu kesi za michoro ni kweli hili ni suala la kitaalamu, na kwa upande wetu Wizara ya Elimu baada ya kutokea tatizo hili sasa hivi tumejipanga vizuri sana kufuatilia masuala haya katika hatua mbali mbali. Kwanza baada ya mchoro kupokea tunaujadili katika vikao wakiwemo wataalamu wakati mwengine tunaalika wataalamu kuja kutufafanulia zaidi ubora wa mchoro huo udhaifu wake na kadhalika.

Pia sasa hivi katika hatua nyengine za ujenzi tunafuatilia mara kwa mara ili kuona ubora wa kazi, lakini pia na kuona muda wa kazi unathaminiwa. Kwa mfano, katika ujenzi wa Chuo cha Utalii tulikuwa tukifuatilia na tukatoa maoni yetu kwamba kwanza kuhusu ubora wa kazi, tukaeleza *concern* yetu lakini pia na wakati, na kutokana na hayo tumeanza kugundua matatizo mapema na sasa hivi tumeyafanyia kazi. Kwa hivyo, kwa upande wetu Wizara ya Elimu tumejipanga namna hiyo katika kufuatilia kazi zetu ili ziwe bora zaidi. Ahsante.

Nam. 92

Uimarishaji wa Elimu ya Watu Wazima

Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi - Aliuliza:-
Lengo kuu la elimu bila malipo ni kuwapatia elimu muhimu wananchi wote ili kuwasaidia katika maisha yao.

(a) Je, wizara ina mpango gani wa kuimarisha elimu ya watu wazima na vipi itawashirikisha katika masuala ya michezo.
(b) Je, wizara ina mpango gani wa kuzisaidia familia masikini sana katika kuhakikisha kuwa na wao hususan watoto wao wanapatiwa elimu ili iwakomboe na janga hili la umaskini.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:

Mhe. Spika ahsante, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 92 lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo.

Kwanza naomba kutoa maelezo ya utangulizi. Nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kuwa lengo kuu la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar la kutangaza

Elimu bila ya Malipo ni kuwawezesha wananchi kuitumia elimu wanayoipata katika kuinua hali ya maisha yao. Ujuzi na maarifa watakayoyapata uwawezeshe kujikwamua kiuchumi na kuweza kuwa na hali bora. Azma hiyo inaendelea kutekelezwa hadi hii leo. Baada ya maelezo hayo napenda kumjibu Mheshimiwa kama ifuatavyo:-

(a) Wizara inaendelea na juhudi za kuimarisha Elimu ya Watu Wazima kwa kuendesha kisomo kupitia madarasa ya Watu Wazima, kuanzisha maktaba katika sehemu za vijijini na kuwawezesha watu wazima kuendelea kujisomea na kwa wale walipiga hatua kuwasaidia kuanzisha vikundi vya ushirika kwa kubuni miradi mbali mbali ambayo inawasaidia kuinua kipato chao. Aidha, wanakisomo wanashirikishwa katika michezo ya aina mbali mbali kulingana na umri wao. Katika maadhimisho ya Juma la Elimu ya Watu Wazima na kisomo hushiriki katika mashindano ya michezo kama vile kuvuta kamba na shughuli nyengine za utamaduni wetu kama vile maigizo, mashairi, ngonjera na tenzi na washindi huzawadiwa.

(b) Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imewapunguzia wananchi gharama za elimu kwa watoto wao kwa kufuta michango ya wanafunzi katika skuli zote za msingi za serikali. Serikali ilizipatia skuli zote za maandalizi na msingi chaki na madaftari ya kuandikia kwa wanafunzi wote na skuli zote zilipatiwa Shs. 500,000/= kwa ajili ya gharama za matengenezo madogo madogo au malipo ya umeme na maji.

Kwa upande wa skuli za sekondari, serikali imechukua jukumu la kulipia ada zote za mitihani kuanzia Mitihani ya Kidato cha Pili, Kidato cha Nne na Kidato cha Sita. Hatua hizo zote zimesaidia sana katika kuwawezesha wanafunzi kutoka familia masikini kupata elimu bora. Vile vile, wanafunzi walioacha masomo njiani wanahamasishwa kurudia tena masomo yao kwa kujiunga na Vituo vya Elimu Mbadala au madarasa ya Elimu Mbadala. Ahsante.

Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi: Mhe. Spika, ahsante sana na ahsante Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri sana aliyoyatoa kujibu swali langu nililoliuliza. Kwa kweli swali hili linabeba historia ya Zanzibar, historia imetueleza jinsi gani wanyonge wa Zanzibar walivyokuwa wakipata tabu na maisha na jinsi gani walivyokuwa wanakoseshwa elimu ambayo ingeweza kuwakomboa wakati ule na ndio ilipofika mwaka 1964 yalipofanywa Mapinduzi...

Mhe. Spika: Mheshimiwa jielekeze kwenye swali usihutubie.

Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi: Sawa nitakwenda kwenye swali, nilitaka kufafanua kidogo ili nieleze. Ninachotaka kusema ni kwamba, iko haja ya kuweka mkazo mkubwa sana kwenye kuwaelimisha watu wazima. Kwa sababu kuna watu wengi sana duniani ambao wamesoma wakiwa watu wazima wameendelea hadi wamefikia *PhD* na wengine ni ma-*professor*. Sasa niulize swali tu, hapa kwetu ni watu wazima wangapi wana viwango vya *degree* au *certificate* au chochote kile, halafu ni wangapi kwa ujumla wao ambao tunao watu wazima wanahitaji kupata elimu ya watu wazima? Kuna mpango gani wa kuwahamasisha wale wengine ambao bado hawajataka kuingia kwenye hiyo elimu ya watu wazima.

Jengine, kwa sababu wengine wanasoma masomo ya *primary*, wengine ...

Mhe. Spika: Mheshimiwa jaribu kufupisha swali lako.

Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi: Sasa najiuliza kwamba hivi karibuni lilifanywa Tamasha la Elimu sasa vijana walishiriki, watoto wadogo walishiriki, lakini sikuwaona watu wazima kushiriki pale, sijui ni kwa nini hatuwashirikishi na wao wakajiona kama wanafunzi wengine.

Mhe. Spika: Ahsante Mheshimiwa kwa maswali yako mawili. Mhe. Waziri jibu swali hili la mwisho tu, kwa nini watu wazima hawafikiriwi kwa sababu lile la mwanzo ni la kitakwimu na sidhani kama una majibu hapo. La mwisho kwa nini watu wazima hawakushiriki kwenye Tamasha la Elimu bila ya Malipo wameshiriki watoto na vijana.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, ni kwamba wizara ina matamasha ya aina mbili makubwa, kuna Tamasha la Elimu ambalo tunaita Elimu bila Malipo na kuna Tamasha la Juma la Elimu ya Watu Wazima. Hili Juma la Elimu ya Watu Wazima limekusudiwa zaidi kwa watu wazima wanaojifunza katika ngazi mbali mbali kuanzia wanakisomo, wajasiri amali na wengine wa viwango mbali mbali na hili jengine linawahusu zaidi wanafunzi wetu katika ngazi za maandalizi, msingi, sekondari na vyuo. Kwa hivyo, kila mmoja tamasha lina wahusika wake wakubwa zaidi, lakini hata hivyo, kama ni ushauri basi tutachukua kwamba kushirikisha wahusika wote katika matamasha yote bila kujali viwango vinavyohusika katika siku zijazo.

Mheshimiwa samahani kidogo, kuhusu hili swali la takwimu lakini pia takwimu zake ni ngumu kupatikana kutokana na fasili yenyewe ya watu wazima iko vipi. Tukisema kwamba waliopitia katika vituo vyetu vya kisomo wakajifunza kusoma na kuandika au kwa tafsiri nyengine mpaka wanaojiendeleza baada ya *Form II* pia tunawaita ni watu wa elimu ya watu wazima vile vile. Kwa mfano, amefeli *Form II* halafu akajiendeleza *Form III* na *Form IV* wanaingia katika mkondo wa elimu ya watu wazima. Sasa masuala kama hayo ni vigumu kuyapatia takwimu zake kutokana na kwamba ile fasili yenyewe tu ya watu wazima ina mashaka yake. Ahsante sana.

Mhe. Spika: Swali hili limekula muda mwingi, Katibu kwa wizara inayofuata.

Nam. 3

Uharibifu wa Mazingira Kutokana na Uchimbaji Kifusi

Mhe. Mussa Foum Mussa - Aliuliza:-

Kwa muda mrefu sasa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji wakati inapojenga barabara za Kusini, Pemba huchimba kifusi katika Shehia ya Mwambe na kwa sasa kumekuwa na mashimo makubwa sana, na wananchi wanashindwa kutumia tena sehemu hizo kwa kilimo.

(a) Je, kuna mpango gani wa kupunguza athari hizo.
(b) Je, serikali inatoa tamko gani kwa wananchi juu ya kufukiwa mashimo hayo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 3 lenye vifungu (a) na (b) linalohusu machimbo ya kifusi huko Mwambe ambayo tunayatumia kwa ajili ya ujenzi wa barabara za Pemba kama hivi ifuatavyo:-

a. Kwa kufuata muongozo wa Idara ya Mazingira, machimbo hayo hivi sasa tumeyarudishia udongo ili yaweze kutumika kwa shughuli nyengine.

b. Tamko la serikali ni kwamba, kwa kuwa tayari tushayafukia hayo mashimo kwa mujibu wa maelekezo kutoka Idara ya Mazingira tunawaambia wananchi sasa hivi wanaweza kuyatumia mashimo hayo kwa shughuli za kilimo na ufugaji wa samaki na tayari wananchi wa

eneo hilo wanatumia maeneo hayo kwa kazi za kufuga samaki. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Mussa Foum Mussa: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri yasiyoridhisha sana ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali dogo la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa mimi ni mkaazi wa Shehia ya Mwambe na Mhe. Naibu Waziri amejibu kwamba mashimo hayo yameshaanza kufukiwa.
Je, ni lini kazi hiyo ilianza kwa sababu mimi natoka huko huko.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Spika, nakubali kwamba yeye ni mkaazi wa huko na mimi nilipokwenda katika ziara yangu mpaka nyumba yake pia nimeoneshwa. Napenda kumhakikishia kwamba nimekwenda na afisa kutoka Idara ya Mazingira na nimekutana na watu ambao hivi sasa wanafanya shughuli ya ufugaji wa samaki, na mimi nimestaajabishwa sana kwa sababu sehemu ile na maji ya chumvi ni mbali kidogo, lakini samaki wale ni wa maji ya chumvi kabisa. Kwa hiyo, mimi nataka kumwambia rasmi kwamba nimekwenda na nimeiona hiyo shughuli yenyewe kwa uhakika kabisa na wananchi wa kule sehemu ya Mwambe anayoisema basi mimi nimezungumza nao na wakashukuru kwa kazi tuliyoifanya. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Ahsante Mheshimiwa kwa sababu ya wakati tutaendelea na ninakusudia kuyamaliza haya maswali yote. Naomba sasa nimwite Mhe. Ali Suleiman Ali, Mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Kijitoupele aulize swali lake.

Nam. 12

Upandishaji wa Bei kwa Vyombo vya Baharini

Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) - Aliuliza:-

Tatizo la usafiri wa vyombo vya baharini kupandisha bei za tiketi bila ya mpango, linapelekea malalamiko kwa wananchi wanaosafiri kwa kutumia vyombo hivyo. Kwa kuwa tatizo hilo lipo hivi sasa na linaendelea.
Je, wizara ina mpango gani wa kulikemea tatizo hilo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 12 kama ifuatavyo:-

Kwanza naomba nikiri kwamba ni kweli kulijitokeza baadhi ya Kampuni za Meli kupandisha nauli za usafiri kiholela pasi na kuishirikisha mamlaka husika. Hivi karibuni ilitokea kampuni moja kupandisha nauli kutoka shilingi 25,000/- hadi shilingi 27.000/- kwa daraja la *economy* bila kuijulisha au kuishirikisha Mamlaka ya Usafiri Baharini (*ZMA*), ambayo ndiyo yenye dhamana ya kusimamia usafiri wa baharini.

Baada ya kutokea tatizo hilo Mhe. Waziri alilikemea suala hilo na kutaka lisitishwe mara moja na baada ya hapo Mamlaka ya Usafiri Baharini walikaa na mmiliki wa kampuni hiyo na matokeo yake baada ya kumuelewesha taratibu zetu alikubali na hivi sasa bei ya nauli imerejea kama ilivyokuwa hapo awali.

Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata): Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri napenda kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa kwanza nampongeza sana Mhe. Waziri Ali Karume pamoja na Naibu wake, baada ya kutokea kadhia hii wananchi wetu imani iliwatoka, lakini baada ya kuonekana kwenye vyombo vya habari na suala lile kweli likakaa sawa hili niipongeze taasisi yake. Lakini je, kwa kuweka juhudi zaidi kwa sababu mambo haya hutokea sana siku za Ijumaa na Jumamosi wasafiri kutoka Unguja na wasafiri wanaotoka Bara kuja huku huwa ni adha, wana ushauri gani au maelekezo gani zaidi kwa wafanyabiashara wa vyombo hivi kuondoa kabisa tatizo hilo lisiendelee.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Spika, ni kweli hili suala lilikuwepo kwa muda mrefu na mimi mwenyewe nilifanya ziara ya kushitukiza pale bandarini na nikakutana na wale wadau tofauti wakiwemo mapapasi ambao wanapandisha bei. Baada ya kukaa na mamlaka hivi sasa tuna mkakati mzuri wa kuhakikisha kwamba bei hazitopanda kiholela na vile vile kama tunavyojua sote serikali ipo katika mpango kabambe wa kuhakikisha kwamba inanunua meli nyengine ya abiria ili kwenda sambamba na makampuni haya, ili kuhakikisha bei hazipandi tena. Mhe. Spika, ahsante sana.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe muda wa maswali umekwisha lakini kuna swali moja limebaki na ningepeda tulimalize. Kwa hiyo, nitatumia muda mchache ili tuweze kulimaliza hili swali la mwisho kwa sababu tulikuwa na shughuli nyingi hapa mwanzo kabla ya kuanza maswali. Katibu kwa wizara inayofuata.

Nam. 46

Athari za Mabadiliko ya Tabia Nchi

Mhe. Suleiman Makame Ali - Aliuliza:-

Pamoja na jitihada za serikali kusimamia na kulishughulikia suala zima linalohusiana na mabadiliko ya tabia nchi, bado kumekuwepo na tatizo la mashamba mengi kuingia maji ya chumvi na kupelekea uzalishaji wa mpunga kuwa katika kiwango cha chini, hali inayopelekea wananchi kukosa chakula cha uhakika, hasa katika maeneo ya vijiji vya Uchangani, Kambaga – Kichanjaani, Mkunguni na Mkumbuu vilivyopo katika Jimbo la Ziwani.

a) Je, serikali inayo taarifa kuhusiana na kuwepo kwa kadhia hii katika vijiji hivi.

b) Je, kama inajua, serikali imechukua hatua gani mpaka sasa ili kuizuia hali hiyo isiendelee tena.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira - Alijibu:-
Mhe. Spika, kwa idhini yako napenda kumjibu Mheshimiwa swali lake lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Serikali inayo taarifa kuhusiana na kuwepo kwa kadhia aliyoieleza katika vijiji alivyovitaja ndani ya Jimbo la Ziwani.

b) Hatua ambazo zimechukuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar mpaka sasa ni pamoja na:-

1) Kuwaelimisha na kuhamasisha wananchi katika upandaji wa Mikoko/Mikandaa kulingana na uwezo wao katika maeneo yao na ujenzi wa matuta katika baadhi ya maeneo yaliyoathirika. Ahsante sana.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Mhe. Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri lakini wakulima wetu hususan maeneo ya Ndagoni kama vile maeneo yalivyoelezwa kwenye swali mama, Kijiji cha Uchangani na pale Tibirinzi, Chake Chake wamekata tamaa kabisa kwa kilimo cha mpunga.

Je, serikali kupitia wizara yake ina mpango gani kuhakikisha kupiga angalau matuta/mikuko ya kuzuia chumvi hii isiingie katika mashamba yale.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, tumesikia na tumelichukua na tutafanya kama ambavyo tunaendelea kufanya katika maeneo mengine yaliyoathirika. Ahsante.

Mhe. Spika: Ahsante Mheshimiwa, muda wa maswali umekwisha.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mheshimiwa kuhusu utaratibu.

Mhe. Spika: Mheshimiwa nisubiri kwanza, Spika akisimama Mjumbe atakaa. Waheshimiwa Wajumbe taarifa ya wageni. Wageni waliopo ni wageni wa Mhe. Miraji Khamis Mussa, Mwakilishi wa wananchi Jimbo la Chumbuni; wakiongozwa na Mbunge wa jimbo hilo Mhe. Ussi Salum Pondeza, pamoja naye amefuatana na Mhe. Haji Juma Kibuji, Mwenyekiti wa Jimbo; Ndugu Mussa Idrissa, Diwani wa Chumbuni, Ndugu Mussa Mohammed, Katibu wa Jimbo na Bwana Haji Mngwali. Karibuni sana Baraza la Wawakilishi. *(Makofi)*

UTARATIBU

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika ahsante sana, nimesimama kwa Kanuni ya 42, Mhe. Spika sijui kama utaniruhusu nisome au inatosha tu.

Mhe. Spika: Kanuni ya 42 naam.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Hoja ya kujadili jambo la dharura.

42 (1) "Baada ya muda wa maswali kuisha, Mjumbe yeyote anaweza kutoa hoja kuwa Baraza liakhirishe shughuli zake zilizoonyeshwa katika Orodha ya Shughuli za Baraza, na lijadili jambo la dharura na muhimu kwa Umma kwa ruhusa ya Spika".

Mhe. Spika, jambo lililotokea hivi karibuni waziri msomi Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira alipandisha bei ya umeme kwa asilimia 20 wakati sheria haimruhusu. Kwa kukiuka sheria ambayo tumeipitisha sisi Baraza la Wawakilishi kifungu cha 36 Mhe. Spika, cha Sheria ya *ZURA* kinachotaka wananchi kushirikishwa katika kutoa maoni yao kabla ya bei mpya ya huduma za umeme, maji na mafuta hazijatangazwa. Jambo hili halijafanyika kwa mujibu wa masharti ya kifungu hiki, hali ya kuwa lipo kisheria na matokeo yake bei ya umeme imepandishwa bila ya wananchi waliopandishiwa bei hiyo kutoa maoni kama sheria inavyotaka.

Mhe. Waziri sheria haimruhusu kupandisha umeme na mwenye mamlaka ni *ZURA* na kifungu cha 36 kimeeleza wazi, wadau au pahali pa kutoa masharti paelekezwe na wadau, *public hearing* haikufanywa, kwenye Gazeti Rasmi haikutangaza, kama Nipashe au Uhuru magazeti muhimu ripoti ya wadau haipo. Mheshimiwa nataka muongozo wa kiti chako.

Mhe. Spika: Ahsante Mheshimiwa nimekusikia kwa bahati nzuri na serikali yenyewe pia imesikia, lakini nadhani mimi ningekushauri hoja yako uiweke vizuri halafu waletee serikali, wakabidhi serikali halafu nafikiri Mhe. Waziri atakuwa na majibu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nakuomba Mheshimiwa ili sisi tuendelee wewe nenda kaiweke vizuri hiyo hoja, waziri mwenyewe muhusika yupo na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais yupo hapa, utawaletea hiyo hoja yako halafu wao watakwenda kuifanyia kazi na baadae tutapata majibu, watatoa maelezo humu kama serikali. Ahsante.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, nakushukuru ahsante.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Spika, nikushukuru kwa kuniona. Mhe. Jaku Hashim Ayoub ametumia kifungu 42 kuhusu jambo la dharura na kutaka Baraza lako tukufu liakhirishe baadhi ya mambo yake ya leo ili kujadili suala hili la dharura.

Mhe. Spika, jambo hili ukimwambia Mhe. Jaku Hashim Ayoub akaweke hoja uzuri itakuwa sio hoja ya dharura, na dharura ni hii ambayo tutaiona hapa itajadiliwa kwa muda huu ili basi wananchi ambao wanamwakilisha Mhe. Jaku Hashim wapate kuiona na wananchi wa Zanzibar nzima, hii kadhia ni kadhia ya nchi nzima na hata sisi inatuhusu.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, kwa idhini yako tungekuomba uturuhusu, kiti chako kiweze kuiruhusu hoja hii ili tuijadili kwa dharura na serikali iweze kutoa majibu. Jambo hili si jepesi kama mnavyoliona Mhe. Spika, nakushukuru. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante kwa msisitizo wako Mheshimiwa, hoja tumeisikia na wanaopaswa kuja kutuletea majibu ni serikali, Mheshimiwa kaita hoja ya dharura nafikiri ni hoja ya kupandisha umeme nafikiri bei za umeme zimepanda na hoja yake kwamba Mhe. Waziri hakufuata taratibu na nimemshauri Mheshimiwa aende akae pamoja na Mhe. Waziri na serikali ipo hapa ili kesho watatuletea majibu.

Nadhani tunakuwa tuko vizuri sana kuliko kuwalazimisha watujibu hapa sasa hivi halafu majibu yatakuwa hayana uhakika sana. Mheshimiwa kaitengeneze vizuri hiyo hoja kama nilivyokuelekeza uwasilishe serikalini, kesho serikali itatuletea majibu. Ahsante, tunaendelea.

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Kufuta na Kutunga Upya Sheria ya Ushahidi Sura ya tano na masuala yanayohusiana nayo

(Kusomwa mara ya Pili)

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, awali ya yote nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia asubuhi ya leo kufika hapa kwa salama na amani na kunipa wakati kuweza kuwasilisha mswada wetu huu.

Mswada huu ambao nawasilisha Mapendekezo ya kufutwa sheria ya ushahidi sura ya tano ya Sheria ya Zanzibar na kutungwa sheria mpya ya ushahidi ya mwaka 2016 ili iendane na hali halisi ya mabadiliko ya Sayansi na Teknolojia katika upatikanaji, ukusanyaji na utoaji, uwasilishaji na uchambuzi na kukubalika kwa usahihi.

Mhe. Spika, sheria ya ushahidi Zanzibar ni kama ilivyo sheria nyengine zilipokelewa kutoka India na ilitungwa mwaka 1917 na hadi sasa haijawahi kufanyiwa marekebisho yoyote licha ya kwamba ifikapo mwezi wa Januari 2017 sheria hii itakuwa imeshafikisha umri wa miaka 100.

Kwa kuzingatia maendeleo na mabadiliko ya kijamii yaliyojitokeza kuanzia wakati huo hadi sasa ni dhahiri kwamba sheria hii imepitwa na wakati na inahitaji kufutwa na kuandikwa upya.

Mhe. Spika, ni ukweli usiopingika kwamba ukuaji wa Sayansi na Teknolojia umeibua mbinu nyingi mpya za makosa ambayo ni changamoto katika utoaji wa haki hasa kwa vile matumizi ya karatasi yamepungua na badala yake matumizi ya kompyuta na nakala laini yamekuwa makubwa yaani *soft copy*. Kufuatia mabadiliko hayo ushahidi wa kisayansi umekuwa na umuhimu mkubwa katika uendeshaji wa kesi za jinai na madai. Sheria ya ushahidi ya sasa haina vifungu vinavyoruhusu matumizi ya ushahidi huo na pia imekosa vifungu muhimu vya kukabiliana na changamoto kadhaa.

Mhe. Spika, mapendekezo yaliomo katika waraka huu yanakwenda sambamba na utekelezaji wa Dira ya Zanzibar ya mwaka 2020 ambayo miongoni mwa shabaha zake ni kuhakikisha utawala wa kisheria unazingatia mapendekezo haya, pia ni sehemu ya utekelezaji wa mpango wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupunguza umasikini yaani MKUZA II 2020 mpaka 2050 unaelekeza haja ya kuimarisha mfumo wa sheria na kuweka mpango wa kutoa haki kwa wakati na kuondosha unyanyasaji wa aina zote.

Aidha hatua hii ni sehemu ya mpango wa mabadiliko katika sekta ya sheria ambayo miongoni mwa malengo yake ni kuwepo kwa sheria zinazoendana na wakati.

Mhe. Spika, utafiti uliofanywa na Tume ya Kurekebisha Sheria ya Zanzibar umeonesha kuweko kwa udhaifu na upungufu mkubwa wa Sheria ya Ushahidi kuhusiana na upatikanaji, ukusanyaji, utoaji, uwasilishaji na uchambuzi wa kukubalika kwa ushahidi hali ambayo imechangiwa kwa kiasi kikubwa na maendeleo ya Sayansi na Teknolojia na mabadiliko ya kijamii na kiuchumi.

Mhe. Spika, kutokana na hali hiyo kuna umuhimu wa kufutwa na kutungwa upya kwa sheria ya ushahidi ili kuongeza wigo katika upatikanaji wa ukusanyaji, utoaji, uwasilishaji na uchambuzi na kukubalika kwa ushahidi.

Aidha mabadiliko hayo yatawezesha sheria hiyo kuendana na wakati uliopo, hivyo kuelekea kuimarika kwa utoaji wa haki katika jamii. Kwa maana hiyo sheria mpya iliyopendekezwa itawezesha kukubalika kwa aina tofauti za ushahidi ambazo hazimo katika sheria ya sasa na hivyo kufanya upatikanaji wa haki kuwa mpana zaidi na kwa uwazi zaidi kwa kuzingatia misingi ya katiba na sheria ya nchi na mikataba mbali mbali ya kimataifa inayohusu haki za binadamu.

Mhe. Spika, mapendekezo ya kutungwa sheria mpya yataweza kukubalika kwa ushahidi wa kielektroniki ikiwemo barua pepe, nukushi, simu na video. Pia mapendekezo haya yatazingatia utapikanaji wa ushahidi wa makosa ya unyanyasaji wa kijinsia hasa kwa watoto, wanawake na watu wenye ulemavu wa akili jambo ambalo ndio kilio kikubwa cha jamii hasa katika kesi za udhalilishaji.

Faida na mapendekezo ya sheria mpya. Mhe. Spika mapendekezo ya sheria mpya yanatarajiwa kuleta faida kadhaa zikiwemo:

Kwanza, kukubalika kwa haki na kumbukumbu za kielektroniki ambazo katika sheria iliyopo haitambuliwi.

Pili, kuwezesha mashahidi waliopo nje ya nchi ambao upatikanaji wao unakuwa mgumu na gharama na kutoa ushahidi kwa njia ya *video link*.

Tatu, kukubalika kwa ushahidi wa kiintelijensia,

Nne, kukubalika kwa ushahidi usio wa kiapo wa mtoto mdogo bila ya kuhitaji kuungwa mkono na ushahidi mwengine, baada ya Mahakama kujiridhisha kuhusu uhakika wake.

Tano, kupokea kwa ushahidi wa mtu mmoja mtoto au muathirika kwa kosa la udhalilishaji,

Sita, kukubalika kwa matumizi kwa njia maalum ya mashahidi na makundi maalum yakiwemo ya walemavu, wanawake, watoto na waathirika wengine kadiri mahakama itakavyohisi inafaa.

Mhe. Spika, sheria hii mpya itasaidia sana katika kupanua wigo upatikanaji wa ushahidi pamoja na kupambana na makosa ya udhalilishaji wa kijinsia kwa wanawake na watoto na watu wenye ulemavu ambao sasa wamekuwa waathirika wakubwa wa matendo ya udhalilishaji kwani sheria hii sasa imeweka mazingira mazuri na rafiki kwa mashahidi wa aina hii.

Kwa mujibu wa sheria hii mtoto aliyefanyiwa matendo ya udhalishalishaji anaweza kutoa ushahidi yeye mwenyewe na ushahidi wake kukubalika Mahakamani bila ushahidi huo kuungwa mkono na ushahidi wa mtu mwengine jambo ambalo lilikuwa halikukubalika katika sheria ya zamani.

Mhe. Spika, ili kuepuka uwezekano wa ushahidi hasa katika kesi ya udhalilishaji kushindwa kutoa ushahidi kutokana na sababu mbali mbali zikiwemo vitisho kutoka kwa mtu aliyemfanyia matendo ya udhalilishaji, aibu, hofu au kutokana na mtu mwengine wa kimaumbile yanasababishwa na ulemavu.

Sheria hii mpya imeipa uwezo mahakama kuruhusu matumizi ya njia maalum ikiwemo kutenganisha mashahidi na watu wengine, kuruhusu kutumia visaidizi vya mawasiliano kwa mtu mwenye ulemavu wa kusikia na visaidizi vyenginevyo, kuruhusu matumizi ya *video link*, hatua zote hizi zimechukuliwa kuhakikisha kwamba walemavu watoto na waathirika wengine wa matendo ya

udhalilishaji wanaweza kutoa ushahidi wa uhuru zaidi na kusaidia katika kuwatia hatiani wahalifu wa matendo hayo.

Mhe. Spika, mapendekezo haya ya sheria ya ushahidi yamefikiwa baada ya hatua za ukusanyaji wa maoni kutoka kwa wananchi wote wa wilaya zote za Unguja na Pemba na taasisi mbali mbali zikiwemo Afisi ya Mwanasheria Mkuu, Mahakama, Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, Jeshi la Polisi, Chuo Kikuu cha Taifa cha Polisi, Vyuo vya Mafunzo, Afisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Benki ya watu wa Zanzibar, Chuo Kikuu cha Taifa SUZA na Chuo cha Usimamizi wa Fedha.

Pia ushauri kutoka katika Taasisi zisizokuwa za serikali ikiwemo chama cha wanasheria wanawake, Kituo cha huduma za Sheria Zanzibar, chama cha wanasheria Zanzibar, Chuo Kikuu cha Zanzibar pamoja na wataalamu wa Teknolojia ya Habari, Mawasiliano na Kampuni za simu *TTCL* na *Zantel* vile vile.

Mapendekezo

Mhe. Spika, yafuatayo ni baadhi ya mambo mbali mbali ya sheria mpya ya ushahidi yanayopendekezwa yawemo.

Jina la sheria kuwa sheria ya ushahidi ya mwaka 2016 kuongezewa tafsiri ya maneno mbali mbali kama vile kompyuta, hati ambayo tafsiri yake inajumuisha hati za kielektroniki, kumbukumbu, Afisa wa polisi, gazeti rasmi, mtoto na Mahakama.

Kukubalika kwa ushahidi wa kielektroniki, maungamo mbele ya hakimu, maungano dhidi ya mshtakiwa mwenza, kutengenishwa maungano na kukubali kumbukumbu za kibiashara, maingizo katika madaftari ya hesabu, kuondosha maneno ya kiutawala ya kikoloni.

Ushahidi utakaopatikana kwa njia ya kiitelejensia, kuingiza maneno ya kumbukubu za kielektroniki, kukubalika kwa hukumu katika mwenendo wa jinai kama ushahidi, kuratibu kuhusiana na ushahidi na saini ya vijiti, kumbukumbu na makosa ya zamani mambo au matukio ambayo mahakama inatakiwa kuchukua indhari na ufahamu, kuchukua ushahidi wa njia ya *video conference*, utaratibu wa shahidi za nyaraka zilizokusudiwa, kuondosha maneno ya vifungu ambavyo vimepitwa na wakati, dhana ya ukusanyaji wa sheria ya uhukumu kesi ya iliyoripotiwa, masharti maalum ya ushahidi kuhusiana na kumbukumbu za kieloktroniki na vifungu vya ushahidi

vinavyohusu ushahidi wa mtoto mdogo na ushahidi wa makosa ya udhalilishaji na mamlaka ya Jaji Mkuu kutunga kanuni kuhusiana na masuala ya ushahidi.

Hitimisho

Mhe. Spika, mswada huu umebainisha mapendekezo ya sheria ya ushahidi yaliyoelezwa katika mswada huu. Ni imani yangu kwamba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu watajadili taarifa hii kwa kina huku wakizingatia kwamba kwa kipindi kirefu sana Zanzibar tumekuwa na sheria ya ushahidi ambayo ilikuwa haiendani na wakati wa sasa na kusababisha matatizo kadhaa katika jamii.

Aidha kilio kikubwa cha kutotiwa hatiani kwa watuhumiwa kwa vitendo vya udhalilishaji wa watoto, wanawake, walemavu na watu wengine kulikuwa kunachangiwa sana na upungufu wa sheria ya sasa ya ushahidi. Hivyo, kupitishwa kwa sheria hii mpya ya ushahidi kutasaidia sana katika kupambana na matatizo hayo.

Shukrani

Mhe. Spika, napenda kuchukuwa nafasi hii kumshukuru sana hasa Mwenyekiti wa Tume ya kurekebisha Sheria pamoja na Kamati yetu ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza la Wawakilishi kwa mchango wao na msaada wao na muongozo wao.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Machano Othman Said: **(Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala):** Mhe. Spika, awali ya yote napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia amani na afya njema iliyotuwezesha kukutana kujadili mswada huu muhimu wa sheria ya kufuta na kutunga upya sheria ya ushahidi sura ya tano na masuala yanayohusiana nayo mbele ya Baraza lako tukufu.

Mhe. Spika, pia naomba kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe binafsi kuwasilisha mbele ya Baraza lako mswada huu unaolenga kuondosha au kupunguza kiasi kikubwa cha changamoto zote za ushahidi ambazo

zinasababisha kusimama na kushindwa kuendelea kwa kesi katika mahakama zetu za Zanzibar.

Sheria ya ushahidi tulionayo hivi sasa imekuwa ikilalamikiwa sana kwamba imeshindwa kukabiliana na changamoto za makosa mengi hasa yanayohusiana na watoto.

Mhe. Spika, kamati yangu kupitia kanuni ya 113 (f) ya Baraza la Wawakilishi ya mwaka 2012 imeweza kushughulikia vyema agizo la kanuni hiyo na kuhakikisha kuwa mswada huu umekuwa na ubora wenye mazingatio ya vipengele vyote ambavyo ni muhimu katika mustakabali wa uendeshaji wa kesi na kuakisi maisha halisi ya Mzanzibari kwa kuzingatia mila, desturi zao pamoja na itikadi zao za kisiasa kiuchumi na kijamii.

Mhe. Spika, sheria ya ushahidi ambayo inatumika wakati huu ni sheria ambayo tumerithi wakati wa Ukoloni ambapo ikifika Januari 2017 itatimiza miaka mia moja, hivyo ni dhahiri kwamba maisha tuliyonayo wakati huu wa utandawazi ni tofauti na maisha yale ya miaka mia moja iliyopita wakati ambao ilitungwa sheria hii. Aidha, kamati yangu inakubaliana na uamuzi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuifuta sheria hii na kuitunga upya kwa mujibu wa maisha ya wazanzibari wa leo na wakati ambao tunaenda nao uliogubikwa na changamoto nyingi za kitaalamu, kiuchumi na kijamii.

Mhe. Spika, kamati yangu inaishukuru Tume ya kurekebisha sheria Zanzibar chini ya Mwenyekiti wake Jaji Mshibe Ali Bakari pamoja na Makamishna wote ambao walishirikiana kwa pamoja kuifanya kazi hii ndani ya kipindi cha miaka mitano na kuhakikisha kwamba Zanzibar imepata sheria mpya ambayo haitomnyima mtu yeyote fursa na haki yake ya ushahidi ya kupambana na vitendo vya ukatili na unyanyasaji dhidi ya makundi maalum ikiwemo watoto, wazee wasiojiweza, watu wenye ulemavu na wanawake ambao ndio waathirika wakuu wa sheria hii.

Aidha, Kamati yangu imefarijika sana kutokana na Sheria hii mpya kutoa fursa kwa watoto ambao wamekuwa wakidhalilishwa kwa vitendo vya ubakaji na ulawiti kutoa ushahidi wao na kukubalika Mahkamani.

Mhe. Spika, zaidi ya hayo, niipongeze wizara ya nchi Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa kazi nzuri waliyoifanya kwa ushirikiano wao na Afisi ya Mwanasheria Mkuu pamoja na taasisi nyengine ambazo zilishiriki katika kufanikisha mswada huu muhimu, ni wazi kuwa

kupitishwa kwa mswada huu kutaleta ufanisi mkubwa wa uendeshaji wa kesi katika mahakama zetu kwa ngazi zote.

Mhe. Spika, kabla sijaanza kutoa maoni ya kamati yangu, kwanza kabisa naomba kuchukua nafasi hii kumshukuru sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mweyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kuwateuwa Wajumbe wawili waliokuwa katika Kamati yetu kuwa Manaibu waziri, nao ni Mhe. Mihayo Juma N'hunga (Naibu waziri Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais), na Mhe. Shamata Shaame Khamis (Naibu waziri, wizara ya nchi Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ. Kamati inawapongeza sana na kuwatakia uendeshaji mwema katika majukumu yao ya kazi.

Mhe. Spika, Vile vile napenda kuwashukuru wajumbe wa kamati yangu kwa michango yao mikubwa waliyoitoa wakati wa kupitia mswada huu ambayo imeweza kuboresha sheria hii mpya tunayoitarajia kuitumia mara tu baada ya kupitishwa ndani ya Baraza na kusainiwa na Mhe Rais, sasa naomba uwatambue, wajumbe waliounda kamati hii, kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Machano Othman Said	Mwenyekiti
2. Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis	M/Mwenyekiti
3. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa	Mjumbe
4. Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Mjumbe
5. Mhe. Nadir Abdulatif Yussuf	Mjumbe
6. Mhe. Ali Khamis Bakar	Mjumbe
7. Ndg. Rahma Kombo Mgeni	Katibu,
8. Ndg. Ali Alawy Ali	Katibu

Mhe. Spika, baada ya utangulizi huo, naomba sasa uniruhusu nieleze baadhi ya marekebisho na mapendekezo mbali mbali ambayo Kamati yetu imeyafanya.

Pia, naomba kuwatanabahisha Waheshimiwa Wajumbe kwamba, hotuba hii inatoa ufafanuzi wa baadhi tu ya vifungu ambavyo vimependekezwa na kufanyiwa marekebisho na Kamati, hivyo maelezo zaidi ya mapendekezo hayo yamo katika muhtasari wa marekebisho yetu ambayo Waheshimiwa Wajumbe tayari mumeshapatiwa.

Mhe. Spika, tukianza na sehemu ya kwanza kabisa ya mswada huu katika kifungu cha 3, ambacho kinatoa tafsiri ya maneno yaliyotumika. Kamati yangu inashauri kuingizwa tafsiri ya maneno mapya ambayo ni "Mtaalamu**",**

“Mkalimani” **, “**Ndoa” na “waziri**”** ili kukidhi haja ya ufafanuzi uliokusudiwa ndani ya sheria hii.

Mhe. Spika, kamati yangu imependekeza kutolewa tafsiri ya “ndoa” badala ya **“**mke au mume**”** kutokana na kupata wasi wasi na tafsiri hii kwani kwa kuzingatia tafsiri iliyotolewa na mswada huu ina uwezo wa kuzitambua ndoa za jinsia moja ambazo zinapingwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar lakini hata Jamhuri ya Muungano wa Tanzania haizitambui, hivyo kuzitambua sheria nyengine za ndoa nje ya Zanzibar ambazo zinatambuliwa na mamlaka zenye uwezo, kunazipa uwezo ndoa zisizo halali kwa sheria na taratibu zetu za nchi, hivyo kutumia tafsiri hii itakuwa ni tatizo hasa tukizingatia kuwa dunia imepata changamoto kubwa ya ndoa hizi na zinatambulika na mamlaka zenye uwezo kwa kuzisimamia kisheria. Kamati yangu inashauri kupitia sheria hii tafsiri ya “mume au mke” itolewe na badala yake kuingizwa tafsiri ya neno “Ndoa”.

Mhe. Spika, aidha katika kuongeza ubora na kupunguza aya zenye utata, ni vyema katika kifungu cha 26(b) tukakitoa kabisa. Kamati yangu inashauri hivyo kwa sababu maana ya kifungu hiki tayari imeelezwa mbele yake katika kifungu cha 27.

Mhe. Spika, katika kifungu cha 54 ambacho kinatoa maoni yanayohusiana na matumizi imani yanapohusika, ni bora katika kifungu kidogo cha (b) kinachoeleza “katiba na serikali ya dini yeyote au jumuiya za misaada;” kibadilishwe na mantiki yake iwe ni uanzishwaji na uongozi wa taasisi za kidini na jumuiya zake; kwa sababu kifungu hicho kimelenga kuonesha miongozo na taratibu za taasisi za kidini na jumuiya zao .

Mhe. Spika, kamati yangu inapongeza sana juhudi za serikali kupitia Tume yake ya kurekebisha sheria, kupitia mswada huu kwa kuzingatia matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano na mfumo mzima wa kidijitali ambao umeenea ulimwengu mzima. Hili ni jambo jipya katika sheria zetu kuanza kutambua matumizi ya teknolojia hii ambayo itatoa msaada mkubwa katika kufanikisha malengo ya Sheria hii. Kwa hivyo, baada ya kupita Sheria hii, matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano itaweza kutumika kwa kutoa ushahidi pale inapohitajika.

Mhe. Spika, kuingizwa kwa vifungu (kifungu cha 66, kifungu cha 103 na kifungu cha 104) vinatoa uwezo wa Mahkama kusikiliza na kupata ushahidi kutoka sehemu yoyote ndani au nje ya Zanzibar kwa kadri Mahkama itakavyojiridhisha kutoka pande zote za mashtaka, pia itapunguza changamoto za kukosekanwa kwa ushahidi pale endapo muhusika wa ushahidi huo yupo nje

ya nchi au kumbukumbu za ushahidi ambazo zilihifadhiwa kwa njia ya kielektroniki zitazingatiwa kama ushahidi wa madai hayo.

Mhe. Spika, aidha, katika kifungu cha 84 (2) ambacho kimetoa maana ya "mdhibiti" Kamati yangu inashauri maana hiyo ibadilishwe na isomeke "maana yake ni mdhibiti wa mamlaka za kuthibitisha aliyeteuliwa na waziri wa teknolojia ya habari na mawasiliano" badala ya ilivyo sasa kama "maana yake ni mdhibiti wa mamlaka za kuthibitisha aliyeteuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar" kwani waziri huyo ndiye atakayekuwa na wajibu wa masuala yote ya teknolojia ya habari na mawasiliano.

Mhe. Spika, katika kifungu cha 136 cha mswada huu katika maneno ya pembeni *(marginal note)* "mashahidi bubu" kamati yangu inashauri katika maneno hayo ya pembeni yaongezewe "au viziwi" ili isomeke "mashahidi bubu au viziwi" na hivyo kufanya maana yake ya ndani kuwa "Shahidi ambaye hana uwezo wa kuzungumza au kusikia anaweza kutoa ushahidi kwa njia nyengine yoyote ambayo itamfanya aeleweke, kama ni kwa maandishi, alama au kwa ishara, lakini maandishi hayo lazima yaandikwe na ishara ifanywe katika Mahkama ya wazi, ushahidi huo uliotolewa utajulikana kama ni ushahidi wa mdomo."

Mhe. Spika, kabla ya kukamilika kwa mswada huu na kuanza kutumika, Kamati yangu inashauri kuongezwa kwa kifungu kipya cha mwisho cha 186 ambacho kitafuta sheria kongwe ya ushahidi sura ya tano na kuanza kutumika sheria mpya ya ushahidi ya mwaka 2016.

Aidha, katika mswada huu kumekosekana kifungu cha 77, na hivyo, kamati yangu inapendekeza mpangilio mpya wa vifungu ufanyike kuanzia 76 na kumalizia kifungu cha mwisho cha 185 ambapo kutakuwa na kifungu cha kufuta mswada wa ushahidi sura ya tano na kuanza kutumika sheria mpya ya ushahidi ya mwaka 2016.

Mhe. Spika, vile vile, Kamati yangu inaomba kwamba sheria hii mpya ya Ushahidi ianze kutumika rasmi mwezi wa Januari 2017 ili kuweka kumbukumbu za miaka mia moja ya matumizi ya sheria hii ambayo asili yake ni nchini India. (*Makofi*).

Mhe. Spika, Kamati yangu ya Katiba, Sheria na Utawala inaishauri Serikali kuitumia vyema Tume ya kurekebisha sheria Zanzibar kwa kuzipitia Sheria zote ambazo tumezirithi na nyenginezo zilizopitwa na wakati ili zifanyiwe

marekebisho badala ya kuachwa na kukaa kwa muda mrefu sana bila ya kufanyiwa mapitio na kuondolewa kasoro zilizomo katika sheria hizo.

Mhe. Spika, pia kamati inapendekeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia wizara ya Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kufanya semina maalum kwa taasisi mbali mbali ambazo zitahusika kwa njia moja ama nyengine katika kutekeleza na kusimamia sheria hii, pia jamii ikiwemo Mahkama, Afisi ya Mwendesha Mashtaka, Afisi ya Mwanasheria Mkuu, Jeshi la Polisi Tanzania na Taasisi za Tiba hasa Hospitali kuu za Umma na jamii kwa ujumla wake.

Aidha, jamii yetu ielimishwe kupitia vyombo vya habari ili iweze kuelewa lengo na dhamira ya sheria hii na jinsi gani itaweza kuwasaidia kujua haki zao za msingi. (*Makofi*).

Mhe. Spika, baada ya kueleza haya machache nawaomba Wajumbe wako wa Baraza lako tukufu kwa hekma na busara, nao waitumie fursa hii ili waweze kutumia, kuelewa na kuuchangia Mswada huu wa marekebisho ya sheria hii ili kuurekebisha na hatimaye kuupitisha kwa ajili ya ufanisi wa wananchi wetu wa Tanzania. (*Makofi*).

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti wa Kamati. Waheshimiwa Wajumbe wachangiaji nilionao mpaka sasa hivi ni wawili tu. Kwa hivyo, naomba nimwite mchangiaji wa mwanzo Mhe. Ali Suleiman Ali na Mhe. Mgeni Hassan Juma ajiandae.

Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata): Mhe. Spika, awali ya yote ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa mbele ya Baraza lako Tukufu nikiwa na afya njema na hali nzuri juu ya kuhakikisha kwamba tunafanya kazi zetu tulotumwa na wananchi wetu kwenye majimbo yetu na nchi yetu kwa jumla.

Mhe. Spika, ninampongeza sana Mhe. Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi pamoja na Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba na Utawala Bora, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, watendaji wote wa wizara, Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa juhudi zake kubwa za kuhakikisha kwamba Mswada huu unakuja, lakini pia sitomsahau Mhe. Jaji Mshibe kwa kazi nzuri aliyotupa Wawakilishi wote kutuelimisha kuweza kujua tunakisema

nini kwa ajili ya usalama wa wananchi wetu juu ya marekebisho haya ya Sheria mbali mbali.

Mhe. Spika, mimi ninaipongeza Serikali kwa kuliona suala hili la kurekebisha sheria ambazo kwa asilimia mia moja zimepitwa na wakati.

Mhe. Spika, sheria hizi tunazozijadili hapa hasa za udhalilishaji watoto, wanawake, wazee yaani jumla kwa jumla tunaweza kusema, hii inafika umri wake miaka mia moja 2017 kwenye mwezi wa Januari. Kwa hivyo, ningeomba sana na tungefanya sherehe maalum siku ya kutia saini Mhe. Rais iwe mwezi wa Januari tarehe ambayo ni kumi na saba ninategemea ndiyo siku halisi inayofikia miaka mia moja, ikawa kama ni historia kwake yeye Dkt. Ali Mohamed Shein kuiona adha hii ambayo imewakabili wananchi wetu katika nchi yetu. (*Makofi*).

Mhe. Spika, mimi katika maisha yangu hakuna hasa tendo linaloniudhi katika nafsi yangu kuliko kudhalilisha au kudhalilishwa mtu. Yaani kudhalilishwa mtu maana yake Mhe. Spika, akiwa mtoto mdogo, akiwa mlemavu, akiwa mtu mzima. Yaani udhalilishaji maana yake ni udhalilishaji. Na mdhalilishaji huwa hachagui wala hana busara, wala hana imani. Huyo sawa sawa ni mtu adui katika maisha ya mtu yule anaomfanyia udhalilishaji huo. Kwa hivyo niseme tu kwamba Mhe. Spika, sheria hii itatupa muangaza mzuri na itawatoa hofu wananchi wetu kwa kutoa taarifa panapohusika.

Mhe. Spika, vijana wetu wengi au watu wengi si vijana tu hata watu wazima. Maana kuna watu umri wa miaka kumi na tano, ishirini na mingapi lakini kuna wengine miaka sitini na sabini nao wanadhalilishwa vile vile. Lakini kubwa ninaweza kusema tu kwamba udhalilishwaji pia hauchagui si mtoto mdogo si mtu wa kati au mtu mzima.

Kwa mfano Mhe. Spika, niipongeze Mahakama yetu ya Mwera au kama nimeisahau wapi juzi ilimtia hatiani kijana mmoja, yaani kambaka mzee wa miaka thamanini. Kafungwa miaka kidogo lakini siingilii Mahakama, miaka tisa lakini ilikuwa haitoshi lakini tena huko siingilii mambo ya Mahakama wanajua wao vigezo vyao. Kwa hivyo tujue tu kwamba hili janga halina kwa mtoto mdogo. Lakini mimi ninasema tu Mhe. Spika, jengine ambalo tumelipata hivi karibuni juzi juzi, ninafikiri jamii yote inasikitika, mimi mmoja na wenzangu waliokuwemo humu. Mtoto wa kambo, yaani mtoto wako mwenyewe au mtoto wa kambo sijui, silielewi vizuri lilivyotokea lakini nimelisikia juu juu moyo unaniuma. Mtoto wa miaka mitatu mzee wake anamuingilia mpaka anamuua. Limetokea juzi.

Sasa jana mimi nilisikia kwenye chombo cha habari katika *Chuchu FM redio*, sana hupenda kusikiliza mchana. Wanasema bora anyongwe, apigwe risasi. Mimi ninaunga mkono kwa kuwa nilikuwa mwanajeshi yule apigwe risasi hadharani hasa asionekane. Maana yake ukimnyonga pia unampa imani lakini risasi ni jambo la mara moja ajute maisha yake.

Kwa hivyo mimi ninaungana na Mhe. Spika, nimefurahi sana Sheria hii kuja kwa wakati huu tuliokuwa nao, ingawa tumechelewa. Lakini niseme awamu yetu hii ya Dkt. Ali Mohamed Shein atapata historia ya maisha yake pamoja na Waziri wake Maalim Haroun Ali Suleiman, Mwanasheria Mkuu, na sisi Baraza la Wawakilishi kwa ujumla tutakuwa tumeweka kitu kizuri kwa manufaa ya jamii yetu inayotutegemea.

Mhe. Spika, tatizo linaloathiri katika kutoa ushahidi. Mara nyingi mtoto mdogo akibakwa au akifanyiwa tendo baya huwa hajifahamu au huwa anaogopa au yule mtu nunda yule, maana ninamwita nunda huyo aliyelisababisha tendo lile, huwa anamwambia nikikusikia nitakupiga kisu nikuue, vitisho.

Leo bahati nzuri Mhe. Spika, utoaji ushahidi utakuwa faragha. Na mtu yeyote mtoto anaweza kutoa ushahidi, maana yake haiwezekani mtoto kabakwa mfano, akishabakwa mfano katika Mahakama anaulizwa aliyekufanyia tendo hilo unamjua. Aah! ninamjua, jina lake nani, hawezi kumtambua, lakini leo akenda akimtolea macho tu mimi aliyenifanya huyu kenda na maji.

Kwa hivyo mimi ninaunga mkono Mswada huu kwamba mtoto asiogope kutoa ushahidi. Halitakiwi jina, inatakiwa sura na ndiyo maana katika kutafuta majambazi kwenye sehemu za uhalifu, wakiwekwa rumande, wanaitwa wale walioshuhudia hebu tuoneshe mtu gani, maana yake hamjui jina, huyu ndiye, wanapitisha pale foleni. Unapita kama Rais anakagua gwaride hivi, wamewekwa mbele yako, unasema huyu hapa, mara ya pili huyu hapa, mara ya tatu huyu hapa, unaletwa mmoja mmoja pale. Kwa hivyo Mhe. Spika, ninasema ushahidi huu utawasaidia sana watoto wetu, na ninatoa wito kwa wazazi tuache tabia ya kulindana. Shihata nimefanya kosa niadhibiwe Shihata, tusitake tena mambo ya baraza la suluhu, hakuna.

Mhe. Spika, hivi vitendo vinatokana sisi wenyewe katika jamii yetu. Mwengine mtoto wa mjomba, mtoto wa shangazi, mwengine Mwenyezi Mungu atunusuru ndio mtoto wako mwenyewe. Kwa hivyo mimi ningeomba sana Mhe. Spika, hili suala la utoaji ushahidi wananchi wetu taaluma hii waipokee na waipongeze Serikali kwa kuwa imekuja wakati unaofaa.

Mhe. Spika, miaka ya nyuma nilipokuwa Mwakilishi huko kwenye Mabaraza yaliyopita Mwanasheria alikuwa ni Marehemu Iddi Pandu Hassan. Tulitunga sheria katika Baraza la Wawakilishi tupo kule pale Kikwajuni. Tukasema kwamba sijui watoto hawa wanaoharibiwa, wanaobakwa, wanaofanywa nini lakini pia mfano kama mtu kakumbana na jambazi na mke wake. Yaani vyovyote vile ilivyokuwa lakini tunasema kadhihirisha, tunaambiwa kwamba ukichukua kigongo ukimpiga cha kichwa akifa yule huna kesi. Kesi yako itakuwa ndogo sana, utahifadhiwa ndani kidogo kwenda huko lakini huna kesi, kwa sababu ni tendo ambalo la uhakika la uso kwa uso. Sheria ile mimi ninafikiri ipo, tena ni sheria nzuri.

Lakini sheria hii ya watoto wadogo, hii iliyowekewa ninafikiria kifungo si zaidi kama miaka thalathini na tisa au arobaini iliwekwa ninakumbuka mimi, yaani zaidi ya miaka thalathini naa. Lakini leo bahati mbaya Mahakama zetu sisemi kama kuna nini siingilii. Unaweza kwenda tendo limefanyika na ushahidi upo, ukazungushwa miezi sita, miaka mitatu, miaka mitano ushahidi hakuna. Naomba vyombo vyetu hivi vya Mahakama. Mimi ninaiomba Polisi, Polisi wanakuwa kazi yao ni ndogo tu kupeleka, lakini tena huko unataka ushahidi gani sijui wa nini. Shihata umekamatwa na meno ya tembo haya hapa, Mwenyezi Mungu aninusuru haitotokea *in shaa Allah* kwa hapa palipobakia.

Sasa meno haya umeshakamatwa nayo wewe. Unakuja kuambiwa kwanza tupate ushahidi panazungukwa nini na kitu kipo mkononi. Kwa hivyo mtoto anapofanyiwa tendo baya, maana yake ameshafanyiwa tusitake mzunguko. Hivyo hili ninasema kwamba sheria hii imeweka wazi itakuwa hakuna mzunguko wa ushahidi mwengine baada ya yule mtenda na mtendewa.

Kwa hivyo niseme tu kwamba naiomba sheria hii Januari mbali kutia saini, lakini ndiyo kuna taratibu zake. Mimi nimetoa hii kama wazo tu. Mhe. Spika, siku ile afanye kama sherehe kama alivyofanya kwenye Mswada wetu wa Sheria ya Mafuta na Gesi. Kwa hivyo siku hiyo waandishi wa habari, jamii yote iitwe, pawe kama itafanywa pale Uwanja wa Amaan pale si vibaya, kwa sababu wananchi wote washuhudie kwamba hili tendo linaudhi katika maisha yetu.

Kwa hivyo niseme wazee wetu, ndugu zetu tuna watoto wetu. Leo Mhe. Spika, kama mtoto anaondoka anakwenda chuoni Madrassa, anaondoka anakwenda skuli anarudi jioni Yarabi Salama akili huna mzazi. Ndiyo maana tukasema tu kwamba tuwe waangalifu kwa pande zote. Mimi niseme kwamba ninarudia tena Mhe. Spika, watoto wadogo wanauma na watoto ndiyo tunaowategemea taifa la kesho. Na haya matendo ya watoto wetu kuharibiwa siyo watoto wa

kike tu, hata wengine wengine wanatoka mafisadi, maadui. Ndugu Hassan anasema tuwaite lugha gani, lakini yetu tunayotumia kwa wale mafisadi, yaani tunasema ni maadui wa watoto wetu na nchi yetu kuwaharibu watoto wetu.

Mhe. Spika, ninaomba sheria hii iende hivi vizuri ifanye kazi zake vizuri na siyo tena lishatokea tatizo unaambiwa aah! mimi maana yake huyo ni mjomba wangu, liondoke hilo. Sheria ifanywe kali zaidi. Maana hapa mtoto akamuadhibu mtoto mdogo aende kama miaka mia jela mpaka kufa kwake huko huko, asitolewe miaka ishirini au miaka kumi na tano. Bado kuna watoto wengine miaka kumi na tano, kumi na sita, kumi na saba, kumi na nane wanaofanya vitendo kama hivyo, akitoka bado anadunda nje. Lakini sheria ninasema iwe kali ya kumuadhibu mtu akajuta maisha yake.

Pia ningeomba ningependekeza baada ya sheria hii kumtia hatiani kama kafungwa miaka hamsini, miaka mia moja lakini na viboko vya kuingilia kama ishirini awe navyo. Viboko ishirini vya kuingia mule jela na miaka mia akitoka si mtu tena lakini japo kumi na tano, ishirini apate vyengine vya kuambiwa kaponee kwako.

Mhe. Spika, hili litatuweka pahala pazuri. Mhe. Spika, ninasema haya kwa sababu wananchi wengi au asilimia mia moja ya Wazanzibari na Watanzania kwa jumla hawana imani na baadhi ya watendaji hawa wa mambo maovu katika watoto wetu. Kwa hivyo niseme mimi linalonipa uchungu zaidi. Mimi wizara yangu au Wizara zangu ninazozifanyia kazi Wizara ya Habari na Utalii, lakini na wizara ninayoifanyia kazi ya Kazi, Ajira, Watoto, Wanawake, Wazee na Vijana, kwa hivyo nimekusanya kila rika, nikawacha walemavu lakini ndiyo tunachukulia jamii moja inatutegemea.

Kwa hivyo niseme tu Mhe. Spika, masuala haya mazuri ambayo Serikali imetuletea, yaani Mswada huu. Mimi niombe tu kwamba Mhe. Spika, tuufanyie kazi upitishwe ili uanze kazi zake haraka, iwe kama tendo ambalo lisitokee tena katika nchi yetu.

Mhe. Spika, jengine nitasema kwa ufupi niipongeze Serikali vile vile au niipongeze Wizara kwa kuliona hili kwamba sasa hivi ushahidi utatoka kwa njia tofauti. Siyo lazima uende pale Mahakamani. Nipo Uingereza au upo Ujerumani unaweza kutoa kwa mtandao wewe mwenyewe ukasema Shihata au fulani kafanya hili, nimeshuhudia ikawa ni ushahidi au hata yule mtoto au mtu mwengine anaweza kutoa ushahidi kwa njia yoyote ya mawasiliano ili kuondoa ile adha. Kwa sababu mtoto ukienda siku nyengine lile adui lililokufanyia tendo baya unaliona pale likikutolea macho unaogopa, utaitwa faragha na utajieleza

kwa njia nzuri. Kwa hivyo Mhe. Spika, naipongeza Serikali kwa kuliona hili na niseme tu kwamba tujiandae kulisherehekea suala hili ambalo litatuletea maamuzi mazuri juu ya hatma ya wananchi wetu.

Mhe. Spika, baada ya hayo ninasema tena naupongeza kwa dhati na kwa moyo wangu wote ndani ya nafsi yangu Mswada huu wa Sheria ulioletwa kwa wakati huu, kwa sababu wakati wenyewe ndiyo tuufanyie kazi juu ya maslahi ya wananchi. Kwa hivyo mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Kijitoupele wote wenye nia njema na nchi hii na watoto wetu na jamii yetu wanaiunga mkono au wanaunga mkono Mswada huu na mimi mwenyewe ninaunga mkono.

Mhe. Spika, ahsante sana. (*Makofi*).

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Ali Suleiman Shihata. Naomba sasa nimwite Mhe. Mgeni Hassan Juma; Naibu Spika, ili na yeye achangie.

Mhe. Mgeni Hassan Juma: Mhe. Spika, nakushukuru na mimi kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuchangia machache katika mswada huu wa Kutunga Sheria ya Ushahidi.

Mhe. Spika, awali ya yote kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema ambaye ametupa uzima na afya na kutupa uwezo wa kutekeleza majukumu yetu tuliyopangiwa.

Mhe. Spika, vile vile niipongeze sana serikali, kwa kuleta mswada huu mbele yetu ili sasa suala zima la ushahidi liwe limefanyiwa marekebisho makubwa, ili iweze kusaidia katika kesi mbali mbali.

Mhe. Spika, niseme tu kwanza nimpongeze sana Mhe. Waziri, pamoja na Mwanasheria Mkuu na timu yake. Lakini vile vile niwapongeze sana Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi, inayohusiana na Katiba, Sheria na Utawala kwa kuweza kudadavua vizuri sana mswada huu, kama kumejitokeza makosa madogo madogo basi wameweza kuyafanyia kazi.

Mhe. Spika, mimi sitokwenda ndani katika mswada huu sana, kwa sababu mswada huu kwa kweli umeniridhisha, na niseme tu kwamba naunga mkono kwa asilimia mia moja.

Mhe. Spika, mswada huu naamini mimi tutaupitisha leo, baada ya kuupitisha naamini sana Mhe. Rais atausaini mswada huu, kwa sababu najua Mhe. Rais

katika suala ambalo lililokuwa linamkera sana ni suala zima la udhalilishaji wa watoto na jinsia. Kwa hivyo, nina hakika Mhe. Rais hivi sasa anausubiri kwa hamu kubwa kuweza kuusaini mswada huu.

Mhe. Spika, lakini kuwepo kwa mswada ni kitu kimoja, na utekelezaji ni kitu kingine, hivi vitu inabidi viende sambamba Mhe. Spika. Nasema hivyo kwa sababu tuna tatizo la kufanya kazi kwa mazoea, hilo ndilo tatizo kubwa ambalo linatukumba, ni kama maradhi au *syndrome* iliyotupata hapa Zanzibar. Madam tumeshazoea njia fulani ya kuendesha mambo yetu, basi inakuwa vigumu sana kubadilika.

Mhe. Spika, mimi nina mapendekezo yangu na ninaomba sana niyalete mbele yako, lakini naomba sana Mhe. Waziri yuko hapa ananisikia, Mhe. Mwanasheria Mkuu ananisikia.

Jambo moja ambalo limezungumzwa vizuri sana na kamati ni elimu inatakiwa itolewe kubwa sana kwa wale ambao wanahusika moja kwa moja, kuhusiana na masuala ya udhalilishaji wa watoto na jinsia, kwa sababu ndani ya taasisi zile ndimo munamojitokeza matatizo mengi na yanapelekea kwamba kesi zile zinarundikana na hazina hukumu, hilo ni tatizo.

Jengine Mhe. Spika, ambalo mimi naliona kwamba ni muhimu, Mhe. Spika, baada tu ya kusainiwa sheria hii, basi ningeomba sana Afisi ya *AG* na Afisi ya *DPP* kesi zote zinazohusiana na suala la udhalilishaji wa watoto, zile ambazo hazijapatiwa hukumu basi zipewe muda maalum wa kuhakikisha kwamba kesi zote zinamalizika. *(Makofi)*

Mhe. Spika, hata kama kesi ilikuwa miaka 10 iliyopita, kesi ile lazima itizamwe upya. Mimi sijui, majalada ya kesi hizi yanachukua muda gani mpaka yanafungwa. Lakini kwa uzoefu wangu niliouona, nimeona kwamba kuna kesi nchi za wenzetu zinaweza kukaa hata miaka 27 hazijapata hukumu, lakini zinakuja kufufuliwa upya na zinapata hukumu.

Mhe. Spika, wasi wasi wangu mkubwa ni kwamba kuna kesi ambazo hazijapata hukumu na wale watuhumiwa wanatembea barabarani, na wanapotembea barabarani tusifikiri wale wamepona gonjwa lao.

Mhe. Spika, mara nyingi mtu anayefanya kitendo kile atarudia tena na tena. Sasa tusiwape nafasi hiyo ya kurudia tena wakaenda kufanya vitendo vile ambavyo sisi na jamii nzima Mhe. Spika, wanalipigia kelele suala la udhalilishaji wa watoto.

Mhe. Spika, suala la udhalilishaji wa watoto limefikia pabaya kwa upande wa Zanzibar, na ubaya zaidi ni kwamba watoto wanaoharibiwa sasa hivi ni wa kiume. Tuangalie sisi wenyewe tutakuja kuwa na jamii gani, lazima suala hili tulipe kipaumbele. Haiwezekani tukasema kwamba sheria tumeshaitunga tunayo, lakini tukaendelea kuwa na yale yale kesi hazihukumiwi, hilo halikubaliki Mhe. Spika. Kwa hivyo, ningeiomba sana serikali, zile kesi zote ambazo hazijapata hukumu na zipo, hata kama zina miaka 30 lakini zirudiwe zitizamwe tena, pamoja na ushahidi huu uweze kutumika.

Jengine Mhe. Spika, ningeomba sana suala zima la aidha, tuwe na Mahakama maalum itakayoshughulika na kesi za udhalilishaji wa watoto na jinsia. Kwa sababu Mhe. Spika, moja katika sababu ambayo wanatoa hao wanaohusika na kesi hizo, wanakuwa na kesi nyingi zaidi, hata zile za kuiba nazi na embe, kesi hizi zote anaweza kupewa mtu mmoja.

Mhe. Spika, tukiwa na watu maalum, lakini tukiwa na Mahakama maalum, au tukiwa na siku maalum, yaani siku moja peke yake katika wiki kwenye kila Mahakama ya kuangalia kesi za udhalilishaji. Mhe. Spika, tiba ya matatizo haya itapatikana. Ningeiomba sana serikali, suala hili la kutenga siku maalum liangaliwe na lipewe uwezekano ili tuweze kuliondosha tatizo la udhalilishaji wa watoto.

Mhe. Spika, sasa hivi ukienda katika vikao mbali mbali. Mimi mara nyingi sana huwa nakutana na kinamama wa chama changu, hata nikienda na ajenda nyengine, akinamama kilio chao ni udhalilishaji, na bado wanaona serikali haijafanya kitu, bado wanaona kwamba hatua hazichukuliwi, kwa sababu wadhalilishaji wako mitaani wanatembea kifua juu na wanasema kwamba hakuna ambaye anaweza kuwakamata, hili liwe basi mwisho. Sheria hii iwalinde watoto wetu. Watoto wamepata fursa ya kujitetea wenyewe, wamepata fursa ya kutoa ushahidi. Lakini haitatosha kama fursa hizi wanazozipata zitavurugwa vurugwa, haitatosha na wala haitakuwa na maana sheria hii leo tunayoipitisha.

Mhe. Spika, eneo la hospitali. Mtoto anakwenda anapimwa na anaonekana mtoto yule mzee wake anasema ameharibiwa. Ukienda kwa wahudumu ambao wamepewa hiyo kazi wanasema kwamba huyu mtoto pengine labda haonekani kitu chochote au mtoto amezoea. Hakuna mtoto anayezoea kudhalilishwa, hata mtu mzima pia.

Kwa hivyo Mhe. Spika, tunaileta sheria lakini lazima utendaji wake ubadilike, hapa tunataka mabadiliko, tukiizungumzia sheria tutazungumzia sheria nzuri

sana, kwa sababu tuna wataalamu wazuri wa kuandika sheria, watu walijifungia siku nyingi wakaandika sheria, lakini tuhakikishe wale wote ambao watakwenda kinyume na sheria hii wachukuliwe hatua, tunamuomba Mhe. Rais.

Tunakuomba sana Mhe. Rais, tunalia sisi wanawake kwa vitendo ambavyo wanafanyiwa watoto, kwa kweli vinatuuma sana. Lazima ifike pahala watu wale ambao kwa kweli wanakwenda kinyume na sheria hizi wachukuliwe hatua za kweli kweli sio zibakie kwenye karatasi.

Jengine Mhe. Spika, ambalo ningeliomba sana nanalisema hili kwa sababu nina ushahidi wa kutosha. Lakini nalisema hili kwa sababu nimefanya upelelezi wa kutosha. Mhe. Spika, naiomba sana serikali suala zima la kupata mashine ya *DNA*.

Mhe. Spika, katika kipindi kilichopita nilileta hoja binafsi, moja katika maazimio tuliyoyaazimia hapa ndani ya Baraza, ilikuwa ni mashine ya *DNA*. Nilijaribu kufanya utafiti ingawa yalitoka majibu sitaki kusema, lakini hicho kitu kilinivuruga kichwa kidogo kwamba haitasaidia sana mashine ya *DNA*, sio kweli. Mhe. Spika, sio kweli. Kwa sababu tulifanya ziara tukaenda Tanzania Bara na tuliwauliza swali hilo. Wakasema mashine ya *DNA* inaweza kutumika kwa kupata vinasaba vya mtu ambaye amemfanyia kitendo mtoto na *scientific evidence* ni muhimu sana katika kutengeneza kesi. Mhe. Spika, ikiwa mpaka leo bado ile mashine hatuna basi bado kutakuwa kuna matatizo.

Mhe. Spika, mimi nimewauliza wanasheria wote wakubwa, wamekiri, nasema tena wamekiri kwamba mashine ile ni muhimu sana kwa ajili ya kuwapa *scientific evidence*, na kuweza kuchukua vinasaba vya mtu ambaye amemuharibu yule mtoto, ili viweze kuleta ushahidi ambao kweli ni ushahidi ambao utaaminiwa. Naiomba sana serikali, hili naliomba sana na nalisisitiza. Naomba sana serikali bajeti inayokuja, basi suala zima la ununuzi wa mashine ya *DNA* lipewe kipaumbele.

Mhe. Spika, mimi nafikiri nimeshasema vya kutosha. Ningeomba sana yale ambayo nimeyasema Mhe. Waziri atakuja kunieleza hapa kwamba tunaweza tukachukua hatua gani, ili haya mambo ambayo nimeyaomba yaweze kufanyiwa kazi. Kwa hivyo, niseme tu kwamba naunga mkono sheria hii, lakini vile vile ningewaomba na wajumbe wenzangu wote tuiunge mkono sheria hii ni muhimu sana kwetu.

Vile vile basi niwatakie kheri wale wote, pamoja na sisi sote, kwa sababu sote inatuhusu kwa njia moja au nyengine, iwe ni sheria ambayo itaweza kuleta matumaini katika jamii zetu. Mhe. Spika, nakushukuru sana.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. Sasa naomba nimwite Mhe. Rashid Makame Shamsi, atafuatiwa na Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto, na Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali ajiandae.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kwa kunipa nafasi hii adhimu ya kuweza kuchangia mswada huu wa sheria ya ushahidi iliyo mbele yetu.

Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kuwa na afya nzuri, na hii leo tokea tunaujadili mswada huu muhimu wa sheria ya ushahidi ambao ulikuwa unasubiriwa kwa siku nyingi.

Mhe. Spika, nimshukuru na nimpongeze sana Mhe. Waziri wa wizara inayohusika maalim wangu maalim Haroun kwa ufasaha wa ufunguzi wa taarifa au hotuba yake inayohusiana na muktadha mzima wa sheria hii.
Vile vile nichukue fursa hii kuipongeza kamati inayohusiana na mswada huu, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala na hususan nimpongeze Mwenyekiti Mhe. Machano Othman Said kwa uwasilishaji wake mzuri na ufasaha. Lakini vile vile kwa marekebisho ambayo wameyapendekeza yahusianayo na mswada huu.

Mhe. Spika, nichukue fursa hii vile vile kuwashukuru wajumbe wawili wenzangu waliotangulia, kwa kuweza kuchangia na kuweza kutoa mapendekezo yao.

Niishukuru vile vile Tume ya Kurekebisha Sheria, chini ya Mwenyekiti wake Mhe. Mshibe, kwa kazi kubwa sana ya ustadi na ya umahiri waliyoifanya hadi kuweza kupata mswada huu, ambao wameuandaa kwa miaka isiyopungua mitano. Tuwashukuru sana.

Mhe. Spika, mswada huu wa sheria ya ushahidi ni mswada mmoja muhimu sana katika mazingira ya visiwa au nchi yetu kwa wakati huu.Niseme tu kwamba mswada huu umechelewa kama walivyotangulia kusema wenzangu. Umechelewa kwa sababu miaka mia ni miaka mingi sana, nina imani sana katika kipindi cha zamani mswada huo uliokuwepo ulikuwa unafanya kazi vizuri, lakini kadiri maendeleo ya sayansi na teknolojia, lakini na maendeleo ya

kijamii na kiuchumi yanapokwenda mbele, basi uhalisia wa utekelezaji wa sheria ya ushahidi unakuwa matatani.

Mhe. Spika, ni ukweli usiopingika kwamba kuchelewa kwa mswada huu kumeweza kuwanyima haki wananchi wengi wa visiwa hivi kutokana na hukumu mbali mbali ambazo zilikuwa zinatolewa ambazo kisingizio chake kilikuwa pengine kutokamilika kwa ushahidi au kutofika kwa mashahidi katika mahakama.

Kwa hivyo, nichukue tu fursa kuwaomba wananchi kwamba Mswada huu wa Sheria ya Ushahidi mimi nadhani kwamba utakuwa ndio 'muarubaini' tosha kwa wakati huu ambao ushahidi na maamuzi ya Mahakama ulikuwa unalalamikiwa sana na wananchi wetu wa visiwa hivi vya Zanzibar.

Mhe. Spika, suala la Sheria ya Ushahidi linatugusa sote tuliopo Barazani lakini na wananchi wote kwa ujumla linawagusa, kwa sababu sote tunaweza tukawa ni watarajiwa wa tuhuma katika maisha yetu mbali mbali. Kwa hivyo, mimi pamoja na kuchangia lakini niunge mkono tu kwamba Mswada huu naukubali asilimia mia kwa mia kwa sababu ya manufaa ambayo yanaweza kulinda haki zetu wananchi sote kwa ujumla katika visiwa hivi.

Mhe. Spika, hapo nyuma kabla ya Mswada huu kuletwa utagundua kwamba makosa yalikuwa ni kidogo, lakini wakati huu makosa yamekuwa mengi. Makosa yalikuwa kidogo kwa sababu jamii yetu ilikuwa na waungwana wengi, hivi sasa waungwana wamepungua. Jamii yetu ilikuwa na waadilifu wengi, hivi sasa waadilifu wamekuwa kidogo. Jamii yetu ilikuwa na watu wanaomuogopa Mungu, hivi sasa watu wanaomuogopa Mungu wamepungua sana. Jamii yetu ilikuwa na watu wenye hofu, lakini hivi sasa hofu kwa binaadamu wengi imepungua. Jamii yetu ilikuwa na watu wanaoona aibu, hivi sasa baadhi ya watu wengi aibu imewatoka na hii inasababisha makosa mbali mbali iwe ya jinai au mengineyo kuongezeka katika nchi yetu na ndio maana kunalazimika sasa kuwa na muarubaini huu wa Sheria inayohusiana na ushahidi ili kuweza kuifanya haki itendeke katika kesi mbali mbali.

Mhe. Spika, hivi sasa kuna mabadiliko mbali mbali wahalifu wamekuwa na mbinu mbali mbali za kiuhalifu, wamekuwa na akili nyingi sana za kuweza kutekeleza maovu pale ambapo wanafanya hivyo, kumekuwa na mbinu za mawasiliano na habari ukilinganisha na hapo nyuma, kwa tafsiri hiyo utakuta kwamba Mswada huu umeweza kutazama mambo mbali mbali kuhusiana na mabadiliko haya ya sayansi na teknolojia, lakini na mbinu mbali mbali na mabadiliko mbali mbali ya kijamii ambayo tunashuhudia.

Mhe. Mgeni, amezungumza suala zima la Sheria au Mswada, Sheria hii tutaipitisha Mwenyezi Mungu akitujaalia, lakini alisema Mheshimiwa Mgeni, namnukuu kwamba; "Kuwepo kwa Sheria ni kitu kimoja, lakini utekelezaji ni suala la pili". Na mimi niungane nae Mheshimiwa Mgeni. Sheria zetu tunazozitunga na mara nyingi hapa ninakuwa nazungumza kwamba tunasifika sana Zanzibar kwa kuweza kupitisha sheria nzuri na wenzetu wa nchi mbali mbali wanakuja wakiiga Sheria na mambo mbali mbali ambayo sisi tumeyaanzisha. Lakini tatizo linakuwa katika utekelezaji wa Sheria hizo, mimi katika hili nichangie tu kwamba ili utekelezaji wa Mswada huu uendane na matarajio ya wananchi wetu na zile kero ambazo zilikuwa zinajitokeza ziweze kuondoka, basi nilikuwa nashauri baadhi ya mambo Serikali iangalie.

Moja ni suala la elimu ambalo wenzetu wana kamati hili walilipendekeza kuhusu elimu kwa wahusika wa mambo ya Sheria, hili ni suala muhimu sana, elimu hii inaweza ikaja ikagawika katika mambo matatu.

Kwanza kuifahamu hii Sheria, hii Sheria ni kubwa ina vipengele vingi kuna ulazima kwamba watendaji wetu wa vyombo vya Sheria kuweza kupata mafunzo ya kina kuona kwamba wanaifahamu sheria hii, lakini kwa sababu ya mustakabali mzima wa masuala ya ushahidi Sheria hii imezungumzia masuala ya Mawasiliano kwa lugha ya alama. Ni vyema watendaji wa vyombo vya sheria basi wawe wanapata mafunzo ya mara kwa mara ili kuona wanakuwa na weledi, wanakuwa na ujuzi na stadi katika kufahamu lugha hii ya alama kwa sababu watuhumiwa au watakaohusika na kesi mbali mbali wengine watalazimika kuzungumza kwa lugha za alama.

Pamoja na kwamba sheria hii inataja wakalimani, lakini ni vyema Mahakimu na Majaji na hata katika ngazi za chini za kipolisi basi kunahitajika lugha ya alama iwe ni sehemu ya watendaji hawa kuifahamu ili kuweza kuona kwamba hata hao mashahidi pamoja na kula kiapo, lakini wasije wakapotosha ukweli pale ambapo hakimu haielewi lugha ya alama. Kwa hivyo, hiyo inapaswa elimu hiyo itolewe kwa watendaji wa vyombo vya sheria.

Lakini vile vile kuna suala zima hili la ushahidi wa ki*electronic*, ushahidi wa ki*electronic* maana yake ni kwamba ni ushahidi unaotokana na vyombo vinavyohusiana na *electronics* ambavyo vipo vingi na vinazuka siku hadi siku, kuna ulazima mkubwa sana kwa elimu hii iwafike watendaji wa vyombo vya sheria ili wawe mahiri, wawe weledi na wawe na ujuzi katika kuona kwamba vyombo hivyo wana uwezo wa kuvitumia ili ushahidi unapotolewa kwa njia hizi isije ikawafanya wao kuwa hawaelewi kwa kina juu ya matumizi ya vyombo hivi. Kwa hivyo, taaluma hii nayo Mhe. Spika, inahusiana na vyombo

hivi vya mawasiliano hususan vya *electronics* basi viweze kutolewa kwa watendaji wetu ili kuona sheria hii inatekelezeka vizuri.

Lakini jengine Mhe. Spika, ni suala zima la elimu kwa jamii ya Wazanzibari, hili wenzetu wana kamati waliligusia na mimi nalisisitiza zaidi kwamba, jamii yetu kuanzia baada ya upitishaji wa sheria hii, basi Wizara inayohusika au Serikali kwa ujumla najua kwamba kuna vipindi mbali mbali vinavyohusiana na sheria lakini suala hili la Sheria ya Ushahidi basi liwe na vipindi maalum katika vyombo vya habari, viandaliwe vipeperushi, semina, mijadala na kongamano na hususan katika vijiji mbali mbali vya Unguja na Pemba ili kuona sasa jamii inau welewa na kuona kwamba vile vile jamii inaridhika na marekebisho au uundaji wa sheria hii ili kuona kwamba, yale matatizo ambayo walikuwa wanakumbana nayo ya kiushahidi basi yanaondoka.

Lakini Mhe. Spika, nije sasa katika suala la uadilifu, katika utekelezaji wa sheria na hususan hii ya ushahidi inategemea sana suala zima la uadilifu na uwajibikaji kwa watendaji wa Mahakama zetu, ukweli kesi nyingi zinacheleweshwa na nyengine zinacheleweshwa kwa makusudi ili kuweza kuondosha ushahidi au kupingana na ushahidi. Vile vile, kuna upotoshaji wa makusudi wa ushahidi, sasa haya yanatokea wakati mwengine kutokana na watendaji wa vyombo hivi vya Mahakama kutokuwa waadilifu, sasa bila ya kuwa na uadilifu maana yake sheria hii japokuwa ni nzuri kama dhahabu basi tusitarajie kwamba yale ambayo tunayataraji kuweza kujitokeza.

Mhe. Spika, uadilifu unaondoka kutokana na suala zima la rushwa hata kama ushahidi mzuri utakuwa umepatikana, lakini suala la rushwa litakapokuwa limetawala katika vyombo vyetu vya Mahakama basi tusitarajie kwamba Sheria hii itakuwa inafanya kazi, itakuwa ni bora ile ile ya kikoloni kuliko hii ambayo tumeiandaa kwa lengo la kuweza kuondosha kasoro. Kwa hivyo, niiombe sana Serikali na tukiombe sana chombo kinachohusiana na suala la rushwa kuweza kuangalia taasisi hizi za Mahakama na Sheria ili kuona suala zima la rushwa linapungua na hatimae kuondoka ili kuona kwamba sheria hii inafanyakazi kama tunavyotarajia.

Mhe. Spika, jambo jengine ni mazingira rafiki ya mashahidi, sheria hii imezungumzia masuala ya mashahidi na ukweli usiopingika ni kwamba mashahidi wengi huwa hawafiki Mahakamani, hawafiki Mahakamani kutokana wakati mwengine na hofu, kutokana na kutojiamini lakini kutokana na vitisho vile vile. Lakini suala jengine la mashahidi kutofika Mahakamani ni suala la kuhisi usumbufu wa nenda rudi pale ambapo kesi zinaahirishwa mara kwa mara na wakati mwengine zinaahirishwa makusudi ili kuweza kuzivuruga kesi

za namna hiyo, ningeiomba sana taasisi inayohusika au Wizara inayohusika na Serikali kwa ujumla kuweza kuandaa mazingira rafiki kwa mashahidi ili mashahidi sasa wawe hawana hofu ya kufika Mahakamani, wawe hawana woga na vile vile, wawe wana uwezo wa kufika Mahakamani.

Kwa sababu suala ambalo wakati mwengine linasababisha hawa mashahidi kutofika ni suala la umasikini, nenda rudi ziko nyingi lakini hawana chochote ambacho wanakipata au kinawasaidia, ningeiomba sana Serikali kuweza kuona sasa mashahidi wanawezeshwa kama nchi nyengine zinavyowezesha mashahidi ili kuweza kuona kwamba shahidi anafika Mahakamni ile siku ambayo amepangiwa. Kwa sababu shahidi akiwa ni masikini leo umemwambia kenda karudi, kesho kenda karudi hatimae anavunjika moyo na uwezo anakuwa hana.Kwa hivyo, vyombo vya Mahakama hivi lazima sasa viwe vinatenga fedha kwa makusudi ili kuweza kuwasidia mashahidi, ili kuweza kuona kwamba wanafika katika vyombo vya sheria na kutoa ushahidi kwa watuhumiwa.

Mhe. Spika, nitoe wito tu sasa kwa jamii kwamba muarubaini huu umepatikana, kwa hivyo, tuwaombe sana jamii kuweza kuona kwamba wanashirikiana na Serikali na wanakuwa tayari katika kutoa ushahidi pale ambapo unatakiwa bila ya hofu na bila ya aibu, ili tuweze kuona sasa kesi zetu nyingi na hususan hizi za udhalilishaji ambazo hivi sasa zimeenea basi ziweze kutekelezeka vizuri.

Mwisho, Mhe. Spika, nije ndani kidogo katika huu waraka wa Mswada, sina marekebisho makubwa lakini ningeomba tu katika kifungu cha tatu sehemu ya kwanza, hapa kuna masuala ya tafsiri ya maneno mbali mbali, tafsiri hizi kiutaratibu ziwe zimekaa *alphabetically*, lakini bahati mbaya pengine wenzetu hawakuliona hili haipendezi hivyo zilivyokaa, kwamba zimeanza na *letter M*, ikaja *K*, ikaja *W*, ikaja *K*, ikaja *N*, ikaja *T*, ikaja *M*, ikaja *T* na ikaja *A*. Mimi nafikiri zingewekwa *in alphabetical order* ili kumrahisishia msomaji kuweza kuona kwamba tafsiri hizi zinasomeka vizuri.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo niendelee tu kusema tu kwamba naiunga mkono asilimia mia kwa mia Sheria hii na nina hakika sana wananchi wangu wa Jimbo la Magomeni nao wataiunga mkono kwa sababu ni mkombozi wa wananchi wote wa Zanzibar. Ahsante sana Mhe. Spika. *(Makofi)*

Mhe. Shadya Mohammed Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kwa kunipatia nafasi hii ya kuweza kuchangia machache katika Mswada huu. Kwanza naomba niendelee kumshukuru Mwenyezi Mungu anayeendelea

kunipa pumzi zake mchana huu na kuwepo hapa katika hali ya uzima na afya njema.

Mhe. Spika, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu, naomba niipongeze Serikali kwa dhati kabisa kwa nafsi yangu na moyo wangu, vile vile, naomba nimpongeze Waziri wa Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa kutuletea Mswada wa Kufuta na Kutunga Upya Sheria ya Ushahidi.

Mhe. Spika, nafsi yangu imefarijika sana kwa kutuletea Mswada huu kama nilivyozungumza wa kutunga upya Sheria ya Ushahidi, nasema haya kwa sababu ipi, mimi kwanza nitajikita sana kwenye kuchangia huu ushahidi wa mtoto, nasema haya Mhe. Spika, ikiwa na mimi sasa hivi nimeingia katika Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana Wanawake na Watoto nikiwa pale kama ni Naibu Waziri.

Mhe. Spika, muda mfupi tu nilioingia pale nimeanza kujionea mwenyewe takwimu kwanza dhidi ya watoto wetu hawa wanaobakwa hususan watoto wa kiume, ikiwa jana tu Mhe. Spika, kwa kuona takwimu lakini jana nimeshuhudia mwenyewe kwa macho yangu Ofisini pale aliletwa mtoto wa kiume chini ya miaka saba, ama nane kama sikosei mtoto huyo nae tayari ameshafanyiwa hicho kitendo.

Kwa hivyo, mimi niseme nimefarijika sana Mhe. Spika, kwa ushahidi huu wa mtoto, kama tunavyotambua Mhe. Spika, watoto wetu wanapofanyiwa vitendo hivi na wakapelekwa Mahakamani, mtoto siku ya kwanza atasema mengine, lakini anaporudia tena anabadilisha kauli, kwa hivyo, ushahidi hapo kidogo unakosekana.Lakini sheria hii sasa hivi inamfanya mtoto yule atakapokwenda kusema ushahidi wake ni ule ule kwa ile mara ya kwanza, kwa hivyo, ni jambo zuri sana na tunasema tunaishukuru sana Serikali na tunaiunga mkono kwa suala hili.

Mhe. Spika, nataka nichukue nafasi hii kuwaomba wazazi wenzangu huko majumbani, Mwenyezi Mungu ametujaalia tumepata sheria yetu nzuri hii na *In shaa Allah* Mwenyezi Mungu atuwezeshe tuweze kuifanyia kazi kwa vitendo, nichukue nafasi hii kuwaomba wale wazazi wenzangu huko majumbani, watoto wetu wanapofanyiwa udhalilishaji huu tusikae wenyewe tukayamaliza nyumbani, tunazidi kulitimua hili janga, lakini endapo tu tutafika kwenye vyombo vya sheria na tukaiwacha sheria ichukue mkondo wake basi nina hakika Mhe. Spika, jambo hili litapungua kwa kiasi kikubwa hapa kwetu na hatimae Mwenyezi Mungu akipenda litamalizika kabisa.

Mhe. Spika, kama nilivyosema mimi nataka nizungumze machache kwa sababu kama sikuiunga mkono na mimi nafsi yangu itanisuta kama nilivyosema na mimi sasa hivi nimeingia katika Wizara hii, ambayo inamgusa sana huyu mtoto anayedhalilika.

Kwa hivyo, nimalizie tu Mhe. Spika, kwa kutoa wito au kwa kuomba. Niombe madaktari wetu pamoja na maaskari hawa wanaoshughulikia masuala haya ya watoto wetu wazidi kutuunga mkono katika Wizara yetu hii ili tuone kwamba suala hili tunalimaliza kabisa katika nchi yetu.

Mhe. Spika, baada ya hayo machache nakushukuru sana na nasema naunga mkono sheria hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa hai kuzungumza machache sana juu ya Mswada huu Sheria ya ushahidi, nimeupitia kwa makini katika vifungu vyake na kwa kweli nimeridhika nayo sana na naikubali.

Lakini sasa Mhe. Spika, hebu na tuiangalie hii dhana nzima ya sheria, nitafsiri kwa haraka haraka inaonekana kama kwamba Sheria hii ndio muarubaini wa matatizo yote ya kisheria, lakini kwa kweli si sahihi kwa sababu wataalam wa falsafa wanasema au wanajiuliza kwa nini binaadamu hafanyi makosa au kwa nini binaadamu anafanya makosa.Tafsiri moja inasema kwamba binaadamu hafanyi makosa sio kwa sababu anaogopa adhabu, au sheria, lakini kwa sababu ya ubinaadamu wake anahisi kitu fulani hakifai yeye kukifanya. Natoa utangulizi huu kwa kusisitiza umuhimu wa kujenga maadili mema kwa jamii yetu ili iwafanye watu waone aibu, kufanya makosa mbali mbali ambayo wanayafanya.

Kwa kuwepo tu sheria itakayomuadhibisha mtu kutokana na makosa haitoshi. Kwa hivyo, nitoe ushauri huu kwamba lazima tufikirie kujenga au kufufua maadili yetu. Tuwafunze vijana wetu mapema kabisa kujenga ubinaadamu ambao utaonea aibu kufanya matendo ambayo yanakwenda kinyume.

Mhe. Spika, sasa hivi inaonekana kama kwamba kuna fahari fulani mtu kufanya kosa. Kwa sababu tumeshindwa kujenga maadili au tumeshindwa kujenga maadili ambayo yatamfanya aepukane na makosa mbali mbali. Kwa hivyo, wakati umefika wa kujenga maadili ambayo yatawafanya binaadamu, yatawafanya wananchi wetu, Watanzania wenzetu, Wazanzibari wenzetu kuogopa kufanya makosa au kukataa kufanya kosa, sio kwa sababu ya sheria, ikiwa kwa sababu ya sheria itakuwa tumekosea. Kwa sababu watu wengi

hawajui kama kuna sheria wala hawaogopi sheria lakini wanaogopa ubinaadamu. Kwa hivyo, tujenge ubinaadamu kwa ajili ya kupunguza haya makosa mbali mbali ambayo yanafanywa na watu wetu.

Mhe. Spika, pia, nilikuwa nikitizama hii sheria kama inakuja bila ya kujali mambo mengine ya kimahakama, bila ya kujali mambo mengine ili itutatulie matatizo yetu, nayo pia sio fikra sahihi. Lazima tutizame sheria hii itahusiana vipi na sheria nyengine zinazoendesha mifumo ya kisheria hapa Zanzibar, hilo ni jambo muhimu sana. Tuihusishe kwa mfano Taasisi ya Mahakama, tuihusishe sheria hii na taasisi nyengine za Ofisi ya *DPP*, na Ofisi za Polisi, Taasisi nyengine za Polisi, lakini pia na jamii, tukifanya hivyo tunaweza tukafanikiwa kwa kiasi fulani.

Mhe. Spika, utaratibu ulikuwepo sasa wa kuendesha taasisi hii hata tukipitisha sheria hii kama hakutakuwa na mabadiliko ya kufanya kazi bado suala la kucheleweshe kesi litaendelea kwa kisingizio kwamba hakuna ushahidi. Sasa jamii ya Tanzania imefika wakati wa kuelewa kwamba kila taasisi inahusika katika masuala ya kisheria ifanye kazi zake kwa ubunifu, kwa ufanisi na kwa weledi, ikiwa taasisi moja tu itashindwa kufanya kazi basi masuala ya ushahidi yanaweza yasiwe na maana kabisa.

Kwa hivyo, nisisitize hapa kama masuala ya ushahidi ni ya *process* kubwa yanahusisha sehemu mbali mbali ya jamii. Kwanza, inahusika jamii yenyewe, yaani watu wenyewe. Je, watu wapo tayari kutoa ushahidi, jibu rahisi kwamba watu wetu hawapo tayari. Lakini tujiulize kwa nini hawapo tayari; wanahofu, hawana ubinaadamu, au lipi, ni lazima tulijue hilo, kwamba inashanga sana kuona tukio linatokea mbele za watu, mchana, kweupe halafu unatafuta shahidi unaambiwa hayupo.

Mhe. Spika, kuna tukio moja jamaa yangu mmoja aligongwa na gari akafariki pale pale, saa 4 asubuhi, lakini mpaka leo hakuna ushahidi wa mtu, wakati ilipotokea ajali watu chungumzima wapo. Sasa tujiulize kwa nini watu wetu wana hofu ya kutoa ushahidi, kwa nini watu wetu hawataki kutoa ushahidi, kwa nini watu wetu hawana muelekeo huo, tukipata jawabu basi litaweza kutusaidia. Lakini tukiendelea katika mfumo huu huu hata tuweke sheria gani itakuwa ni tatizo.

Mhe. Spika, tuje katika wahusika wa pili katika masuala ya ushahidi nao ni polisi, nao pia wanahitaji kujengwa upya, kubadilishwa *mind set* yao, kutumia weledi wao na kufanya kazi kwa kujituma. Ikiwa hawatofanya kazi zao kwa uweledi na kwa kiwango basi bado sheria hii itaendelea vile vile kutoleta

matokeo ambayo wananchi wetu wanayahitajia. Lakini pia Ofisi nyengine zinazohusika ya *DPP* nayo pia wanahitaji kufanya kazi kwa uweledi, lakini ufanyaji kazi wao pia unategemea huku mwanzo, unategemea kwa jamii, unategemea kwa polisi.

Mhe. Spika, mara nyingi tumekuwa tukilaumu namna Ofisi hii inavyofanya kazi lakini pengine katika hali halisi wao wanafanya kazi kwa uweledi, wakitizama faili na majalada wanayaona hayana uzito wowote, kwa hivyo, na wao pia hawaoni kama kuna haja. Nafikiri ni muhimu sana Ofisi hii nayo kufanya kazi kwa ufanisi wake, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu nayo pia kufanya kazi kwa ufanisi na uweledi na Mahakama yenyewe. Kwa hivyo, utakuja hapa duwara zima la jamii likiwa katika hali ya ufanisi suala hili litawezekana. Tuitizame sheria hii katika ujumla wake inaonekana kama mnaitizama katika ushahidi wa unyanyasaji wa watoto. Hii ni sheria imekuja katika suala zima kwa ushahidi wa makosa yote ya kijinai, tuitizame katika nukta hiyo.

Mhe. Spika, tumesema kwamba ni muhimu wananchi wetu na wananchi wetu, jamii yetu kupatiwa elimu ya sheria, mimi naona tofauti kabisa, natofautiana na wengi juu ya mkabala tunaoutumia kutolea elimu hizi za jamii, tunatumia vyombo vya habari, magazeti, lakini tunatumia kwa maoni yangu njia za kimapokeo ambayo athari yake ni ndogo, utakuta mambo mengi yanatolewa katika vyombo vya habari siku hadi siku lakini bado watu hawajabadilika, kwa nini? Huenda kama njia tunayotumia za kuelimisha watu si sahihi. Kwa hivyo, ni lazima tufikirie upya *what is the best approach* ya kuelimisha watu masuala haya ya elimu ya jamii tunayo, *it is public education*, ni lazima tuzifikirie upya, lakini kwa kukaa Mwanasheria katika televisheni, kuandika makala, kufahamisha jambo fulani, nahisi sio sahihi sana katika zama hizi. Tufikirie njia sahihi ya kuelimisha watu, vyenginevyo, tutaendelea kuona kila siku baada ya kupungua makosa yanaongezeka siku hadi siku.

Mhe. Spika, kwa hivyo, tufikirie upya, na ningesisitiza suala labda tunaweza kufanikisha hasa wakati wa utekelezaji wake. Kuna kitu wataalamu wanakiita '*Case Flow Management'*, hili ni jambo muhimu sana. Ushahidi utakusanywa wa kutosha. Lakini kama hakuna utaratibu mzuri wa kuendesha kesi bado kilio cha wananchi kitaendelea kuwepo. Lazima kila kitu kisimamiwe na moja katika *factor* muhimu sana katika kusimamia kitu chochote ni kujali wakati. Lazima tuwe na wakati mahsusi wa kusikiliza kesi, sio kwamba kesi isikilizwe maisha, sio utaratibu mzuri. Ndio nikasema kwamba suala hili la Sheria ya Ushahidi liangaliwe kutokana na vipengele vyengine vya mfumo mzima wa uendeshaji wa shughuli za Mahakama. Kwa hivyo, ni jambo muhimu sana na

nadhani kukiwa na *management* nzuri hili suala ambalo linalolalamikiwa sana la kesi kuchelewa pamoja na mambo mengine nafikiri litaondoka.

Mhe. Spika, nimalizie kwa kusema kwamba naiyunga mkono sheria hii na naomba pia na Wawakilishi wenzangu wengine waiunge mkono. Lakini pia tuwe na matumaini baada ya jamii nzima kuelimisha na jamii nzima ikaweza kuishi katika maisha ya kuheshimu sheria nadhani tunapokwenda tutafika. Ahsante sana.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Spika, nashukuru sana na mimi kupata fursa ya kuchangia Mswada wetu huu uliokuja kwa nia njema na Mwenyezi Mungu aweke mkono wake katika hali ya kuufanikisha katika nia ambayo tumeikusudia.

Mhe. Spika, mimi nataka niseme kabla sijaendelea mbali naunga mkono asilimia kwa mia hii sheria ambayo imepitishwa kwa nia njema. Sheria hizi ambazo tunazitunga siku zote, tokea hapo zamani zipo sheria ambazo zinakidhi haja kwa haja, lakini tatizo letu linakuja kwenye utekelezaji.Mheshimiwa bado Wazanzibari tunakwenda kwa udugu, bado Zanzibari sheria haijachukua mkondo wake na bado tunafanya kazi kwa mazowea, kwa kujuana na kama itakuwa ndio hivi basi hata kama tutatunga sheria za kiasi gani bado zitakuwa hazikidhi haja. Lakini kwa sababu tunasema ni mabadiliko basi twende nayo kwa wakati hali halisi ilivyo na mimi najua kwamba mabadiliko yamejiongezea kwa hali mbaya sana kwenye visiwe vyetu hivi mambo haya yanatokea matukio ya kila aina, naweza kusema suala hili la udhalilishaji wa kijinsia naweza kusema umekamata hatamu.

Mhe. Spika, jumla ya sheria ambazo tunazikazia kamba au kuzikazia hukumu moja hii ya jinsia. Mimi mwenyewe huwa ni mdau wa kupiga kelele sana. Hili ni suala ambalo kwa ukweli kila mtu linamgusa, maana tunavyozungumza kila siku mtoto wa mwenzio ndio mtoto wako na ukisema kwamba wewe halitokufika si kweli na likikufika ndio itakuwa ule usemi unaosema; "mkuki kwa nguruwe kwa binaadamu mchungu". Mtu hufanya mazingira yake anayoyajua mwenyewe akapata mtoto wake katika maumbile ambayo Mwenyezi Mungu amemjaalia, hatakiwi aharibikiwe kwa njia moja au nyengine. Lakini mtoto yule anapofikia katika tatizo dogo tu ambalo mtu sijui kwa uwendawazimu wake au kwa tatizo lake ambalo linaweza likamuharibia mtoto maisha yake na bado yule bwana akaendelea na maisha yake mazuri na hata akikaa huko jela anaona yeye ni bora arudishwe maana kuna msosi mzuri.
Mhe. Spika, mimi kabla sijaingia huko ndani kwa kuchangia basi kwanza nitoe tahadhari. Tatizo tulilonalo tunaambiwa kila siku katika jumla ya kujikinga,

katika jumla ya ulinzi unaanza nao mwenyewe. Suala hili tumelibadilisha ulinzi tumeuachia serikali, wewe mtoto wako hakuhusu, mtoto wako unamuacha kila hali. Serikali zilizopita ambazo ndizo hizi hizi za muhula tu za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kila Rais aliyekuja alikuja na haja ya kukinga watoto na wanawake kwa njia moja ama nyengine.

Rais wa Awamu wa Kwanza Shekhe Karume hapa katika umri wangu mdogo mtoto wa miaka asiyofika 18 alikuwa haruhusiwi kutembea zaidi ya saa 2 za usiku na waliokuwa wakifanya kazi hiyo kwa enzi hizo tulikuwa tunawaita Valantia tu na wala walikuwa polisi hahusiki. Lakini sasa hivi unamkuta mtoto mdogo wa miaka 10 au 12 wa kike unamkuta saa 5 usiku anarudi *tuition* katika vichochoro, yatakayomfika anakumbana na watu tofauti halafu useme mtoto yule kabakwa wakati ambako wewe mwenyewe umeanza na tatizo lile katika hali kama hii.

Mhe. Spika, sheria nyengine zinahitaji kurudishwa kwa kuonekana kama wazee wameshindikana kuzizuia watoto wao, basi serikali ichukue mkondo wake. Watoto wanaozidi miaka 18 unamkuta kwenye *disco* na jinsi walivyovaa na unajua maumbile ya binaadamu hayapo, unamfanya mtu ambaye hata haelemewi na masuala yale unamtia ushawishi wa kuwa akufanyie masuala yale baadae akikukamata unasema amekubaka. Ningeomba sana serikali ikasaidia wazee na suala hili likachukua mkondo wake kupunguza mambo haya, maana najua kwamba serikali katika jumla ya matatizo yake yote haya ambayo yanafanya ili serikali ipunguze matatizo ya ubakaji, lakini inaonekana wazee wamegonga ukuta. Mhe. Spika, ingawa watoto wa siku hizi hawasikii pamoja na sheria zetu ambazo nyengine zinamlinda mtoto ukimpiga unafungwa, ukimkataza haisemezeki. Kwa hivyo, kabla sijaingia huku nilikuwa naelezea matatizo ambayo ili tuweze kujizuia sheria hii ya miaka 18 izuiwe kwa Zanzibar na mtoto akikamatwa basi na mzee wake atapata hatia, hilo lilikuwa tatizo.

Lakini jengine Mheshimiwa, alipokuja Mzee Aboud Jumbe alisema kwamba mtoto wa kike atakapotiwa mimba basi na yeye atafungwa miaka miwili na mtoto wa kiume atafungwa miaka mitatu, ilisaidia kidogo mzee kidogo kuhangaika na matatizo, lakini ukiizuia kamba moja unamfanya mmoja umemfunga mmoja unamwambia apige, Mheshimiwa, hali hii itaendelea na tutakuwa hatujui linalotupiga.

Mhe. Spika, baada ya dibaji ndogo hiyo lakini pia naongeza tena kabla sijafika mbali, matatizo ya nyumbani yamekuwa makubwa sana. Wazee wa nyumbani wanachangia tatizo, sisi mwanzo ilikuwa mtu huthubutu kumwita mtoto

mchumba wake, ilikuwa hairuhusiwi, ilikuwa inajulikana kwamba mchumba ni mtu wa nje, wa baba, wa mama, wa bibi, wa nje, leo ndio unamwambia mwanao mchumba wako huyu na akifika siku za Sikukuu unamwambia mkatie nguo mchumba wako huyu, unaanza kumpalilia mapenzi kabla hajawa yule mtoto na masuala ya mapenzi, wazee wameyafikisha hayo na majumbani ndiyo yaliyokuwepo hayo. Sasa haya mambo mengine Mheshimiwa tutakuwa na kazi kubwa sana, hasa Mhe. Castico na Mhe. Shadya, ambao wanashughulika katika mambo haya na wana kazi ngumu sana, maana na wazee wanachangia.

Mhe. Spika, nataka niende tena kwenye matatizo ya watoto wanaokamatwa na hizi shughuli. Mtoto ukimkamata na tatizo hili unamshtua sana, kwa sababu ukienda kuelezea lile tatizo, vikosi vyetu vya polisi na watu wengine wanalichukulia *force* kama kitu kikubwa sana wakati pale wanataka ushahidi, baada ya kumchukua mtoto katika mazingira mazuri, ama akapewa askari wa kike ambaye mtulivu akamuhoji kwa kila kitu, anaingia askari pale uso wake unatisha, sasa anakuwa hajulikani kama anakuwa pamoja na yule jamaa au ndio yupo kwenye kazi yake.

Mimi ningeshauri hizi kesi wahudumu wake wakawa ni watu wazuri hasa wanawake, mama waliokuwa kidogo wametimia katika kukaa nao wale watoto kuwahoji. Kumbukumbu zile kama tulivyosema basi zirikodiwe zile za mwanzo ambazo yule mtoto atakuwa anazisema ili wakati ambapo atakuwa anatakiwa ushahidi hata akiitwa katika mazingira mengine ule ushahidi wa mwanzo atakuwa amekwisha kuusema. Lakini watoto wanatishwa na mtoto ukimwita kwenye suala la askari mtoto unamtisha sana. Ningeshauri sana katika jumla ya vipengele vyetu basi tukawa na upendeleo juu ya yule mtoto kuwekwa katika mazingira hayo.

Mhe. Spika, nirudie katika mazingira mengine, kesi zetu za Mahakamani. Mahakama haina uwezo wa kushughulikia masuala makubwa sana ya utoaji wa fedha za mashahidi na ufatiliaji. Bado tunaipitisha sheria Mungu akitujaalia, lakini hali kadhalika utoaji wa mashahidi kama hawakufatiliwa na Serikali ikaweka mkono wake kama shahidi kaona kweli na akakataa basi bado sheria nyengine tuongeze ili mtu huyu naye achukuliwe hatua kama ni machanganyio wa kuchangia masuala kama haya.

Mhe. Spika, lakini mimi nataka niseme jengine kwamba katika sheria ambazo zipo ambazo wengine hasa wanawake, Mheshimiwa, najua suala letu tulililoliweka kwamba wanawake wanaweza, wanawake sijui ukiwawezesha, sasa hivi hawataki tena wanasema wanaweza. Mheshimiwa, nao wanasababisha

kupata ubakaji ambao wa kulazimisha.Mheshimiwa, wanakwenda katika maeneo wanajiamini hawataki tena kupelekwa wala kuelekezwa jambo.

Unamkuta mwanamke saa 7.00 za usiku anakwenda peke yake wala huwezi kuona kwamba askari asimchukue mwanamke yule, anakaa pale kufanya nini. Likitokea la kutokea Serikali asubuhi inaambiwa hawa watu wamebaka wakati mwenyewe anataka. Masuala haya ni lazima unapotizama mbele utizame na nyuma, Serikali isitizame mtazamo mmoja wa kutizama baada ya kufanyiwa. Lakini lengo kubwa ni kuzuia matukio, mwanamke yeyote atakaekutikana kuanzia saa 6 za usiku askari amchukue akalale kituoni kama ana mumewe atakwenda kumchukua huko huko, kama ana mtu mwengine atakwenda kumchukua huko huko, lakini asimuache. Baadae akileta matatizo ndio yanakuja. Sasa siku nyengine tu amegombana na mumewe anatoka, akifika njiani huko anapata matatizo, kwanza ni moja la kuwa Mheshimiwa, yule mwanamke hatotoka ndani tutazuia ndoa, mwanamke asitoke usiku, *otherwise*, atoke na mume wake. Mheshimiwa, hilo nilikuwa nalizungumza kidogo liwe la uhakika katika mazungumzo yetu.

Mhe. Spika, jengine ni kumong'onyoka kwa maadili. Sisi wanaume hasa tabia zetu tunaojifanya mashekhe vilemba. Mashehe vilemba wanajaribu kupingana na nguvu za Mungu katika maumbile, anajifanya msafi lakini usiku anabadilika au katika mazingira mengine. Sasa anajizuia katika mazingira ambayo mwisho anakuwa chizi baadae anafanya matukio yaliyokuwa sio ya kawaida.

Mhe. Spika, wazee wetu wa zamani mtoto wake akifika miaka 18 au 20 atahiari amlishe, amvike kwa ushirikiano lazima aowe. Mheshimiwa, hizi sheria tutazitunga, tutachinjana na tutafungana kama hatujapata mustakbali wetu sisi wenyewe wa kuzuiana katika mazingira haya basi bado suala hili Mheshimiwa, litakuwa tata na tutavutana tu kwa sababu lazima kijana akishafika miaka 18 kuendelea mbele maumbile yake yanabadilika na hasa ulimwengu wa sasa hivi, akitizama *WhatsApp* zinamvutia, akitizama *TV* ndio hazisemeki na *TV* nzuri ni ile inayoonesha wanawake na nguo zao fupi wakicheza au michezo mengine ambayo na tunajua Mheshimiwa, tushapita katika sehemu za baleghe tunajua matatizo yetu vijana wanakuwa wanacharukwa vibaya.

Sasa mimi ningemuomba Waziri wa Sheria ambaye tunaye katika kumkabili na suala letu hili katika jumla ya sheria zetu tutakazozifanya atunge na Kanuni za wanawake na watoto usiku atakaenekana awekwe ndani ili tupunguze hili jopo. Kwa sababu kwa kuwaachia watoto wakenda *disco*. Maana yake kuna *disco* moja hapa jeshini wanalita *Entebbe*. Mheshimiwa pale *under fifteen* ndio wanaoingia mule, wewe na mimi hatutakiwi, si kike si kiume na ukirudi

pikipiki moja ina watu sita, mke mume, mke mume, ndio zinaongozana. Mheshimiwa tunakwenda wapi, hali imekuwa ngumu kweli kweli.

Kwa sababu huu ni mporomoko wa maadili na hiyo *Entebbe* imepanda chati kwa namna hiyo, mimi nataka hili Baraza la Wawakilishi siku moja wengine waliokuwa mashekhe waliokwenda Makka wasende, sisi tuliokuwa tunakwenda mwakani twende tukatizame kabla hatujenga Makka. Tukachungulie tu Mheshimiwa, uone ulimwengu wa Zanzibar ulivyoharibika unataka kuwazuia vipi watu wale.(*Makofi*)

Sasa mimi Mheshimiwa ningejaribu kwa sababu mimi huu Mswada nilivyousoma asilimia karibu 70 mpaka 80 udhalilishaji ndio mgumu, ndio unaotufikisha hapa, sijaja kwenye mambo ya jinsia ninakuja hii yetu sisi ya kike na ya kiume. Mhe. Spika, dakika sio zipo kidogo, maana yake nina mambo yangu usije ukatikatiza kati.

Mhe. Spika: Bado mbili.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Aka! Mheshimiwa, ninakushtua ndio unanambia hivi! Nipe tano, Mheshimiwa.

Mhe. Spika: Haya.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Sasa kama nilivyosema kwamba ninamwambia Mhe. Waziri, unajua bora 'kuziba ufa kuliko kujenga ukuta'. Hatuna nia ya kufungana, sheria hii haikutungwa kwa sababu tuje tuchinjane, tuje tukamatane na tuje tufanye kitu gani hapana. Lakini hali imeshakuwa mbaya hatuna budi kuipitisha tukaona uwajibikaji wake utakuwa hivi. Lakini kama kuna njia za kuweza kuzuia kuliko kufika kupelekana kwenye sheria Mheshimiwa, hilo ningekushauri kwa sababu wewe ni mtu wa Katiba na Sheria ukapita misikitini ukalazimisha watu kama vile kwenye muhajirina kwamba watu waoe wapunguze vijana ili tupunguze na hili jukumu.

Mhe. Spika, jengine nataka niseme kwamba katika masuala ambayo ya viongozi wetu hasa hawa Mawaziri, mitandao yetu inafanya kazi kwa kuambiwa watu, hivi sasa nasikia watu wote wanapiga kelele hapo maisara, nasikia kuna nyumba, kuna mambo, kuna balaa gani, watu wanaoana, Mhe. Waziri, uko wapi, kalitizame hilo tatizo lipo. Watu wote mpaka mimi jana wamenitumia *massage* ndugu zangu wananambia watoe watoto chuoni, sijui tusiwapeleke pahali gani, nyumba hivi sasa za mambo haya zimekithiri na

zinajulikana. Sasa wewe unasema Mheshimiwa, unataka kumtafuta mtu, mtu huyu hapa nyumba zinajulikana watu wanaoana.

Mhe. Spika, sasa mimi nataka niseme kwamba nawaomba mawaziri wetu sasa hivi mitandao inasema mambo mengi na mimi nataka niseme tunatiliana maanani na moja tu, sasa hivi kuna mitandao tele inasema kuna maji yameingizwa madude gani. Waziri aende akatizame ni la kweli au si la kweli, halafu aseme, watu wanakuwa na hofu, kila jambo lina hofu na sasa tunategwa. Lakini Mheshimiwa, ninalotaka kulitoa indhari kwa Mhe.Waziri na wanasheria wetu, hii sheria ni mtego. Sheria hii inaweza ikazungumza mtu ambaye ana hatia au hana hatia.

Kwa sababu nchi yetu hatuwezi kusema kwamba haijajengeka kisiasa wala haijajengeka kichuki. Matokeo yetu tunaweza tukafanya jambo hili kwa nia njema, lakini kumbe sio madhumuni yake. Ningewatahadharisha majaji, nikawatahadharisha na viongozi wengine kuitumia sheria hii vilivyo ili kuona haki inatendeka, si kwamba tumeifanya sheria hii ili ije iwe kikwazo au iwe ni pahali pa kutiana adabu.

Mhe. Spika, nimeshaona mambo mengi na katika mambo mengi mtu anahukumiwa kuuliwa au kufungwa kama kaua aliyeua sie au aliyefanya kosa lile sie na nina uhakika hukumu za vitu hivi havitokuwa hukumu ndogo. Kwa hivyo, ningewaasa majaji wetu wakawa makini katika hili, wakaa na Mungu pamoja katika kuhakikisha kwamba anakula kiapo kwa Mungu kwamba anafanya uadilifu, asije mtu akapita katika masuala ya itikadi zetu, ama za kukomoana kisiasa na mambo mengine. Nia yetu ni kuhakikisha watoto wetu Mungu awajaalie tuondokane na tatizo hili.

Mhe. Spika, kabla sijamaliza la mwisho mimi nilikuwa nazungumza tu kwamba, kwa kweli tulikuwa tukipiga makelele sana Mheshimiwa, na mimi nataka tuangalie kitu kimoja kabla ya mtu huyu anaefanya madhambi kwa watoto wadogo, kwanza akapimwe akili, inawezekana si akili yake hasa matatizo yetu ya ulevi wa madawa yetu na mambo mengine. Mwenyezi Mungu aninusuru kwanza, sifikiri mtoto wa miaka 3 au 4, Mheshimiwa, itanipata hamu gani kwenda na mtoto kama huyo, mambo yaliyojaa Mwenyezi Mungu barka alizozitia.(*Makofi*)

Mheshimiwa, Naunga mkono hoja asilimia mia kwa mia. .(*Makofi*)

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Spika, na mimi ninashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia mswada huu. Mimi kabla ya yote napenda kuchukua nafasi hii

kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema aliyetujaalia leo hapa tukasimama katika Baraza letu hili ikiwa ni siku ya kwanza ya mkutano wetu huu wa Baraza, tunamuomba Mwenyezi Mungu mwenyewe atupe uwezo mkubwa wa kujadili mambo yetu kwa maslahi ya taifa letu.

Baada ya hayo Mhe. Spika, mimi nachukua fursa hii kumpongeza sana Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora na timu yake nzima iliyokaa kwa muda mrefu kujadili mswada huu na hatimaye kuuleta Barazani ili uweze kupata baraka za hapa. Ni matumaini yangu mimi kwamba wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi tutaunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja. Kwa sababu mswada huu kama walivyotangulia kuzungumza wenzangu wengi ni ukombozi wetu sisi na vijana wetu na vizazi vitakavyokuja, kama tunavyoangalia sheria tuliyonayo ikifika mwezi wa Januari mwakani inatimiza miaka mia, baba yangu mimi aliyenizaa hajafikisha.

Sasa ni jambo la kufurahia kwamba baada ya miaka 100 tunapata sheria nyengine mpya ya ushahidi. Mhe. Waziri, hongera sana na timu yako na mimi nachukua fursa hii kukupongeza tena. Lakini mimi katika mchango wangu ingawa wenzangu wengi hasa Mhe. Rashid, kanifilisi mambo yangu mengi lakini ni uelewa mzuri na watu wanaonekana wana hamu ya kuchangia yale ambayo ni mazuri. Lakini mimi naungana na wenzangu kwamba lengo la mswada huu ni kuweka mazingira bora ya kiushahidi ili kujenga umadhubuti katika kesi. Kwa sababu bila ya ushahidi hakuna matokeo bora ya kesi, ili kesi Mheshimiwa, iwe kesi na yapatikane matokeo bora ya kesi inahitaji ushahidi ulio mzuri.

Mhe. Spika, pamoja na mambo mazuri ambayo tunayategemea tuwe tunayo lakini bado mimi nasema kwamba tuna *challenges* nyingi ambazo zinatukabili kwenye vyombo ambavyo ni vya kusimamia mambo haya. Tunahitaji kuwa na watumishi walio na uadilifu wa hali ya juu. Kwa sababu imani ya mwananchi ni kwamba anapofanyiwa kosa nje anakimbilia kwenye Mahakama, ili aende akapate haki yake Mahakamani. Ingawa jana wakati wa uwasilishaji kwenye semina mkufunzi wetu alitwambia mtu anaekimbilia Mahakamani kila wakati huwa akili yake saa nyengine inakuwa sio sawa. Lakini Mahakama ndio baba, tukimbilie wapi, wananchi imani yao ni kukimbilia Mahakamani ili kuona anapata ile haki ambayo ameikosa au anaweza kuikosa.

Lakini Mheshimiwa, bila ya kufichana kuna jambo moja ni kilio cha wananchi ambalo na mimi naomba Baraza hili na Wizara inayohusika kwamba kuna baadhi ya mambo sasa lazima wayatizame upya. *Challenges* nyingi tulizonazo

ni kwenye hivi vyombo vyetu kama Polisi, Ofisi ya Mwendesha Mashtaka *DPP* na Mahakama yenyewe. Hivi vitu vilikuwa ni vyema vikawa na muingiliano wa karibu katika ufanisi wa mambo yao. Lakini inaonekana kwamba hakuna uwiano wa karibu wa mambo haya kati ya vyombo hivi vitatu.

Mfano jana mimi wakati nachangia lakini sikusubiri tena kwa sababu nilikuwa niko kwenye muda wa kusali nikatoka kwenda kusali, sikujua kama nilijiwa au sikujibiwa na mkufunzi aliyekuwa akituongoza, lilikuwa ni suala zima la upelelezi kwanza. Mhe. Spika, suala la upelelezi kwanza, Mhe. Spika, hili suala ni tatizo, suala hili linasababisha mrundikano mkubwa wa kesi. Mahakamani utakuta kuna upungufu wa kesi lakini ukenda Polisi kuna milima ya ma*files*, kesi hazendi Mahakamani, shauri ya upelelezi kwanza, upelelezi kwanza mtuhumiwa anakamatwa, anasubiriwa *DDP* mwendesha mashtaka atoe idhini, yaani akamilishe upelelezi ipatikane idhini ndio kesi iende Mahkamani. Mtuhumia kakamatwa na ikidhibiti *red-handed* ni moja katika ushahidi ambao jana pia tumeelezwa kama mtu kakamatwa na ikidhibiti ni ushahidi. Lakini *DPP* mpaka yeye ajiridhishe kwamba kweli hili ni kosa ndio kesi iende Mahkamani. Jambo hili Mheshimiwa, limekuwa ni kikwazo kikubwa.

Athari zake ni nini, suala la upelelezi kwanza ambalo mimi nimeliona ni kwamba suala la upelelezi kwanza linachukua muda zaidi ya miezi 2 kulisubiri jalada kutoka kwa *DPP* kupelekwa Mahkamani, wakati huo mtuhumiwa kawekwa nje kwa dhamana. Unatoa nafasi kwa mtuhumiwa kuweza kukimbia kwa sababu miezi miwili mpaka mitatu yuko nje. Pia, kunatoa nafasi ya kutengeneza mianya ya rushwa. Kwa sababu mtuhumiwa anapokuwa nje anajua anajipanga vipi ili kukabiliana na kesi inayomkabili.

Lakini kwa nini Mheshimiwa, pamoja na sheria yetu hii nzuri ya ushahidi ambayo tunaileta tusitumie mfumo wetu wa kuwa mtu akikamatwa anawekwa kutuoni, anachukuliwa anapelekwa Mahkamani, akifika Mahkamani kama ushahidi hakuna kesi itaondolewa, inatusaidia sisi, inaisaidia Polisi na wananchi wanajenga imani. Lakini leo mhalifu kafanya kosa kwa mujibu wa sheria masaa 24 akimaliza anatakiwa apewe dhamana kesho unamkuta mtaani anadunda, anaendelea na uhalifu wake na anajipanga jinsi ya kutafuta njia ya kuweza kumaliza kesi.

Mhe.Spika, jambo hili mimi naomba na ninapendekeza lichunguzwe na litizamwe upya, ikiwa kuna utaratibu wa kuwa lazima iwepo Sheria ya upelelezi kwanza yaainishwe makosa maalum kwamba kosa hili lazima lipelelezwe ndio liwekwe Mahkamani, sio kwamba kila kesi kwanza lazima iende kwa *DPP* ipelelezwe kwanza ikisha ndio ipelekwe Mahkamani.

Mhe. Spika, mimi naona suala hili la upelelezi kwanza pamoja na dhana nzima ya sheria tunayoitaka kuipeleka ambayo mimi nina imani kwamba tutaipitisha kwa asilimia 100 inaweza ikaondoa ule utamu wa hii sheria ambayo tunaipitisha leo hii au kesho Mwenyezi Mungu akipenda. Naomba Mwenyezi Mungu atujaalie kwa roho safi, wawakilishi tutaipitisha ili itumike kuwa sheria. Mhe. Spika, *challenge* ya pili ambayo ipo kwenye upelelezi kwanza ni kwamba, Polisi wameshamaliza, yaani wamethibitisha kama hii ni kesi lakini pia na yeye *DPP* kaamua kama hii ni kesi, lazima *DPP* aende akaisimamie mwenyewe, DPP aende mwenye Mahkmani akasimamie kesi zake, ikisha ndio kesi hiyo iweze kuendelea. Mhe. Spika, mimi naona huu ni urasimu, napendekeza kwamba suala hili mimi naomba liangaliwe upya.

Jengine kuhusu mswada wetu wa sheria ambao tunataka kuupitisha. Kwenye sheria hii tunayotegemea kuipitisha ni kuwa kuna ushahidi ambao mtoto akiutoa hautohitaji ushahidi wa mtu mwengine. Mhe. Spika, ni jambo zuri kwa sababu tumeona watoto wengi wanadhalilishwa na nakubaliana na hilo, lakini pia nilikuwa napendekeza ushahidi wa mtoto uwekwe muda maalum kwa mtoto ambaye ushahidi wake hautohitaji kuwa na ushahidi wa mtu mwengine, ili tusije tukafanya kitu kikaja kikatudhuru baadae.

Mhe. Spika, kwa sababu ikiwa mtoto anawezwa kuulizwa masuala akajibu ni vizuri ukapatikana ushahidi wa mtu mwengine, isipokuwa yule mtoto ambaye hata ukimwambia jambo alilokuwa halijui, mimi napendekeza ushahidi wake uwe wake peke yake usihitaji ushahidi wa mtu mwengine. Kwa sababu tukiyaachia haya yanaweza yakatokea mtu akampanga mtu kutokana na mambo yetu tuliyonayo ya leo akamwambia wewe nenda kaseme kadha, kadha, kadha. Ikiwa ushahidi ni wa mtoto, mtoto akitoa ushahidi hauhitaji ushahidi wa mtu mwengine, ni hatari. Hivyo, tunaweza tukaja tukaingia kwenye matatizo. Kwa hiyo, ni vyema tukaweka umri maalum wa mtoto ambaye ushahidi wake hautohitaji ushahidi wa mtu mwengine.

Mhe. Spika, kuhusiana na ushahidi wa kielektoroniki mimi nafikiria ni kweli nakubaliana nao kwamba dunia sasa yote ni dunia inayokwenda na wakati. Sasa hivi ulimwengu wote uliopo ni ulimwengu wa *digital*, na ushahidi wa kielektoroniki mimi nasema ni mzuri zaidi, kwa sababu ushahidi huu ingawa sasa hivi watu wanaweza ku-*copy* na ku-*paste* baadhi ya mambo lakini bado yatakuwa yana vyanzo vyake vya kuweza kuthibitisha. Kwa hiyo, mimi kwa upande wa ushahidi wa kielektroniki nakubaliana nao na naunga kwa asilimia mia kwamba ni njia ambayo wenzetu duniani wameanza kuitumia kwa muda mrefu sasa. Na sisi Zanzibar kwa sababu ni miongoni mwa watu mwa dunia hii ni lazima twende sambamba na wenzetu duniani.

Mhe. Spika, mimi kwa upande wangu nilikuwa sipendi nichangie mambo mengi isipokuwa haya ambayo nimeyaona kwamba ni tatizo. Lakini Mheshimiwa la mwisho kabla ya kumaliza nilikuwa nataka kuzungumza kuhusu suala zima la ubakaji na unyanyasaji.

Mhe. Spika, suala la ubakaji na unyanyasaji wa kijinsia sambamba na madawa ya kulevya katika nchi hii limekuwa ni tatizo. Kwa hiyo, sheria hii imekuja wakati muafaka lakini sheria hii itakuwa haitafanya kazi ikiwa kama walivyosema wenzangu watumishi wa vyombo ambavyo vimepewa mamlaka ya kusimamia sheria hawatokuwa waadilifu kwa kufanya kazi kwa uadilifu. Mfano, leo Mhe. Waziri Maudline Cyrus Castico, kila anaposimama na anaposema anazungumzia suala la unyanyasaji wa wanawake na watoto, lakini utakapokwenda Mahakamani ukafanya uchunguzi ni kesi ngapi zimeripotiwa na ngapi zimetolewa hukumu. Utakuta pengine ni asilimia 10 au 15. Kwa hiyo, tutoe wito tuviombe vyombo vinavyosimamia haki kwenye kesi za udhalilishaji wa watoto na wanawake pamoja na madawa ya kulevya kwamba zipewe kipaumbele tofauti na kesi nyengine ingawa zote zina umuhimu wake, lakini hizi ni athari kwa taifa letu na zinaweza zikatia doa taifa letu.

Mhe. Spika: Una dakika moja tu Mheshimiwa.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Spika, baada ya hayo natamka kwa dhati ya nafsi yangu kwamba naunga mkono mswada huu kwa asilimia 100, na nawaomba wajumbe wenzangu tuunge mkono kwa asilimia 100 ili tuweze kuupitisha uwe sheria na uweze kutumika kwa maslahi ya taifa letu. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini: Nakushukuru Mhe. Spika, kwa kupata wasaa huu wa kuchangia hoja hii ya serikali ya Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mhe. Spika, awali ya yote baada ya waheshimiwa wengi kuchangia mengi kabisa ya msingi ambayo kwa kweli tulikuwa tunahitaji kuwaambia wenzetu kwenye muhimili huu wa sheria nafikiri wengi wamegusia na mimi sitaki nirejee. Kwa kweli nashauri sana Mhe. Waziri, ayazingatie sana haya masuala hasa yanayohusu ushahidi, kwa nini watu wa Zanzibar wengi hawapendi kutoa ushahidi, nini tatizo? Kwa hiyo, tuwafatilie tufanye utafiti wa kina tujue hasa ushahidi upo lakini watu wanaogopa au hawataki kwenda kutoa ushahidi, kwa nini? Kwa hiyo, tufatilie tujue, kesi nyingi sana huwa hazikamiliki au zinachelewa kukamilishwa ushahidi haupo na watu hawataki kwenda kutoa

ushahidi. Kwa hiyo, mimi ningemuomba sana Mhe. Waziri, alifatilie hili suala kwa kina kabisa tujue kwa nini.

Mhe. Spika, nipo hapo hapo kwenye ushahidi, kwenye ukurasa wa 69 katika ule ufafanuzi. Inasema;

"Ushahidi namaanisha njia ambayo jambo linalodaiwa kutokea, ukweli ambao ukiwa kama utawasilishwa kwa upelelezi".

Mhe. Spika, *experience* imeonesha mara nyingi sana kuwa ushahidi hauwasilishwi kwa upelelezi, ushahidi upo unapelekwa lakini kwa njia moja au nyengine unapotoshwa. Kuna ushahidi tosha Mheshimiwa madawa ya kulevya yamekamatwa, yamehifadhiwa baada ya muda siku ya kesi mifuko ya madawa ya kulevya inakwenda kufunguliwa inakutwa saruji. Sasa Mhe. Spika, mimi nashauri sana tumejaribu kuangalia sana humu hao wanao*temper* na ushahidi kama ni askari, ama wafanyakazi wa Mahakama au Majaji wenyewe Waheshimiwa hilo bahati mbaya sana kama itatokezea.

Lakini nataka kushauri kiweko kifungo maalum cha wao na wao kuadhibiwa, kwa sababu ushahidi upo umepelekwa na stakabadhi zipo, dawa ya kulevya inakwenda kukutikana saruji, aaah, hata kama kuna *metabolic process* yoyote iliyotokezea haiwezi dawa ya kulevya ikageuka ikawa saruji. Sasa hili Mhe. Spika, namuomba sana Mhe. Waziri, hawa wanao*temper* na ushahidi kama huo kuupotosha nao tungeweka kifungu humu cha kuwaadhibu, hiyo itasaidia sana. Mhe. Spika, jengine kwenye ukurasa wa 68 kazungumza Mhe. Waziri, kwenye mswada wake ame-*define* hili suala la Mahakama linajumuisha Majaji, Mahakimu na watu wote isipokuwa watatuzi wa migogoro. Mimi nilikuwa naomba nimuongezee tu nataka kushauri aongezee. Mimi nimepepeleza kama Mahakama zetu ukianza za mwanzo mpaka Mahakama Kuu ni chumba maalum kilichojengwa na pale unapandishwa kizimbani, unawekwa pale ni mahala maalum. Sasa labda katika hii *definition* ningeongezea tu kwamba ni chumba maalum, maana yake ukisema inajumuisha Majaji, Mahakimu na watu wote aah, suala la chumba nacho au ile *chamber* naona kidogo haiku-*qualified* humu. Kwa hiyo, bora na hii angeitia kuonesha hasa.

Lakini kwa kuongezea zaidi nataka kuuliza tu ili kwa kufahamu tu Mhe. Waziri, Majaji mara nyingi sana wana vazi maalum na ni heshima yao wenyewe kwa kisheria wavae joho, baada ya joho na kofia zile. Sasa zile kofia siku hizi naona hazivaliwi ndio utamaduni tumeubadilisha au vipi maana yake ile ndio *status* yao wenyewe tumefata Uingereza na *Alhamdulilah* Majaji wetu wengi baada ya Uingereza wamesoma Chuo Kikuu hapa lakini utaona wengine

nasikia kwenye Mahakama Kuu, ama Mahakama ya Rufaa ndio wanavaa, kwa nini wanapovaa ile unajua kweli Jaji yule pale na joho lake na kofia yake anazungumza kijaji kabisa. Sasa nataka kufahamu tu kwa nini imeondoshwa ile kofia siku hizi?

Mhe. Spika, jambo la tatu niliona *somewhere* humu ndani akitajwa Ofisa wa Polisi kimenipotea kifungu gani. Ningeshauri sana huyu Ofisa wa Polisi awe *qualified*, tukizungumza Ofisa wa Polisi tunamzungumza kuanzia ngazi gani. Haya Mhe. Spika, niseme kwamba kwa bahati mbaya sana tunapokwenda unajua sisi wawakilishi wa wananchi mara nyingi sana anakwita mwananchi wako wa jimbo kuna kesi hii, kuna tatizo hili, tunakwenda kwenye vituo vyetu. Tunapokwenda kwenye vituo mle wale askari wanapochukua maelezo ya mwanzo pale mapozi, Mhe. Spika, utasikitika wakati mwengine. Utasikitika kabisa yanakuwa yale maelezo mwenyewe anavyoandika pale, yaani utavunjika moyo pale pale, utaona duh! Hii kesi ndio itakwenda hii. Maana yake unaona hasa kwamba hivyo anavyoandika, Mwenyezi Mungu akujaalie Mhe. Spika, usiende kushuhudia pale.

Mhe. Spika, ninachotaka kusema namuomba sana Mheshimiwa, wale wanaochukua maelezo ningeomba sana Mhe. Waziri, wawe angalau *qualified* wanaweza kuandika vizuri. Kwa kweli baadae anakusomea, basi utamrudisha mara tatu, hivi sivyo nilivyosema, hivi sivyo nilivyokusudia. Kwa hiyo, kidogo hao maofisa wa Polisi kama ninavyosema wawe *qualified* humu lakini nao wawe *competent* wanajua nini wanachofanya, wengi wao sifikirii kama wanapata *review* ya sheria ya masomo haya, na hilo ningemshauri sana Mhe. Waziri pamoja wakishirikiana na Jeshi la Polisi wapate mafunzo ya mara kwa mara wajue hizi sheria hasa. Najua wengine ndio wanakwenda wanapata *promotion* lakini kwenye huku kwa kawaida huku nako tuna matatizo sana.

Mhe. Spika, naomba nimalizie tunaposema suala la utawala bora na hili tunamshukuru sana Mhe. Rais wa Zanzibar Dkt. Ali Mohammed Shein, huwa analisemea sana. *The rule of law* ni kitu kimoja wapo kinaipa nchi heshima, nchi yoyote kama kuna utawala wa sheria ndio hapo tunasema demokrasi ipo, ndio nchi inaheshimika, nchi inaendelea. Sasa hili Mhe. Spika, namuomba sana hili serikali hata Mhe. Makamu wa Pili, yupo, kwa kweli *the rule of law* lazima nchi yetu tuisimamie ipasavyo. Mambo ya kujuana juana hii na msalie Mtume, huyu shemeji yangu, huyu nani, haiyendi, lazima tuzingatie, hapo ndio ninaposema kweli kuna utawala bora, uwazi upo, uwajibikaji katika Polisi na Majaji nao ipo.

Kwa bahati mbaya sana baadhi ya Majaji wetu hawawajibiki ipasavyo, lakini chombo gani kinachosimamia wawajibike ipasavyo? Hili lazima nalo tuliangalie Mahakimu naambiwa nao hivyo hivyo, chombo gani kinawasimamia. Kweli ni muhimili lakini kweli ndio muhimili, lakini waachie tu wafanye watakavyo. Kwa kweli jamii inafika mahala wanachukua sheria mikononi mwao, unasema aah, unapeleka huko, huko hakuna maana huko, ndiyo yale aliyozungumza Mheshimiwa, mmoja kwamba unamuona kesho mtu anatamba mitaani anakucheka, wewe utanishtaki mimi, mimi mtoto wa mjini bwana, utaniweza wapi wewe, anakutambia mbele ya uso.

Mhe. Spika, umenipa muda mdogo lakini kwa kweli hayo machache ndio nilikuwa nataka kuzungumzia na kwa kweli naunga mkono kwa asilimia mia moja. Nakushukuru sana, ahsante sana.(*Makofi*)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, tuna wachangiaji watatu watakaokuwa wamebaki kwa *session* ya jioni na ni mawaziri, kwa hiyo, tutakaporudi ataanza kuchangia Mhe. Maudline Cyrus Castico, atafuatiwa na Mhe. Said Soud Said na baadae atakuja kumalizia Mhe. Salama Aboud Talib, ingawa nafasi bado ipo kama kuna mtu au Mhe. Waziri mwengine ambaye atataka kuingia kwenye orodha wakati huu ataleta jina kwenye kiti hapa halafu tutaweza kumzingatia na yeye.

Baada ya maelezo hayo, naomba nitoe tangazo nimeombwa niwatangazie Kamati Tendaji ya UWAWAZA inaombwa ikutane katika ofisi ya Naibu Spika mara baada ya kuahirishwa kwa shughuli hii.

Waheshimiwa Wajumbe, kwa muda uliobaki haumtoshelezi mtu mwengine kuchangia ni kama dakika tano tu, kwa hiyo, naomba nitumie nafasi hiyo kusitisha shughuli za Baraza mpaka saa 11:00 jioni.

(Saa 6:50 mchana Baraza liliahirishwa mpaka saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Naibu Spika, kwa heshima kabisa naomba na mimi nichukue nafasi hii kuungana na wenzangu ambao kwa nia moja na kwa makusudi baada ya kuangalia kwamba, sheria tunayoitaka kuizungumza sasa hivi ni sheria ambayo imechukua karne nzima, imechukua miaka mia moja. Ukiangalia chanzo cha

sheria hii ni sheria iliyotoka India. Sasa tunaona kwamba muda wote ambao tumeishi katika nchi yetu tumekuwa tukitumia ule utaratibu wa watu wa India ambao waliona unafaa.

Kwa hiyo, napenda nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi ya kuona na mimi nitakuwa mmoja wapo katika kushiriki kutoa sheria hii ya India ya miaka mia moja na hatimaye kupata sheria mpya ambayo kwa sasa hivi itakuwa inaweza kuzungumza mambo mazuri yanayohusiana na masuala ya ushahidi wa mtoto.

Mhe. Naibu Spika, ukiangalia katika kipindi cha uongozi nimegundua kitu kimoja katika sheria nyingi za Zanzibar. Sheria nyingi za Zanzibar ni nzuri sana ukifananisha na sheria nyingi katika nchi nyengine duniani na hasa kwa kuwa Zanzibar inakubaliana na masuala ya kimataifa. *Classifications* nyingi sana za sheria zinazotungwa kimataifa kwa kupitia *ILO- Convention* mbali mbali kwa Zanzibar zimerekebishwa na kwa Tanzania pia zimerekebishwa, kwa hiyo, zinatumika kwa vizuri sana. Lakini tatizo linalojitokeza ni kwamba katika masuala ya utekelezaji ndio kwenye tatizo, sheria kama sheria nyingi ni nzuri na karibu zote zina utaratibu wa kutaka kumtetea mtoto ipasavyo. Lakini sasa katika haki na ulinzi wa mtoto tatizo kubwa ni masuala pale yanapofika mahali pa kuona kwamba kuna kulindana.

Mhe. Naibu Spika, mtu unajua amekosa kabisa lakini kwa kuwa ni rafiki, au ni ndugu, au mtu wa karibu unamlinda. Kuna kitu kinaitwa 'muhali', muhali unatugharimu kupita kiasi kwa ndugu, familia na kwa marafiki. Kuoneana aibu kwa watu ambao wanaheshimiwa katika jamii, yaani mtu mwenye heshima katika jamii akifanya kosa watu wengine wanaona ni aibu kutaka kumchukulia hatua, kwa hiyo, wanaona bora waliache au wamezee lile suala. Kwa hiyo, mkosa anabaki ni mwenye haki na aliyekosewa anakuwa ni mtu ambaye ananyooshewa vidole vya kudhihakiwa na kuoneshwa kwamba unaona sasa suala limekwenda lakini mimi nimetoka na sina tatizo.

Mhe. Naibu Spika, kitu kikubwa ambacho kitaweza kutusaidia ikiwa tutaweza kurekebisha hii sheria tukaanza nayo kama tunavyosema, mwaka kesho itatimiza miaka mia moja kamili ni pale tu ambapo vyombo vyetu vitakuwa na uadilifu na watakaoshughulikia sheria hii wawe ni watu wanaweza kuogopa, wana hofu ya Mwenyezi Mungu, pasipokuwa na hofu ya Mwenyezi Mungu na kujitambua kwamba binadamu kuna siku moja utakwenda kujibu hoja kwa mwenye amri kubwa zaidi, utafanya mambo yako utahisi kuwa maisha ni kitu cha kawaida tu.

Pia, ile tabia ya watu kuogopa Mahakama, japokuwa jana tulikuwa tunafundishwa na Mhe. Mwanasheria, Jaji Mkuu amesema kwa kawaida wale watu ambao wana vitabia vya kwenda Mahakamani mara kumi kumi, kila jambo dogo anakwenda Mahakamani kidogo wana matatizo ya akili, kutafuta kesi za wenzao, maneno yasiokuwa na maana, kutafuta hoja za kumjengea mtu mazingira yasiokuwa salama, wanakuwa wanaonekana kwamba hawa wana matatizo. Lakini kwa mtu ambaye ni shahidi anayekwenda kumsaidia mtu mwengine nadhani hakuna sababu ya kuogopa Mahakama, sana sana unakwenda kutenda haki yako ya kuweza kuhakikisha kwamba mtu unayekwenda kumtetea unamtetea ili na yeye aweze kupata haki yake.

Mhe. Naibu Spika, hawa waharibifu ambao wanaonesha kama kuna maradhi fulani yameingia, haiwezekani wewe kila siku tunasikia mtu kabakwa, mtoto kadhalilishwa, sijui kafanywa nini. Kichwani kuna nini na huyu mtu hana mawazo mengine mema hata moja ni kuwaza hilo tu, akili yake yote iko kwenye jambo hilo tu, hawazi maendeleo, jambo jema na chochote kile na hasa pale inapokujia kutia aibu zaidi unapokuta mtu wa karibu, wa ndani ya nyumba unaetegemea kwamba atamlea, utapata haki kwake, atakutetea huyo ndiye anayekuwa mtu wa kwanza kukuharibu na pale anakutisha kwamba labda nitakuuwa, ukisema sijui nitakufanyia nini.

Kesi ya mwisho ambayo imenishangaza hivi juzi amepatikana binti mmoja ambaye anasema amebakwa na baba yake wa kambo, lakini huyu baba alichokuwa anafanya kila siku anamngoja mkewe hayupo anamchukua mtoto anamfunga kitambaa cha uso. Kabla hajamfunga kitambaa cha uso anachukua udi anafukiza, anasema maneno, anasema; "ukisema utakufa, utapandwa mapepo", mtoto anaingia hofu. Kwa hivyo, imekuwa huyu mtoto amefanywa zaidi ya mara tatu, hasemi kwa mzazi wake. Lakini Mwenyezi Mungu tu jambo likifika muda na wakati wake huyu mama ametoka kwenye shughuli amekuja akamfuma *live.* Kapelekwa Mahakamani kama kawaida kesi iko Mahakamani na inaendelea.

Sasa mambo kama haya tusipobadilisha *attitudes* zetu wenyewe kitu muhimu kwanza ni kubadilisha *attitudes* ya wananchi, tufike pahala tujitambue kwamba hili jambo sio la kawaida, ule mji Sodoma na Gomora uliunguzwa kwa sababu ya tendo hili na sisi tunakosa baraka nyingi Zanzibar kwa sababu tunaendekeza jambo hili, sio kama ni mageni vitabu vyote vitakatifu vinasema maneno haya. Kwa hiyo, tufike pahala tutambuane na turekebishane tujitambue.

Mhe. Naibu Spika, jambo hili limekuwa ni wimbi kubwa sasa hivi lazima kuwe na operesheni maalumu. Operesheni maalumu kama maafa yanayotokezea

wakati wa masika kukazuka maafa, wengine watakosa mahali pa kukaa tunahangaika tunachangia nguvu kwa pamoja lakini linakuja suala la kipindupindu pia. Kipindupindu kinapotokezea kila mmoja anahangaika, sasa hivi tumeingiliwa na kipindupindu cha masuala ya ubakaji na udhalilishaji limekuwa ni jambo kubwa na ni janga la kitaifa, tukiyasema yote hapa inatisha na ni aibu, maana yake tukisema sana watu wa nje watatutambua na watasema alaa! kumbe Zanzibar ndio imefikia mahali hapo, kitu ambacho hakipendezi.

Hata hivyo, ile hali tuliyokuwa tunaringia ya kusema Zanzibar kuweza kushinda malaria, kweli sasa hivi malaria kila mmoja anatushangaa, watu wametoka Philippines, wametoka wapi kuja kujifunza mmefanya miujiza gani hii malaria imetoka Zanzibar. Kumbe tunaweza tukiamua kufanya kitu.

Mhe. Naibu Spika, lakini kuna ongezeko pia, tukisema katika masuala ya kutoa *data* za watu wa UKIMWI tunasema Zanzibar tuko kwenye *point* 2 au ngapi, kesho na keshokutwa tukija kuanza kupima kwa sababu hawa wabakaji madhali wanabaka ovyo watakuwa ni waambukizaji wa UKIMWI pia, watoto wetu wangapi watakuwa wameathirika; mama zetu wangapi watakuwa wameathirika, wazee wangapi watakuwa wameathirika.

Je, gharama ya maendeleo ya kuendeleza hii nchi yetu itakuwepo kama sio kuanza kushughulikia wagonjwa, kama sio kuanza kushughulikia watu ambao wanakuwa na athari mbali mbali, hata masuala ya *cancer* yatakuwepo. Kwa sababu masuala ya *cancer* yanaambukizana pamoja na matendo mengine ya ngono yanaanzia huko, wewe kila mtu anashika kama tochi usiku na mchana anaranda tu akitafuta watoto kuwaharibu, imekuwa tochi au imekuwa kitu gani. Mhe. Naibu Spika, mimi kama mwanamke katika jamii kuna suala jengine ambalo linaumiza sana ni watoto walemavu hawakupenda, hawakutaka haya. Vijana, wazee ni juzi tu tunakuta mambo. Leo nimesoma kwenye gazeti mama wa miaka 80 anaingiliwa na mtoto wa miaka 28, huyu si kutaka laana tu za kijitu kizima za kuzeeka kabla ya wakati wake kimemshinda kipi.

Pia, napenda niseme kwamba nipongeze vyombo vya sheria, Mwanasheria Mkuu na vyombo vyake vyote, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala; Kamati ya Baraza, hatimaye Mhe. Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein, ambaye amekuwa akifanya jitihada kubwa sana za kuhakikisha kwamba suala hili lifike pahala tupumzike.

Mhe. Waziri, amejaribu kuleta hili suala, anasema suala hili kumbe halikufanyiwa leo na jana, Mhe. Jaji Mshibe alikuwa anazungumza jana

anasema amelifanyia *research* ya miaka mitano, sasa likifika pahala hatujalifanyia kazi itakuwa halina maana.

Kwa hiyo, mimi kwa ujumla nipende kusema kwamba, tukinge kuliko kungoja kutibu na tufike pahala hii sheria hata ikiletwa kama hatutabadilika, hatutakuwa waadilifu na vyombo vinavyohusika havijafanyiwa kazi ya ziada ili tuweze kuelimisha jamii unapokwenda kuzungumza na huyu polisi au unapoanza kwenda kupeleka hizi hatua zitakuwaje, itakuwa tunafanya kazi ya bure. Kwa sababu roho ya rushwa iko pale pale, roho ya muhali iko pale pale, roho ya uongo iko pale pale na mambo mengine mengi yako pale pale. Lakini tukishikamana tukafanya jambo tukisema basi latosha, naamini kabisa tutafika pahala tutabadilika, lakini tujikumbuke sasa hili neno la 'ole kwetu'. Sasa sisi kama ni wazazi katika kipindi hiki wajukuu zetu watalelewa wapi?

Mwanzo kabisa kwenye sheria hii inapoaanza inasema; mwanamke na mwanamme ndio wana ndoa, lakini ukianza kusema au mwanamke au mwanangu nakaribisha vitu ambavyo vitakuja kuingia hapo tuje tuanze kuwa na ndoa moja, wanaanza kuelimisha watu, watataka kudai haki kwamba wana haki ya kufanya vitu vya namna hiyo. Je, tutakwenda wapi? Tutakimbilia wapi? Najua yanatuuma kwa kuwa kuna wengine ndugu zetu hasa wa karibu wanafanya mambo haya, lakini hatuna jinsi ya kuwafanya kwa sababu hatujafika pahali pa kusema huyu mtu akikamatwa ahukumiwe au anyongwe hadharani, au afanywe nini, ni mambo ambayo tumo katika kuhangaika.

Kwa hiyo, napenda niungane na wale wote watakaoipitisha hii sheria na wananchi walioko huko nje tutaendelea kuelimisha na kuelimisha, lakini pia nitoe wito wale wote ambao wamefanyiwa masuala ya ubakaji wasiache kupeleka taarifa, wasiseme sheria hazifanyi kazi. Taarifa inaweza kuwa ndio chanzo cha kuweza kutafuta mikakati mipya ya kuweza kuhakikisha tunafanya nini na wanapokwenda katika vyombo vya sheria waangalie wanazungumza na polisi wamtambue kwa jina, wakienda hospitali wamtambue kwa jina, wakienda wanakochukua talaka wachukue *copy*, sio wafike tu wakae. Kwa hiyo, haki zipo tuendelee kuelimisha wenzetu na wananchi wahakikishe kwamba jambo hili wanalifuatilia vizuri.

Mhe. Naibu Spika, nipende kusema tu nawapa pole sana wale wote ambao wameharibiwa na kesi ziko Mahakamani, ziko mahali gani na kesi zao zinazungushwa tu, nawapa pole sana kwa kuwa najua ni jinsi gani wanaumia. Lakini tujue tu kwamba sasa hivi kuna kama kimtandao, hiki kimtandao ambacho huenda kikawa kinafadhili hata watu wa nje tusipotafuta namna ya kudhibiti hatutaweza kutoka hapa. Sheria ni nzuri kama nilivyosema mwanzo

sheria za Zanzibar ni nzuri sana, kila unayoitizama imekaa kwenye mstari wake na hakika inaonesha kabisa kwamba tukizifuatilia hizi sheria zinaweza kufanya kazi.

Pia, nitoe wito kwa wazazi tupunguze wakati wa kuacha watoto kutembea ovyo na kitu kingine simu. Mtoto wa miaka mitano au anakwenda *primary* anapewa simu ya nini, *WhatsAppp* tena pesa nyingi anafundishwa mambo chungunzima mule. Kuna kijukuu changu kidogo cha mwaka mmoja anafungua *WhatsApp*, anajua mahali pa kubonyeza. Sasa kama akionekana unaona kitu cha kawaida anaona ni kazi ya kawaida.

Hapa tulikuwa tunazungumza masuala ya ubakaji wa wanyama na binadamu yamekithiri mpaka, sasa tunaanza kuzungumza ya wanyama, hebu tumalizane na hili la binadamu tuwe *serious* kuhakikisha kwamba kila mmoja anakuwa mlinzi wa mwenzake na tufanye mikakati ya kuhakikisha kwamba jamii huko chini ndio ishiriki, isiachiwe kwamba ni kazi ya mtu mmoja hatutavuka. Sheria peke yake haitatosha kama sisi hatutachangia katika mambo haya na wale wanaohisi kwamba wamefanyiwa hivi wasiendelee kuona kwamba aa, mimi nishafanyiwa basi nishakuwa mtu wa ovyo, hapana, wewe ulitendewa kwa sababu hukutaka.

Kwa hiyo, nataka kuthibitisha kwamba wizara yangu ina kitengo cha *Cancelling* cha kukushauri ili urudi huko mahali, usiendelee kwenda kupotea na kutumbukia kwenye shimo la milele huko, ukadhani kwamba kwa kuwa ushafanyiwa basi ushakuwa sio mtu wa maana, bado wewe tunakuhitaji katika familia, hizo tabia zinaweza kuachwa na ukaanza kuwa ni kiumbe kipya; haijalishi umefika kiwango gani, haijalishi umeharibiwa kiasi gani, haijalishi wewe umeteswa au umenyanyaswa mara ngani, bado nafasi ya kurudi kuwa ni mtu mzuri katika jamii ipo. Tunakupenda, tunakujali na tunakuhitaji, unaweza kubadilika, kama mlevi anaweza kuambiwa akabadilika kwa nini huyu aliyefanyiwa mambo ya unyanyasaji na akaitwa majina anayoitwa mpaka akafikishwa kwenye eneo la baradhuli asiweze kubadilika, anaweza kubadilika. Tuwatie moyo watoto wetu tusiwafukuze na tutafute ni watu gani wanaowaharibu ili nao hawa wanahitaji *cancelling*, sio kitu cha kawaida, ni kuchanganyikiwa huku.

Mhe. Naibu Spika, kwa hivyo, napenda niunge mkono sheria hii iliyoletwa kwa asilimia mia moja na ninamtakia afya njema Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein, apate afya yake na aitie saini hii sheria kwa sherehe kama alivyoitia ya mafuta na hii pia aifanyie sherehe, kwa sababu imekuwa kadhia, ili na sisi tupate heshima na tuendelee vizuri.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo machache, nakushukuru sana.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako na mimi naomba nichukue nafasi hii, kwanza nianze kumpongeza sana Mhe. Waziri, kwa ajili ya kuleta Mswada wa sheria hii mpya ya ushahidi. Sheria hii kwa kweli naiunga mkono sana kwa sababu katika sheria hii ushahidi pia unaweza kutolewa kwa njia ya siri. Sasa tumekuwa mashuhuda kwamba muda mwingi sisi wanawake lakini na wananchi wengi kwa ujumla tunashindwa kwenda Mahakamani na kusimama kutoa ushahidi, lakini sheria hii imeweza kutufanya sasa hivi tuweze kutoa ushahidi wetu na sheria hii kwa kweli itatupa nguvu na itawapa wananchi sana nguvu ya kutoa ule woga. Mara nyingi watu wanaogopa, wanakuwa wanashindwa kabisa kusema ukweli na kwa sababu ya ule usumbufu mwingi ambao unatokea na vitisho ambavyo vinatokea, lakini kwa namna ya sheria hii ilivyo na ilivyoandikwa basi tunashukuru sana kwa wizara husika na Mhe. Waziri, kuleta sheria hii na hatimaye leo tunaweza kuijadili hapa.

Mimi naamini kwamba sheria hii itatoa mashirikiano ya kutosha baina yetu, lakini pia wanawake wengi watapata fursa ya kuweza kusema ukweli na kutoa ule uhalisia wa mambo ulivyo. Kwa sababu sasa hivi unapokwenda kumsimamisha mtu pale *public* anashindwa kabisa kusema uhalisia na hasa ukiangalia kama alivyosema mwenzangu Wazanzibari tunajuana, muhali umekuwa mwingi wakati mwengine unaona kabisa kitendo hiki kibaya lakini aliyefanya ni mtoto wa mjomba, mtoto wa shangazi, kwa hiyo, unashindwa kusimama ukamsimamia kutoa ule ushahidi ipasavyo.

Kwa hiyo, mimi naomba niunge mkono sana sheria hii na ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, ninawaomba na wenzangu pia waunge mkono mswada huu ili iwe sheria kamili na iweze kutumika kwa faida yetu sote Wazanzibari na Watanzania kwa ujumla. Ahsante sana.

Mhe. Waziri Asiye na Wizara Maalum (Said Soud Said): Mhe. Naibu Spika, ahsante, kwanza napenda kutoa shukurani nyingi kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mweyekiti wa Baraza la Mapinduzi pamoja na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa jitihada zao za kusimamia vyema harakati za maendeleo ya Wazanzibari.

Vile vile, nachukua nafasi hii kuwapongeza Wawakilishi wote Unguja na Pemba kutokana na jitihada zao nao za kusukuma maendeleo katika majimbo yao, kwa sababu sote ni mashuhuda pale ambapo hufanya mambo mazuri tu na yanayoifanya serikali ionekane kwamba inapiga hatua.

Mhe. Naibu Spika, serikali imefikiria kuleta mswada huu kwa umakini kabisa, na sababu ya msingi ni kuwajenga uwezo wananchi na kuwapa nafasi ya kujenga imani ndani ya serikali yao ili kuwaondolea yale matatizo ambayo yalikwishajengeka katika visiwa hivi, kwamba watu wanafanya wanavyotaka na wanapofika Mahakamani unakosekana ushahidi wa kutosha na wahalifu wanaendelea kujivuna. Kwa hiyo, nachukua nafasi hii kumpongeza Mhe. Waziri, kwa kuleta mswada huu ambao kwa namna moja au nyengine umejenga maelewano makubwa kati ya polisi na waendesha mashtaka ambao kwa muda mrefu tumekuwa tukiona wananchi wanakosa haki zao.

Mhe. Naibu Spika, hoja hii ni hoja ambayo kwa Wazanzibari na Watanzania wote ambao wanaishi hapa Zanzibar ni hoja ya msingi kabisa ambayo kwa muda mrefu imekuwa ikifikiriwa namna gani serikali inaweza kupata ufumbuzi wa kuliondoa tatizo hili la udhalilishaji na hatimaye kuweza kuleta nafasi ya uhakika kama vile ambavyo Wazanzibari wamezowea.

Mhe. Naibu Spika, si vibaya kwa watu kama hawa ambao kwa makusudi wamejenga utaratibu wa kuweza kudhalilisha vijana wetu au kuendesha vitendo vya ubakaji pale wanapokamatwa basi kwanza ni vizuri wakapelekwa Soba ili warekebishwe kwanza akili zao. Kwa sababu vitendo hivi havimpelekei mtu mwenye akili kuvifanya bali huwa ni mtu ambaye tayari ana *mental problem,* ama ana *mental disease,* ama ana *mental disturbance* zinazomchanganya mpaka kufikia hatua ya kufanya hivyo.

Mhe. Naibu Spika, Uengereza mtu akishashindwa na jambo la maana la kufanya basi mwenyewe huwa anajipeleka *Sober* kwa ajili ya kuweka akili yake vizuri. Sasa na hawa wenzetu ambao kwa makusudi wanaendesha haraka hizi wao wenyewe hawawezi kwenda *Sober,* lakini ni vizuri wakapelekwa *Sober* kwa makusudi wakishakuwa makini ndio wakaanza kupelekwa Mahakamani na hakuna haja ya kwenda pale wakaanza kuyumbishana kati ya polisi na muendesha mashitaka. Kimsingi ni kwamba pale sasa hivi ushahidi ambayo tayari umepatikana na ambao umeelezwa kwa yakini kabisa kwamba utawaondolea matatizo wananchi, basi hakuja haja ya kuchukuwa muda. Ni vizuri kesi hizi kwa wingi sana zikachukuwa wiki moja tu.

Kwa hiyo, nawashauri majaji kwamba ule wakati wa kuwasumbua Wazanzibari kwa kutafuta ushahidi huu na ule umekwisha na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imetengeneza hoja hii kwa makusudi ili kuwaondolea matatizo Wazanzibari juu ya kadhia hii ambayo imezuka hapa visiwani Unguja na Pemba.

Mhe. Naibu Spika, katika mazingira ya kujenga umoja wa Wazanzibari nidhamu na utamaduni wetu wa asili lazima uendelezwe katika mazingira mbali mbali ili kuwafanya Wazanzibari waendelee kuishi katika nchi yao kwa amani na utulivu. Kutokana na sheria hii nina imani kabisa kwamba yale ambayo tunayazoea Wazanzibari katika miaka mingi iliyopita ya kuliona suala hili kwamba ni suala baya, nina imani hoja hii ya kudhalilishwa itamalizika mara moja katika maisha haya tunayokwenda, kwa sababu utaratibu wa kutoa ushahidi Mahakamani umekuwa ni wa urahisi mno kiasi kwamba kila mtu anaweza kwenda kutoa ushahidi, kila mtu ana uwezo wa kuweza kuwasilisha ushahidi kwa njia moja hata ya kielektroniki ilimradi ushahidi utakuwa ni ushahidi na suala hili litakuwa halina mjadala.

Kwa hiyo, tunatoa wito sisi kama serikali kwa wale Polisi wababaishaji ambao kwa makusudi huwasumbua wananchi katika hoja kama hizi na kwa wale majaji ambao kwa makusudi huwa tayari wanachukuwa rushwa ili kuzibabaisha kesi kama hizi wawe tayari kwamba serikali haitakuwa tayari kwamba kesi hizo zinapotezwa, zinaambiwa hazina ushahidi, hili suala hatutakubaliana nalo. Kwa hiyo, nasema kwamba majaji pamoja na Polisi wawe tayari kuhakikisha wanafanyia haki Wazanzibari kwa mujibu wa sheria na taratibu za nchi.

Mhe. Naibu Spika, ninachokiomba kwa Wawakilishi wote sasa hivi ni kwamba sote kwa pamoja tukubaliane kuupitisha mswada huu ili nchi yetu itoke hapa ilipo na isogee mbele kwa faida ya wananchi waliotuchangua.

Baada ya hapo Mhe. Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia chini ya mia na naamini wenzangu wote wamesema hivyo, kwa vile ni suala la kusema tu kwamba mswada huu umeshapita. Ahsante Mhe. Naibu Spika. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, na mimi nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kunijaalia kusimama leo hii na mimi kupata wasaa wa kuchangia mswada wetu huu wa Sheria ya kufuta na kuandika upya sheria ya ushahidi.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli ujaji wa mswada huu kuwa sheria ni kilio cha muda mrefu sana kwa sababu wananchi wetu walikuwa wakipiga kelele juu ya suala zima la ushahidi hususan unawahusu watoto kule mahakamani. Kwa hivyo, kuja kwa sheri hii kwa upande mwengine naweza kusema kwamba ni ukombozi sasa hivi kwa Wazanzibari na vile vile kuja kwa sheria hii baada ya kusainiwa utakuwa vile vile ni pigo kwa wale watu wote ambao wanaofanya

vitendo viovu kwa watoto wetu na wakachukulia ule udhaifu wa kwamba ushahidi wa watoto mbele ya Mahakama unakuwa hauna uzito sana kwa njia moja au nyengine.

Kwa hivyo, kwa kuja sheria hii kutawezesha watoto kuendelea kupata haki yao ya msingi na vile vile wale wote ambao wenye nia ya kuwahujumu watoto hivi sasa baada ya kusainiwa sheria hii itakuwa mwisho wao umefika. Sasa niombe wananchi wote wa Zanzibar wakiwemo wananchi wa Jimbo langu la Pangawe kwa sababu miongoni mwa wananchi ambao waliokuwa wakipiga zogo sana suala hili la kuwa ushahidi ambao unaopelekwa kule Mahakamani wakati mwengine ambao unahusu watoto unakuwa kidogo ni dhaifu kiasi ambacho haki za watoto zinakuwa hazipatikani.

Sasa wananchi wote wa Zanzibar niwaombe kwamba sheria hii tukijaalia itasainia akipenda Mwenyezi Mungu hivi karibuni na Mhe. Rais, lakini kusainia kwa sheria hii ni jambo moja kama walivyoeleza wenzangu lakini utelezaji wa sheria hii ni jambo jengine, tunapozungumza utekelezaji wa sheria hii sio kwa maana tunakusudia hii wizara au serikali, lakini pia wananchi kutoka ngazi za chini wao ndio miongoni mwa watekelezaji wa sheria hii.

Kwa hivyo, sheria hii ili iwe nzuri katika utekelezaji wake lazima wananchi wa Zanzibar tushirikiane kwa pamoja kuhakikisha kwamba tunatoa ushahidi tunapoitwa mahakamani, kwa sababu imezoeleka katika baadhi ya jamii zetu Zanzibar hususan katika yale masuala ambayo yanayohusu watoto matendo ambayo wanaofanyiwa watoto huwa wananchi baadhi yao wanamalizana huko huko mitaani.Jambo ambalo kwa kufanya hivyo unakuwa humtendei haki yule mtoto kwa sababu mtoto haki unapoivunja jua kwamba unampa adhabu na inawezekana ikawa ni sababu ya kutofanikiwa kwake katika maisha.

Kwa sababu mtoto anapofanyiwa jambo baya na hawa watendaji wa matendo haya kwa watoto basi suala lile inawezekana yule akawa na kumbukumbu nalo na vile vile wakati mwengine wakati alipokuwa akifanyiwa kitendo kile anafahamu basi wakati wote anakuwa anaona haya hususan pale ambapo anakutana na watoto wenzake au anapokutana na wananchi wengine.

Kwa hivyo, wito wangu kwa wananchi wote wa Zanzibar tushirikiane kwa pamoja kuhakikisha kwamba wale ambao wanawahujumu watoto wetu basi tushirikiane kwa pamoja kuhakikisha kwamba watu hawa wote wabaya wanafikishwa mahakamani na vile vile tuwe tayari tunapoitwa mahakamani kutoa ushahidi. Kwa sababu unapotoa ushahidi mahakamani ni sababu kuu ambayo inaweza ikapelekea yule mtoto kupa haki yake hiyo. Kwa hivyo, ni

vyema tujitahidini katika kutakikisha kwamba tunapohitajika mahakamani kutoa ushahidi tuwe tunatoa huo ushahidi.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine, suala la watoto katika upande wa Mahakama. Limezungumziwa na Waheshimiwa Wawakilishi mbali mbali kwamba ni vyema Mahakama zetu zikawa zinafanyakazi kubwa kuhakikisha kwamba zinalinda haki za watoto. Vile vile, kwa upande wa Mahakama Mhe. Naibu Spika, kwamba hivi sasa hivi tuna Mahakama ya watoto pale Vuga, lakini Mhe. Naibu Spika, kama unakumbuka hivi karibuni Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, pia alizindua lile jengo la Mahakama ya Chake Chake Pemba, lakini ndani yake ikiwemo hii Mahakama ya watoto.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, tunaenda vizuri tu kuhakikisha kwamba watoto wetu wanalindwa na sheria mbali mbali. Kwa hivyo, kila mazingira ambayo yatampelekea mtoto kulindwa tunahakikisha kwamba tunayaboresha ili mtoto aweze kupata haki yake kamili. Sambamba na hilo, Mhe. Naibu Spika, hivi sasa tuna jengo la Mahakama ya watoto ambako lipo Mahonda, jengo hili karibuni *Inshaalla* Mhe. Rais, atapata fursa ya kwenda kulizindua. Sasa umalizikaji wa jengo hili la Mahakama ya watoto vile vile itatuzidishia nguvu zaidi kulinda haki za watoto na wale wabaya wote kuhakikisha kwamba wanapewa adhabu ya kutosha.

Mhe. Naibu Spika, naomba pia nitumie fursa hii kuwaomba majaji, mahakimu wa Mahakama zetu kwamba wanapoletewa yale masuala mbali mbali hususan yanayohusiana na watoto kama sheria itakuwa inatoa adhabu kwa mfano kutona mwaka mmoja hadi miaka minane, basi ni vyema Waheshimiwa hawa wakakiangalia hicho kifungo kikubwa zaidi kuwapa hawa wafujaji wa watoto wetu ili iwe ni dawa na funzo kwa wote ambao wanafanya matendo haya na wale watakao kuwa na nia ya kufanya matendo haya bila shaka watasita kufanya matendo haya.

Mhe. Naibu Spika, suala la elimu vile vile limetolewa kwamba ni vyema tukazidisha elimu. Hilo tumelichukuwa na elimu itazidi kutolewa na pamoja na watu wengine kuhakikisha kwamba mahakimu na majaji vile vile elimu iweze kutolewa kwa Afisi ya *DPP* na Polisi pamoja na wadau wote ambao wanahusika kwa njia moja au nyengine na suala hili la watoto.

Mhe. Naibu Spika, kwa hayo machache niseme kwamba niwaombe Waheshimiwa Wawakilishi, tuunge mkono mswada wetu huu ili iwe sheria. Kwa hayo, machache naomba kusema kwamba naunga mkono mswada huu asilimia mia juu ya mia. Ahsante. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spia: Ahsante Mhe. Naibu Waziri, sasa nitampa nafasi Mhe. Waziri, aje ili aweze kujibu hoja za Wajumbe. Mhe. Waziri, karibu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, naomba kuchukuwa nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia tena kukutana jioni hii ya leo kwa ajili ya kukamilisha kazi yetu muhimu hii ya taifa.

Mhe. Naibu Spika, nimebahatika kupata wachangiaji 18, wachangiaji 14 wamechangia kwa kusema, wachangiaji 4 wamechangia kwa maandishi. Naomba kwa ruhusu yako...

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa Waziri, naomba nikukatishe nina wachangiaji wengine wanne ambao wameleta sasa hivi wamechangia kwa maandishi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi na Utawala Bora: Sasa mimi madhali sijapata, kwanza nitashindwa kufanya majumuisho kwa sababu sikupata taarifa zao. Sasa watambulikane tu wako na wanne sasa majina yao siyajui Mhe. Naibu Spika, labda utanisaidia baadae kuwataja. Watajwe wanne kwenye *Hansard* ili wajulikane na wao kwamba wamechangia, mimi nitawaja hao wengine halafu...

Mhe. Naibu Spika: Naomba mpelekee Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi na Utawala Bora: Lakini wanisamehe waliyoyaandika sitoweza kuyafanyia majumuisho kwa sababu ndio nimeyapata sasa hivi.

Mhe. Naibu Spika, naomba kwa ruhusa yako niwataje hao waliochangia waliowahi mapema. Kwanza namshukuru sana Mhe. Machano Othman Said Mwenyekiti wa kamati ya Katiba, Sheria na Utawala. Pia, nawashukuru:

Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)
Mhe. Mgeni Hassan Juma
Mhe. Rashid Makame Shamsi
Mhe. Naibu Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na watoto
Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali
Mhe. Suleiman Sarahan Said
Mhe. Omar Seif Abeid
Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame

Mhe.Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na watoto
Mhe. Waziri wa Ardh, Maji, Nishati na Mazingira
Mhe. Said Soud Said (Waziri asiekuwa na Wizara)
Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma

Waliochangia kwa mandishi mapema ni kama hawa wafuatao:

Mhe. Mohammed Said Mohamed (Dimwa)
Mhe. Mtumwa Peya Yussuf
Mhe. Zaina Abdalla Salum
Mhe. Bahati Khamis Kombo

Wengine walichangia kwa maandishi ambao sijayasoma ni:

Mhe. Said Omar Said
Mhe. Tatu Mohamed Ussi

Mhe. Naibu Spika, hii moja naona haina jina
Mhe. Naibu Spika, na hii pia haina jina.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa, ameandika jina lake ni Mhe. Saada Ramadhan Mwenda, limo jina lake humo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, hamna jina humu, Mheshimiwa wa Wingi huyu ameandika yeye na Mhe. Saada R. Mwenda. Hawa wote wamechangia sasa hivi kwa maandishi Mhe. Naibu Spika. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, nichukuwe nafasi hii kuwashukuru waliochangia wote. Kwa kweli Msaada huu umepata bahati moja kubwa umechangiwa sana kwa kupewa ushauri na sisi kama ni Wizara ya Katiba, Sheria na Utawala Bora tutakahikisha kwamba ushauri tulioupata wote tunauchukuwa na tunakwenda kuufanyia kazi kidhati kabisa.

Mhe. Machano Othman Said, tunamshukuru sana katika kamati alifanya kazi kubwa sana kiasi ambacho kwamba mambo mengi aliyotueleza tumeyachukuwa kwenye kamati tumeyafanyia marekebisho na si haba tumashukuru kwamba yamesaidia sana kufanya mswaada wetu huu kuwa bora zaidi.

Lakini pia alitoa ushauri mzuri sana kwamba sheria zote sasa hivi kuna haja ya kuzipitia tena na kuona kwa kiasi gani tunaweza kuzifanya marekebisho. Ni kweli sheria nyingi zimepitwa na wakati na nichukuwe nafasi hii kumshukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali amefanya jitihada kubwa sana ameorodhesha sheria zote karibu 385 zilizokuwepo sasa hivi na kuwapeleka sekta husika wizara zote ili kila mmoja aangalie sheria gani inahitajia kufanyia marekebisho na yeye Mwanasheria Mkuu ameshauri zile sheria ambazo zifanyiwe marekebisho basi zote amezitaja mle hii iangaliwe na inahitajiwa kufanyiwa marekebisho. Mhe. Mwanasheria Mkuu, tunakushukuru sana kwa kazi nzuri. (*Makofi*)

Lakini pia Mhe. Machano Othman Said, alishauri vile vile tufanye semina kwa taasisi mbali mbali ambazo zitakuwa zinasimamia sheria hii vyombo vyote Mahakama, Afisi ya Mwanasheria Mkuu kwa *DPP* na jengine zote tutajitahidi kupitia wizara yetu kusimamia jambo hili ili jambo hili lifanyike.

Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata), amechangia kitu kimoja muhimu sana, amesema jambo hili ni muhimu na limetimiza miaka mia sasa hivi na akamuomba Mhe. Rais, kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, kwa kupitia kwa Mhe. Spika, asubuhi kwamba ni vyema sheria hii ikasainiwa Januari 2017, uamuzi huu ni wake mwenyewe Mhe. Rais, sisi tutampelekea maombi tuone kwa kiasi gani hilo litawezekana. Mimi nina hakika Mhe. Rais, hatokaa jambo hilo kwa sababu sheria imeshatimiza miaka mia na atasaini tukijaaliwa.

Jengine Mhe. Ali Suleiman Ali amezungumza suala zima juu ya Sheria ya watoto alikuwa mkali sana kuona kwamba watoto wanadhalilishwa na hawatendewi haki. Mhe. Naibu Spika, sheria hii imekuja kwa sababu ya kudhibiti mambo hayo na tutahakikisha kwamba sheria hii inapewa meno na inafanyakazi yake vizuri wale, wote watakaokamatwa katika jambo hili baya wanalolifanya si kwa watoto tu, kwa walemavu, na wengine akinamama na wengine wote, hata kwa watoto wa kiume basi wote watashughulikiwa ipasavyo kwa mujibu wa sheria hii. (*Makofi*)

Mhe. Mgeni Hassan Juma, tunakushukuru sana kwa mchango wako mzuri. Mhe. Ali Suleiman Ali, samahani alisema wanaofanya makosa haya wapigwe viboko. Sasa Mhe. Ali Suleiman Ali, nikurudishe nyuma kidogo kwamba Sheria ya Viboko ya adhabu ya viboko imeshaondoshwa sasa hivi. Ninapenda kumjuulisha Mhe. Mjumbe kwamba, Sheria yetu ya ya Mwenendo wa Adhabu Nam. 6 ya 2004 imefuta adhabu ya viboko. Haipo sasa hivi lakini Sheria hii imepewa meno ya kuchukuliwa hatua za kufaa kwenye Mahakama zetu.

Mhe. Mgeni Hassan Juma, amesema sana na wengi wamesema jambo hili kwamba tujitahidi kutoa elimu juu ya jambo hili kwa sababu ni jipya. Pia, amezungumza suala la Mahakama Maalum ya Watoto, amezungumzia suala la ushahidi wa daktari na suala la *DNA*.

Mhe. Mgeni, ninakushukuru kwa mchango wako. Ninapenda kukuhakikishia kwamba elimu itatolewa kwenye vyombo vyote na taasisi zote juu ya jambo hili. Lakini kuhusu Mahakama ya Watoto Mhe. Mgeni, kwa taarifa yako jambo hili limeshachukuliwa hatua Mahakama ya Vuga na Chake Chake Pemba, zipo tayari Mahakama hizi Maalum kwa ajili ya Watoto. Na chombo cha *DNA* tutakaa na taasisi inayohusika ili kuona kwa kiasi gani jambo hili tunalifanyia kazi kwa pamoja. Ni chombo muhimu na kinataka kufanyiwa kazi.

Mhe. Rashid Makame, tunakushukuru sana kwa mchango wako mzuri. Elimu itolewe kama nilivyosema ni jambo zuri itolewe elimu kwa kutumia vyombo hivi vya elektroniki. Mashahidi wawezeshwe kimaslahi. Tumelisikia pia tuandike tafsiri kwa *alphabetical order*, tumechukua hilo na tutalirekebisha. Uadilifu kwa watendaji hili ni jambo muhimu sana.

Hii ni Wizara ya Utawala Bora na ndiyo maana yake Waheshimiwa mutakumbuka tutakuwa na semina ya maadili hapa katika wiki hizi zinazokuja. Kwa hivyo, suala la maadili ni lazima na watendaji wa Ofisi hizi lazima wawe na ukweli, wawe wawazi na wahukumu kwa mujibu wa sheria zilivyo, watende haki. Kwa hivyo, suala la maadili litapewa uzito mkubwa sana. (*Makofi*)

Mhe. Shadya, ameunga mkono na yeye lazima aunge mkono kwa sababu watoto wapo chini ya Wizara yake. Tunakushukuru sana kwa mchango wako mzuri.

Mhe. Mmanga, umezungumzia zaidi kuhusu kujenga maadili. Jeshi la Polisi, *DPP*, watendaji wengine watumie majukumu yao kwa ufanisi na kwa uledi. Umesema vile vile Mhe. Mmanga, kwamba tutumie njia nyengine za utoaji wa elimu ya jamii juu ya sheria badala ya vyombo vya habari. Sasa bahati mbaya umesema tusitumie vyombo vya habari lakini hukutoa ushauri tufanye nini. Kwa hivyo, *In shaa Allah* tukijaaliwa ukipata wasaa tukutane utushauri tufanye vipi katika njia nzuri zaidi. Kwa sababu sisi tunatumia vyombo vya habari, tunatumia viongozi wetu katika maeneo yetu mbali mbali; kwenye Shehia zetu kwa Masheha na viongozi wengi.Tutajitahidi kushirikiana na viongozi katika maeneo hayo ya Shehia na mengine ili tuweze kutoa taaluma hiyo.

Mhe. Suleiman Sarahan Said, alikuwa na mambo mengi ya kuzungumza. Mhe. Sarahan, alisema Serikali ifanye juhudi za ziada za kuimarisha Sheria ya Kumlinda Mtoto chini ya umri wa miaka 18. Pia, wahudumu wa kuwahoji watoto kutotumia vitisho au lugha kali wanapowahoji watoto.

Zitungwe Kanuni za wanawake wanaozurura usiku. Anaomba Serikali ifuatilie kuhusu la nyumba ya Maisara inayosadikiwa kuwa ni ya maovu. Majaji wafanye uadilifu kwa mujibu wa kazi ya Serikali, hilo limeshalijibu. Lakini kuhusu Mhe. Sarahan, anaomba Mhe. Naibu Spika, kwa kupitia kwako kwamba Sheria ya Kumlinda Mtoto tayari Serikali imeshapitisha Sheria Nam. 6 ya 2011. Na kuhusu utaratibu wa kuwahoji watoto tayari sheria hii mpya ya ushahidi imeyazingatia hayo, sina wasi wasi.

Kuhusu suala la uadilifu wa Majaji. Tayari nimeshalitolea ufafanuzi juu ya suala hilo, kuwepo kwa nyumba ya Maisara inasadikiwa inatumika kwa matendo maovu. Hiyo sisi hatuna taarifa nayo, lakini tutashirikiana na vyombo vinavyohusika kuona kwamba kama nyumba hiyo ipo ili tuchukue hatua za kufaa.

Kuhusu haja ya kutunga Kanuni za kudhibiti wanawake wanaozurura ovyo usiku Mhe. Naibu Spika, suala la uhuru wa kutembea ni la Kikatiba kwa mujibu wa Kifungu cha 16 (1) cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984. Hivyo, ni vyema jamii ikafuatilia nyendo za vijana wetu ili wasiitumie vibaya uhuru huo. Kwa hivyo, ni jambo letu wenyewe lipo kwenye dhamana yetu, kila mmoja ni dhamana ya jambo hili, tusingojee Serikali. (*Makofi*)

Mhe. Omar Seif, alishauri tuwe na watumishi walio waadilifu, nimeshalizungumza suala hilo na ndiyo maana yake tuna Tume hii ya Maadili imekuja kwa suala la kujenga maadili yetu mazuri. Na asiwe na wasi wasi suala hili tutalishughulikia kwa mujibu wa sheria.

Pia, Mhe. Naibu Spika, tulipata mchango wa Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame. Dkt. Mwinyihaji, alizungumza juu ya masuala yafuatayo. Sababu za watu kutokutoa ushahidi Mahakamani, ni kitu gani hawataki kwenda. Tafsiri ya Mahakama, Ofisa wa Balozi ngazi gani ni *qualified* na *competent* kwa kuchukua maelezo, *the rule of law* Zanzibar. Masuala hayo ndiyo ya kimsingi aliyozungumza Mhe. Dkt. Mwinyihaji. Ninamshukuru sana kwa masuala yake.

Sababu za watu kutotoa ushahidi ni pamoja na muhali uliopo katika jamii. Muhali umetujaa sana ndani ya jamii yetu. Lakini pia hofu wakati mwengine, mtu anaogopa, kukataa tamaa mapema na hata utamaduni wetu pia nao unaleta

matatizo. Tafsiri ya Mahakama tayari imeshafanywa tafsiri katika Kifungu cha 3 cha Sheria hii. Kwa utaratibu wa sasa Ofisa wa Polisi ana uwezo wa kuchukua maelezo ya mlalamikaji katika vituo vyetu vya Polisi.

Kuhusu haja ya kusimamia utawala wa sheria. Serikali inaendelea na hatua mbali mbali za kuhakikisha kwamba nchi yetu inaongozwa kwa kufuata utaratibu wa sheria ikiwa ni pamoja na kuanzisha mamlaka mbali mbali, ikiwemo Idara ya Utawala Bora. Na bahati nzuri Mhe. Dkt. Mwinyihaji, mwenyewe alikuwa Waziri ambaye anayehusika na utawala bora, haya mambo anaelewa. Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Hujumu wa Uchumi pamoja na Tume ya Viongozi nazo zimeundwa kwa ajili ya jambo hilo.

Tulipata mchango mkubwa sana kutoka kwa Mhe. Mohamed Said Mohamed.Naomba nimshukuru, ninapenda nimuhakikishie kwamba maelezo yake aliyotoa yote ya marekebisho ya vifungu mbali mbali vya 87 mpaka 108 tumeyachukua na asiyiwe na wasi wasi kwa uadilifu tutayafanyia kazi ili tuweze kuchukua hatua.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo mafupi naomba kutoa hoja sasa. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, Mhe. Waziri, ameshatoa hoja, sasa niwaulize wale wanaoukubaliana na hoja hiyo wanyooshe mikono, wanaokataa.Wanaokubali wameshinda. (*Makofi*)

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, sasa naomba kutoa taarifa kwamba Baraza lako likae kama Kamati ya Kutunga Sheria ili kuupitia Mswada huu kifungu baada ya kifungu.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, tutapitisha Mswada wetu kwa mafungu. Kwa hivyo, kama kutakuwa na mtu ana hoja yake ndani ya mafungu yale, ataiangalia vizuri na atasimama kwa ajili hoja yake, sawa.

KAMATI YA KUTUNGA SHERIA

Mswada Wa Sheria Ya Kufuta Na Kutunga Mpya Sheria Ya Ushahidi Sura Ya Tano Na Masuala Yanayohusiana Na Hayo Pamoja Na Marekebisho Yake

Sehemu ya Kwanza - Vifungu vya Awali

Sehemu ya Pili	-	Uhusiano wa Matukio
Sehemu ya Tatu	-	Kukubali
Sehemu ya Nne	-	Maungamo
Sehemu ya Tano	-	Maelezo ya Watu ambao Hawawawezi Kuitwa kama Mashahidi
Sehemu ya Sita	-	Maelezo yaliyofanywa kwenye mazingira maalum pamoja na marekebisho yake
Sehemu ya Saba	-	Hukumu za Mahakama wakati zinapohusika pamoja na marekebisho yake
Sehemu ya Nane	-	Maoni ya Mtu watatu yanapohusika pamoja na marekebisho yake
Sehemu ya Tisa	-	Wakati Tabia zinapohusika bila ya marekebisho
Sehemu ya Kumi	-	Matukio ambayo hayahitaji kuthibitishwa
Sehemu ya Kumi na Moja	-	Ushahidi wa Mdogo pamoja na marekebisho yake
Sehemu ya Kumi na Mbili	-	

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Mwenyekiti, nilimsikiliza sana Mhe. Waziri, na wakati nikichangia au nililetea *schedule of amendment*, lakini akiniambia zitazingatiwa. Sasa nina uzoefu mkubwa sana wa kukaa na Warabu kule Chuo Kikuu, walikuwa wakikwambia *inshaallah*. Sasa hujui *inshaallah* utapata au *in shaa Allah* hupati.

Sasa nilikuwa ninataka kujua tu marekebisho yangu...

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa, naomba ueleze ni kifungu cha ngapi.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Kifungu cha 87. Nilileta *schedule of amendment.*

Mhe. Mwenyekiti: Hatujafika huko Mheshimiwa.

Sehemu ya Kumi na Mbili	-	Ushahidi wa Waraka pamoja na marekebisho yake
Sehemu ya Kumi na Tatu	-	Nyaraka za Umma pamoja na marekebisho yake

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Mwenyekiti, nilileta marekebisho au *schedule of amendment* katika Kifungu cha 87. Sasa nimemsikiliza vizuri sana Mwalimu wangu Mhe. Haroun Ali Suleiman, akisema kwamba atayazingatia

na nina uzoefu mkubwa wa kukaa na Warabu wanasema *in shaa Allah*, sasa *in shaa Allah* sijui nimepata au nimekosa. Naomba ufafanuzi.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, mimi siyo Muwarabu, yeye kakaa na Waarabu. Mimi ni Mzanzibari, Mtanzania na Mmakunduchi.

Sasa nilichosema ni kwamba kwa sababu tayari Kamati hii ya Katiba na Sheria ambayo ni kamati yetu ya Baraza imetupa maelezo yake na marekebisho yake na yeye katuongezea mengine. Kwa hivyo, mimi sina wajibu wa kufanya hivyo moja kwa moja isipokuwa nitakaa na Kamati yangu ya Katiba na Sheria tena tutizame hayo aliyotuletea lakini tutayaangalia na tutayazingatia.
Lakini mimi si Muwarabu.(*Makofi*)

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Mwenyekiti, nimemfahamu sana Mhe. Waziri, na kikubwa hapa tunatunga sheria. Na mimi ni Mjumbe ambaye ninataka kujua *schedule of amendment* ambayo nimeileta. Nilizingatia na kufanya kazi kubwa sana. Ukiniambia unakwenda kukaa na Kamati, sijajua inapita au haipiti. Nitajuaje kama huko itakuwa itapita havipiti vitu vyangu ambavyo nimevileta.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu ambayo ameyatoa Mhe. Waziri, labda tu niongezee kwenye Kifungu cha 87 ambacho Mhe. Mohamed Said Mohamed, ameleta jadweli lake la marekebisho.

Kwenye Kifungu hichi Mhe. Mwenyekiti, kubwa ambalo Mhe. Mohamed Said Mohamed, amefanya ni kuweka lugha sawa. Sasa hilo kwanza nimshukuru kwa kuweka hiyo lugha sawa, lakini nimwambie kuwa Kifungu hichi na marekebisho yake ambayo ameya-*propose* tunakubaliana nayo. (*Makofi*)

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Sehemu ya Kumi na Mbili	-	Ushahidi wa Waraka pamoja na marekebisho yake
Sehemu ya Kumi na Tatu	-	Nyaraka za Umma pamoja na marekebisho yake
Sehemu ya Kumi na Nne	-	Dhana juu ya Nyaraka pamoja na marekebisho yake

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Mwenyekiti, na hapa katika ukurasa huu Kifungu cha 90 nilileta vile vile *schedule of amendment*. Ninataka niekewe wazi au ninataka kidogo waniambie imekubaliwa au haikukubaliwa.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, hakuna matatizo hili suala hata mimi nina uwezo nalo la kulikubali, halina matatizo tutarekebisha. (*Makofi*)

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Sijalisikia uzuri.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri, anasema hajasikia vizuri.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, sasa mimi mrefu jamani ninakuomba siwezi kuinama sana hivi kwenye hii *microphone*.

Mhe. Mohamed Said Mohamed, ninasemaje kwamba marekebisho yako mimi nimeyakubali na tutayarekebisha kama ulivyopendekeza, haina matatizo. (*Makofi*)

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Sehemu ya Kumi na Nne	-	Dhana juu ya Nyaraka pamoja na marekebisho yake
Sehemu ya Kumi na Tano	-	Hati pamoja na marekebisho yake
Sehemu ya Kumi na Sita	-	Jukumu la Kuthibitisha
Sehemu ya Kumi na Saba	-	Zuio
Sehemu ya Kumi na Nane	-	Mashahidi pamoja na marekebisho yake
Sehemu ya Kumi na Tisa	-	Mahojiano na Mashahidi pamoja na marekebisho yake
Sehemu ya Ishirini	-	Kukubali Kusiko Sahihi na Kukataliwa Ushahidi pamoja na marekebisho yake

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, ilivyokuwa Kamati ya Kutunga Sheria umeupitia Mswada wangu Kifungu kwa Kifungu na kukubali pamoja na marekebisho yake, sasa naliomba Baraza lako Tukufu liukubali. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, Mhe. Waziri, ameshatoa hoja, sasa niwaulize wale wanaokubaliana na hoja wanyooshe mikono, wanaokataa. Wanaokubali wameshinda. (*Makofi*)

MSWADA WA SHERIA YA USHAHIDI YA MWAKA 2016

(Kusomwa kwa Mara ya Tatu)

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja kuwa Mswada wa Sheria ya Ushahidi ya 2016 usomwe kwa mara tatu. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, Mhe. Waziri, ameshatoa hoja, sasa niwaulize wale wanaokubali wanyooshe mikono, wanaokataa. Waliokubali wameshinda. (*Makofi*)

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)
(Muswada wa sheria ya Serkali ulisomwa kwa mara ya tatu na kupitishwa)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, shughuli za leo zimefikia hapa, zimefikia mwisho. Kwa hivyo, nimtakie Mhe. Waziri, kila kheri utekelezaji uliotukuka bora na niwashukuru Wajumbe wote ambao wamechangia Mswada huu. Na ninatarajia kwamba Mswada huu utaleta matumaini katika jamii yetu.
Baada ya kusema hayo naahirisha Kikao Waheshimiwa Wajumbe hadi kesho tarehe 24/11/2016, saa tatu asubuhi.

(Saa 12.05 jioni Baraza liliahirishwa hadi
tarehe 24/11/2016 saa 3.00 asubuhi)